**BUNGE LA TANZANIA**

**MKUTANO WA SABA**

# MAJADILIANO YA BUNGE

**Kikao cha Pili – Tarehe 11 Aprili, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Biashara ya Nje *(BET)* kwa mwaka 2003/2004 *(The Annual Report and Accounts of the Board of External Trade (BET) for the year 2003/2004).*

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita atakayeuliza swali la kwanza, napenda kusema kwamba tunayo maswali 16. Kwa hiyo, ni dhahiri, tukichukua nyongeza nyingi ama ndefu, itakuwa vigumu kumaliza yote na si vizuri tukaendelea kuwa tunaahirisha majibu. Kwa hiyo, nitakwenda haraka kidogo na kwa utangulizi huo, sasa naomba Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake ambalo linaelekezwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Na. 14

### Vita Dhidi ya UKIMWI

**MHE. BAHATI ALI ABEID** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu inaendelea kupambana na Ugonjwa wa UKIMWI ili upungue na hatimaye kumalizika kabisa; na kwa kuwa kuna *NGOs* zinatoa elimu juu ya

kujikinga na UKIMWI na elimu kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI ili waendelee kuishi kwa matumaini na bila ya kueneza kwa wengine:-

(a) Je, kuna *NGOs* ngapi zinazofanya kazi ya kuelimisha hadi vijijini?

(b) Je, takwimu za Serikali zinaonesha kuwa UKIMWI unapungua au unaongezeka?

(c) Je, katika Mikoa ambayo takwimu zinaonesha kuwa wameathirika zaidi Serikali imeweka mikakati gani ya kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, takwimu kutoka kwa Wakala wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI wa Mikoa, zinaonesha kwamba hadi kufikia Machi, 2007, asasi zisizo za Kiserikali *(NGO)* zipatazo 4,500 zimekuwa zikitoa huduma katika Mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mikoa inayoongoza kwa kuwa na asasi hizo kwa wingi ni Dar es Salaam, Iringa, Pwani, Mwanza, Mbeya, Ruvuma, Tanga na Shinyanga. Mikoa yenye idadi ndogo ya asasi hizi ni Manyara, Rukwa, Kigoma, Tabora, Lindi na Singida. Sababu kubwa kwa mikoa hii kuwa na idadi ndogo ya asasi hizi ni ugumu wa mawasiliano ya barabara na mwamko mdogo wa wananchi kuanzisha asasi hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na utafiti uliofanyika kuanzia Desemba, 2003 hadi Machi, 2004, kiwango cha UKIMWI nchini kwa jamii yote na hasa umri wa miaka kati ya 15 - 49 ni asilimia saba. Kiwango hiki kinatofautiana kufuatana na jinsia, ikiwa ni asilimia 7.7 kwa wanawake na asilimia 6.3 kwa wanaume. Kiwango hiki pia kinatofautiana kwa mjini, kiwango ni asilimia 10.9 na vijijini ni asilimia 5.3. Pia kulikuwa na tofauti ya elimu. Kwa wale wenye elimu chini ya elimu ya sekondari kiwango kilikuwa ni asilimia 5.3 na kwa wale waliopata elimu ya sekondari na kuendelea kiwango kilikuwa asilimia 8.2. Kimkoa, kulikuwa na tofauti, mikoa inayoongoza ni Mbeya asilimia 13.5, Iringa asilimia 13.4 na DSM ni asilimia 10.9%. Mikoa ambayo ina idadi ndogo ni Kigoma na Manyara, yenye asilimia mbili. Kutokana na takwimu hizi, hatuna ushahidi kwamba, kiwango cha UKIMWI kinapungua, tatizo bado ni kubwa na ili kupata usahihi wa hali halisi ya kiwango cha UKIMWI nchini utafiti mwingine utafanyika baadaye mwaka huu kuanzia Juni ili kuweza kuelewa hali halisi.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imelenga kudhibiti UKIMWI nchini kwa kuzuia wale wananchi asilimia 93, ambao hawajaambukizwa ili wasiambukizwe na pia kuwaelimisha juu ya ugonjwa wa UKIMWI, athari zake na jinsi ya kujikinga na pia kutoa tiba na matunzo kwa wale asilimia saba, ambao wamekwisha ambukizwa. Mikakati

iliyopo inalenga kuelimisha jamii juu ya athari, kinga na huduma zaidi kwa wananchi wote hadi vijijini. Vituo vya kuwahudumia wananchi kuhusu masuala ya UKIMWI vitaongezwa kutoka 200 vilivyopo sasa hadi 700 katika mwaka wa fedha ujao (2007/2008). Aidha, ushauri nasaha utaendelea kutolewa ili wananchi wengi zaidi wajitokeze kupima kwa hiari, kujua afaya zao na kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

Serikali pia itaimarisha mikakati ya kudhibiti UKIMWI mahali pa kazi *(Workplace Interventions),* mfumo wa ufuatiliaji na itafanya tathmini ya UKIMWI nchini, kama nilivyokwishasema hapo juu. Juhudi za kutafuta rasilimali zaidi za kutekeleza na kufuatilia mipango ya kudhibiti UKIMWI nazo pia zitaendelezwa.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, kwa kuwa azma ya Serikali ni kupambana na janga hili la UKIMWI na kwa kuwa swali langu mama linauliza zaidi hizi *NGOs* zinazofanya kazi ya kuelimisha mpaka vijijini; na kwa kuwa Naibu Waziri amejibu hapa kuwa *NGO* nyingi hazifiki vijijini kwa sababu ya barabara; je, Serikali ina mkakati gani wa kuziba mashimo barabara hizi angalau zipitike, hizi *NGOs* ziweze kufanya kazi mpaka vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, katika Ilani yetu ya mwaka 2005, Chama cha Mapinduzi kiliiagiza Serikali ya Awamu ya Nne, kuhakikisha ifikapo mwaka 2010 miundombinu ya mawasiliano na hasa barabara inaongezwa ili iweze kupitika kwa mwaka mzima na hivyo kuwawezesha wananchi wengi kufika mahali wanapotaka kwa mwaka mzima. Kwa hiyo, naamini ile kauli yetu haijabadilishwa na hata jana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu alijibu hivyo. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Tanzania ni moja kati ya nchi zilizoathirika sana na maradhi ya UKIMWI; na kwa kuwa Serikali pamoja na Taasisi mbalimbali huwa zinaweka mikakati maalum ya kupunguza ongezeko ya maradhi hayo; na kwa kuwa sababu kubwa inayosababisha ongezeko la maradhi hayo tunaielewa sisi Watanzania na watu wote duniani, kama huelewi tutakuelimisha baadaye; *(Kicheko)*

Je, hatuoni kwamba kuandaa baadhi ya vipindi vya matangazo katika vyombo vyetu vya habari hasa *Television,* huwa vinakiuka maadili kwa vile vipindi hivyo vinapooneshwa, vinaonesha vitu ambavyo watoto wasioelewa kunafanyika nini au kinaendelea nini, huwa tunapata mashaka majumbani tunaulizwa baba au mama kitu gani wanafanya wale watu ndani ya gari? Tangazo hili linamaanisha kwamba huyu bwana kamshikilia huyu mtu tufanye japo mara moja, ni ongezeko gani la UKIMWI linaweza kupunguzwa kwa njia ile; kwa nini tusiweke *Censor Board* ya kupunguza matangazo ambayo yanaashiria moja kwa moja na kuamsha hisia nyingine kwa watoto wetu walio wadogo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda niseme vipindi

vyote ambavyo vilikuwa vina matangazo ya kupotosha havipo tena. Kwa sasa hivi vipindi vilivyopo ni vile ambavyo vinalenga kuwafunza watu wa rika zote, namna ya kuepukana na maambukizi ya UKIWMI. Dunia hii ya utandawazi, vipindi hivyo vinavyoonesha ambavyo Mheshimiwa Mbunge anadai kwamba, vinakiuka maadili si vya hapa kwetu tu, ni dunia nzima. Tutaondoa programu moja ya hapa, kwingine watafungua wataona, lakini nina hakika kabisa kwetu sisi vipindi vya aina hiyo vya kutia aibu havipo tena.

Na. 15

**Barabara Kati ya Kasera na Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa ukosefu wa barabara kati ya Kasera, Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga, pamoja na Kata tano katika Tarafa ya Maramba ni kero kubwa kwa wananchi; na kwa kuwa wananchi hulazimika kusafiri kwa zaidi ya km 80 kwa gharama kubwa badala ya safari ya umbali ulio chini ya km 20 kutoka Kasera kupitia Mkinga - Magodi na Mwanyumba - Maramba, barabara ambayo ni nzuri zaidi na niliwahi kuipendekeza katika swali langu Na. 127 la tarehe 3 Julai, 2006; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ziara yake, aliwaahidi kuwa Serikali itajenga barabara hiyo haraka iwezekanavyo:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuchukua hatua zinazostahili dhidi ya tatizo hilo ili kuwaondolea kero wananchi walio kwenye maeneo inamopita barabara hiyo?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, mradi huo upewe kipaumbele cha juu kabisa hivyo utekelezaji wake uanze katika mwaka wa fedha wa 2007/2008?

(c) Je, ni lini hasa Serikali inakusudia kutekeleza mradi huo, utakaoamsha ari ya maendeleo kwa wananchi wa Wilaya ya Mkinga?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruku Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga, Kasera na Maramba. Barabara hii imefanyiwa uchunguzi wa awali, Makao Makuu ya Tarafa ya Maramba inapitia maeneo ya Kasera, Mkinga, Magodi, Mabokweni hadi Maramba. Barabara hii ina jumla ya urefu wa kilomita 50. Aidha, sehemu kubwa ya barabara hii ni tambarare, yenye kutoa

chemichemi wakati wa mvua. Pia maeneo ambayo barabara inapita ni ya udongo wa mfinyanzi kwa asilimia 50. Ujenzi wa barabara utajumuisha kunyanyua tuta la barabara na ujenzi wa madaraja manne katika maeneo ya Kombe Mwomongo, Kimunyu, Begeyu na Mwanumbu. Gharama za awali za barabara hii kwa kiwango cha changarawe, zinakadiriwa kufikia shilingi bilioni moja na milioni kumi.

(b) Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya maendeleo ya mwaka 2007/2008 ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, kwa kutumia fedha za *Local Government Capital Development Grant (LGCGD),* shilingi milioni thelathini za Kitanzania zitatumika kwa ajili ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya barabara ya Kasera na Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga.

(c) Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu utakapokamilika Serikali itafahamu gharama halisi zinazohitajika za matengenezo ya barabara hiyo na kupanga mipango ya utekelezaji wa ujenzi huo kadri hali fedha itakavyopatikana.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda nisisitize kwamba, hii barabara ni ya muhimu sana na napenda nipate taarifa kamili; je, ni lini hasa ujenzi utaanza kwa sababu haya ni maelezo ya matatizo ambayo hayana uhakika? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, kwa mwaka huu wa 2007/2008, fedha zimetengwa kwa ajili ya kufanyia upembuzi yakinifu. Upembuzi yakinifu ukishakamilika, barabara hiyo itawekwa kwenye mipango ya maendeleo na itajengwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Umuhimu wa barabara hii unafahamika na vipaumbele mara nyingi vinatolewa kwa zile Wilaya ambazo zimeanzishwa hivi karibuni.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hali ya barabara ya Kasela kule Mkinga inafanana kabisa na kile ambacho tumekizungumzia cha barabara ya Singida - Kilongero - Ntinko na Ntinko Hospitali - Iyambi Hospitali - Hospitali ya Rufaa ya Haidu. Barabara hii inahudumia zaidi ya watu laki tano, wengi wao wakiwa wagonjwa wanaotegemea hizo hospitali tatu zilizo katika huu mtandao nilioutaja;

Je, Serikali itatimiza lini ahadi yake iliyoniahidi hapa Bungeni kwamba barabara hii inayounganisha hizi hospitali tatu itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ahadi zinazotolewa na Serikali ziko pale pale na zinawekwa kwenye mipango ya Maendeleo ya kila mwaka. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, awe na subira, ahadi zinazotolewa Bungeni hatudanganyi, ni ahadi za ukweli na zitatolewa ufafanuzi na utekelezaji wake utakwenda kwa awamu, kulingana na upatikanaji wa fedha za Serikali. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amezungumzia mafungu ya fedha ya *Capitation Development Grant,* ambazo zinakwenda katika Wilaya zetu. Lakini utakuta fedha hizo mpaka hivi sasa Mkinga na Pangani zimechelewa, awamu ya pili bado hatujapata.

Je, ni sababu zipi zinazofanya pesa hizi zichelewe kufika katika maeneo yetu kwa sababu ni msingi mkubwa kwa maendeleo yetu? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, fedha za Serikali zinatokana na makusanyo na mapato ya Serikali. Pia zinatokana na Wahisani na zitatolewa kutokana na upatikanaji. Fedha hizi zikichelewa kupatikana, ina maana kwamba hata kutolewa zitachelewa. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, tuwe na subira, fedha hizo zitatolewa kulingana na upatikanaji wake.

Na. 16

**Kuongezeka kwa Hewa chafu Nchini**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa ni ukweli usiofichika kwamba kuna shughuli nyingi za binadamu hapa Tanzania ambazo husababisha ongezeko la hewa chafu *(Carbon Dioxide)* na kwa kuwa kuna mpango wa Umoja wa Mataifa unaoitwa *Carbon Credit,* unaowanufaisha watu ambao shughuli zao za uchumi zinapunguza ongezeko la hewa chafu:-

(a) Je, Serikali inaweza kutoa maelezo ya kutosha kuhusu mpango wa *Carbon Credit?*

(b) Je, Serikali inaweza kutueleza ni Watanzania au kampuni gani hapa Tanzania zilizonufaika na mpango huo?

(c) Kwa kuwa Watanzania walio wengi hushughulika na kazi za kilimo; je, ni aina gani ya kilimo kinaweza kunufaika na *Carbon Credit?*

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa joto duniani ni matokeo ya mlundikano wa gesi joto hasa hewa mkaa *(Carbon Dioxide).* Ongezeko hili limeleta madhara kijamii, kiuchumi na mazingira. Hapa Tanzania madhara hayo yanajidhihirisha katika kupungua

kwa kiwango cha theluji katika kilele cha Mlima Kilimanjaro, kuongezeka kwa matukio ya ukame na mafuriko ya mara kwa mara na kuenea kwa magonjwa kama vile malaria, katika maeneo ambayo ugonjwa huu haukuwa wa kawaida na mmomonyoko wa ufukwe na ukanda wa bahari.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na mabadiliko haya, Jumuiya ya Kimataifa ilipitisha Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi *(The United Nations Framework Convention of Climate Change)* wa mwaka 1992. Tanzania iliuridhia mwaka 1996. Nchi wanachama wa Mkataba zilipitisha Itifaki ya Kyoto ya mwaka 1997. Itifaki hii inazibana nchi zilizoendelea, kupunguza uzalishaji wa gesi joto ifikapo mwaka 2012 kwa asilimia si chini ya 5.2 ya viwango vya uzalishaji wake mwaka 1990. Itifaki hii ilianza kutekelezwa mwaka 2005 na Tanzania iliridhia mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, Itifaki ya Kyoto inasisitiza wajibu wa kwanza kwa nchi zilizoendelea ni kupunguza gesi joto katika nchi zao. Hata hivyo, Itifaki imeruhusu mifumo ya upunguzaji wa gesi hizi kwa ushirikiano baina ya nchi. Mfumo huu unaohusisha nchi zinazoendelea unajulikana kama *Clean Development Mechanism (CDM).* Katika mfumo huu nchi iliyoendelea huwekeza katika miradi au mradi unaosaidia katika maendeleo ya nchi inayoendelea na kupunguza gesi joto. Kwa kufanya hivyo, nchi iliyoendelea hupata *Carbon Credits* zinazoisaidia nchi hiyo kutimiza wajibu wake chini ya Itifaki. *Carbon Credit* moja ni *unit* inayotolewa kwa kila tani moja ya hewa inayozuiwa kuingia hewani. Aidha, ipo mifumo mingine ya hiari, inayohusu ushirikiano kati ya nchi zilizoendelea *(Joint Implementation)* na biashara ya gesi baina ya nchi hizo *(Emissions Trading).*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya utangulizi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama wanachama wa Mkataba na Itifaki, Serikali inautambua Mpango wa Umoja wa Mataifa kuhusu *Carbon Credit,* ulio chini ya Itifaki ya Kyoto. Mpango huo ambao unazihusisha nchi wanachama wa Itifaki ya Kyoto na unaruhusu nchi zilizoendela kutekeleza miradi ya ushirikiano katika nchi zinazoendelea. Upo utaratibu wa kimataifa unaosimamia miradi ya aina hii, ambao husimamiwa na Bodi ya Kimataifa ya *CDM.* Kila nchi mwanachama hutakiwa kuweka taratibu za kushiriki katika mpango huo. Ofisi ya Makamu wa Rais tayari imeandaa utaratibu wa kushiriki katika miradi ya *CDM.* Kipaumbele ni miradi ya nishati, viwanda, kilimo, upandaji miti, utunzaji misitu na udhibiti wa taka. Kutakuwa na Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Mpango na Miradi ya *CDM,* itakayoshirikisha sekta binafsi.

(b) Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya taasisi zinazotegemea kuanza kunufaika na mfumo huu. Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kupitia mradi wake wa kuzalisha umeme kutokana na taka za Dampo la Mtoni, inatarajia kuanza kufaidika na mpango wa *Carbon Credit* kuanzia Juni, 2007 kwa kipindi cha miaka kumi ijayo. Mradi huu unatekelezwa kwa kushirikiana na Kampuni ya *Global* kutoka Italia. Makampuni mengine ambayo yameonesha nia ya kushiriki ni pamoja na *EUROMET (T) Ltd* ya Dar es Salaam; *Green Resources Ltd* ya Mufindi, *Mwanguya Kyoto Works Ltd* ya Dar es Salaam; *Umeme Jua Ltd* ya Dar es Salaam; *Tanga Cement; Katani Ltd* ya Tanga na

*Abeche Palms Planting Enterprise*. Makampuni ya Kimataifa ni *Mitsubishi Corporation Ltd* ya Japan; *Seekab Ltd* ya Sweden na *The 20th Metallurgical Construction Corporation* ya China.

(c) Mheshimiwa Spika, aina ya kilimo ambacho kinaweza kunufaika na mpango wa *Carbon Credit* ni kile kinacholenga kuzalisha nishati itokanayo na mimea kama miwa, alizeti, mbarika, mawese, jatrofa na mironje na shughuli yoyote yenye lengo la kupunguza utoaji wa gesi joto, kwa mfano, udhibiuti wa taka zitokanazo na mlundikano wa mabaki ya baadhi ya mazao, kilimo mseto na mashamba ya miti.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa William H. Shellukindo, ameuliza swali la msingi sana. Mabadiliko ya tabianchi kutokana na ongezeko la joto ni ajenda kubwa duniani. Wanasayansi wanaamini ongezeko hili lisipodhibitiwa, litabadilisha jiografia ya ulimwengu na kuathiri kuwepo kwa uhai wa binadamu na viumbe duniani. Tanzania na nchi zinazoendelea, hutoa kiasi kidogo cha gesi hiyo lakini hubeba mzigo mkubwa wa madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi. Juhudi zetu pia zitalenga zaidi katika kujiandaa kujikinga na madhara hayo au kupunguza makali yake *(adaptation).*

Mheshimiwa Spika, Tanzania imehusika sana na mjadala wa suala hili. Nilipata heshima kubwa ya kuwa Msemaji Mkuu wa kundi la nchi 133 katika majadiliano ya mwaka 1997 yaliyopelekea kupitishwa kwa Itifaki ya Kyoto ya Mkataba wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Profesa Mark J. Mwandosya, kwa maelezo mazuri haya ambayo kwa kweli ni mara ya kwanza kuyapata. Nina swali moja la nyongeza. *(Makofi)*

Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Bumbuli na Wilaya ya Lushoto kwa ujumla, wamejitahidi sana kupanda miti na hata ikasababisha mwaka 2006 mvua zilinyesha kuanzia Febriari mpaka Desemba. Sasa katika hali hiyo, je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba wakati ukifika ile Kamati ikifanya kazi basi Wilaya ya Lushoto na hasa Jimbo la Bumbuli, iwe katika orodha ya miradi ya kuweza kufaidika na *Carbon Credit?*

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuwa nimemwona Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mbunge wa Kiteto, ambaye hatukuwa naye tangu tarehe 5 Julai, 2006, alikuwa anaugua na akapelekwa India. Ni jambo la furaha na la kumshukuru Mwenyezi Mungu na ni dhahiri afya yake ni njema. Kwa sababu hiyo sasa nampa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa maneno yako ya utangulizi na napenda kuliarifu Bunge ya kwamba, nimerudi na nimepona. *(Makofi)*

Baadaye nitatoa shukrani kama nitapata nafasi ila napenda niitumie nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kujibu kwa ufasaha sana swali hili ambalo ni geni kweli kweli katika nchi yetu. *(Makofi)*

Katika nchi yetu kuna misitu ya asili ambayo ikifanyiwa uchunguzi vizuri, tunaweza tukafaidika kwa kupata fidia katika Mashirika ya Kimataifa. Misitu ya asili ndiyo inayoleta hasa hii *Carbon Dioxide Credit.* Ukiangalia Kiteto kuna msitu mmoja wa asili, ambao una sifa kubwa katika Bara la Afrika, ambao unaitwa Suledo, umepata *Ikweta Initiative Award* na kuna misitu mingine mingi tu katika nchi yetu. Je, ni lini Serikali itafanya mpango ili misitu hii ambayo ninaizungumzia, iweze kuingizwa katika Mfumo wa Umoja wa Mataifa ili iweze kufidia na kuweza kuoteshwa kwa urahisi katika nchi yetu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, naomba niungane na wewe na Waheshimiwa Wabunge wengine, katika kumpa pole. Bila shaka tumefurahi kwamba, afya yako imerudi kama kawaida na tumefurahi kukuona hapa Bungeni.

Kuhusu Msitu wa Suledo na Hifadhi za Tanzania kuingia katika Mpango huu wa *Carbon Credit,* hili ni suala la msingi sana, linajadiliwa sasa katika majadiliano yanayoendelea katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa unaohusu tabianchi. Nchi zinazoendelea zimejenga hoja kwamba, sehemu kubwa za nchi zao au ulimwengu uweze kufaidika kwa kuvuta ile hewa ambayo inachafua ulimwengu. Kwa hiyo, inasaidia kupunguza makali ya ongezeko la joto. Kwa maana hiyo, inabidi tufidiwe ili tuweze na sisi kuendelea kuitunza hiyo misitu. Huu mjadala utakapokamilika, naamini tutatoa ripoti na watu wa Kiteto watatusikia. Nakushukuru. *(Makofi)*

Na. 17

**Kero za Muungano**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi hukutana mara tatu ka mwaka kushughulikia kero za Muungano; na kwa kuwa kero hizo ni nyingi:-

(a) Je, ni kero ngapi zilizokwisha shughulikiwa kikamilifu tangu viongozi hao waanze utaratibu huo?

(b) Je, ni kero ngapi zilizo katika mchakato wa kushughulikiwa?

(c) Je, ni kero zipi ambazo hazijaanza kushughulikiwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, naomba nitoe maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama ilivyoainishwa kwenye nyongeza ya kwanza ya Katiba hiyo, masuala ya Muungano yako 22. Vikao vya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, hukutana angalau mara tatu kwa mwaka, kwa madhumuni ya kujadili jinsi ya kutatua vikwazo vinavyokabili utekelezaji wa masuala ya Muungano kwa awamu. Mpaka sasa vikao hivi vimefanyika mara mbili, tarehe 22 Mei, 2006 Mjini Dar es Salaam na tarehe 21 Novemba, 2006 Mjini Zanzibar.

Baada ya utangulizi huu, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, masuala yaliyoshughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi kikamilifu ni haya yafuatayo:-

- Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu, ambayo ilipata kikwazo kutumika Tanzania Zanzibar kutokana na Ripoti za Tume hiyo kushindwa kufikishwa kwenye Baraza la Wawakilishi, kutokana na kutokuwepo kwa kipengele kinachomtambua Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Utawala Bora wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika Sheria hiyo na hivyo kupelekea Waziri huyo, kushindwa kufikisha ripoti hizo katika Baraza la Wawakilishi. Sheria hii sasa imerekebishwa na inaweza kutumika pande zote mbili za Muungano.

- Uvuvi katika Bahari Kuu ilikuwa ni kero ambapo pande zote mbili za Muungano zilikuwa zikitoa leseni za uvuvi katika bahari moja. Marekebisho yamefanywa katika Sheria ya Kusimamia Uvuvi kwenye Bahari Kuu, kwa kuundwa Mamlaka ya Uvuvi ya Muungano. Sheria hii sasa itatumika katika pande zote mbili za Muungano.

- Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili wanapoleta bidhaa zao Tanzania Bara baada ya kuwa wameshalipia kodi Zanzibar, yameshughulikiwa kwa kufungwa mtandao wa kompyuta unaoitwa *ASYCUDA++* tokea Juni, 2006. Mtandao huu utahakikisha kwamba, kodi inayotakiwa inalipwa kikamilifu Zanzibar na hivyo kuepusha wafanyabiashara hao kutozwa tena wanapopeleka bidhaa zao Tanzania Bara.

(b) Masuala ambayo yanaendelea kushughulikiwa ni yafuatavyo:-

- Masuala ya ugawanaji wa mapato yatokanayo na misaada kutoka nchi za nje, faida ya Benki Kuu na Mikopo, yameshughulikiwa na Tume ya pamoja ya Fedha,

ambayo tayari imeshatoa taarifa yake kwa Serikali zetu mbili. Serikali zetu mbili zitapitia ushauri uliotolewa na kisha kupata muafaka.

- Utekelezaji wa Sheria ya *Merchant Shipping Act* - Wizara ya Miundombinu (SMT) na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ) zimeunda Kamati ya kushughulikia faida zinazopatikana kwa kuwa mwanachama wa *International Maritime Organisation (IMO)*, ili kuweka bayana jinsi ya kugawana faida za kiuchumi kwa pande zote mbili za Muungano.

- Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki - Wizara husika za pande mbili ziliagizwa kuunda Kamati ambayo pamoja na mambo mengine, itabainisha miradi ya maendeleo ambayo nchi itanufaika kutokana na kuwa mwanachama wa Jumuia hii ili pande zote za Muungano zinufaike. Miradi hiyo ni pamoja na uendelezaji wa bandari, viwanja vya ndege na *East African Power Master Plan.*

- Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia - suala hili linaendelea kufanyiwa kazi, ambapo iliamuliwa atafutwe mtaalam mwelekezi atakayezishauri Serikali zetu mbili, juu ya utaratibu bora wa kugawana rasilimali hizi kwa manufaa ya pande zote mbili.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwamba, masuala ya Muungano yako 22, ni dhahiri kwamba, baada ya vikao hivi viwili, bado yapo maeneo kadhaa ambayo bado hayajashughulikiwa. Maeneo haya yataendelea kushughulikiwa katika vikao vinavyofuata.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ya ufasaha sana. Pamoja na utatuzi wa matatizo hayo yanayoendelea hivi sasa, sijui anayo habari kuwa moja katika kero inayowaudhi sana watu hivi sasa ni suala la magari. Magari yenye namba za Tanzania Bara au za Jamhuri ya Muungano yanatumika Zanzibar, lakini yale magari yenye namba za ZNZ yakija huku upande wa pili wa Muungano ni vurugu kubwa, watu wanatozwa fedha kiajabu ajabu na hawaendeshi magari yao. Hivi tatizo hili watalitatua lini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, suala la namba za magari ni utaratibu wa usajili. Huko nyuma kulikuwa kuna matatizo mawili; kwanza kulikuwa na magari yaliyopitishwa Zanzibar yalikuwa yanalipiwa ushuru pungufu na hivyo yanapoletwa Tanzania Bara, wanatozwa ile tofauti ya ushuru unaotakiwa. Lakini toka mtandao wa kompyuta nilioutaja wa *ASYCUDA++* kufungwa, suala hili limekwisha. Tatizo lililobaki sasa ni utaratibu wa usajili.

Lazima tukiri kwamba, utaratibu wa usajili wa Tanzania Bara, unataka magari yote yabadilishwe namba kuwa na namba ambazo zinalingana. Kusema kweli hili liko bayana na gharama zake zinajulikana. Si kweli kwamba kuna utaratibu wa kiajabu ajabu. Hili mimi binafsi nimewahi kulishughulikia na inaonekana wazi kabisa kwamba, mtu atakapokuwa amelipa ushuru kikamilifu, baada ya mtandao wa kompyuta huu, basi

anachofanya akifika Tanzania Bara ni kubadilisha tu namba na gharama yake ni shilingi laki moja na elfu arobaini na tano kupata namba zinazotakiwa. *(Makofi)*

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kero kubwa ya Muungano inahusiana na mgawanyo wa mapato ya Muungano; na kwa kuwa Tume ya Pamoja ya Fedha imeshawasilisha katika Serikali zote mbili, ripoti ambayo walitakiwa kuIfanyia kazi na ni muda mrefu toka ripoti hiyo iwasilishwe (Agosti, 2006); sasa ni kwa nini Serikali inachukua muda mrefu kueleza hatma ya ripoti hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba, Tume ya Pamoja ya Fedha imewasilisha ripoti yake Serikalini. Lakini nataka Waheshimiwa Wabunge watambue kwamba, utaratibu wa kushughulikia suala si rahisi kama inavyofikiriwa. Serikali zote mbili, lazima ziipitie kutoka ngazi za Watendaji ifike katika Kamati ya Makatibu Wakuu, ifike katika Baraza la Mawaziri ndipo uamuzi utolewe na baada ya hatua hizo, ndipo sasa pande mbili zikutane kwa madhumuni ya kukubaliana yale ambayo pande zote imeridhika nayo. Kwa hiyo, mchakato huu unaendelea na katika siku za hivi karibuni, tutatoa taarifa rasmi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona ni haki kwa kuwa nyongeza zote zimetoka Kambi ya Upinzani, nitoe nafasi ya mwisho kwa Mbunge kutoka CCM.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza na pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa jibu lake kuhusiana na suala la kwanza la nyongeza linalohusiana na ZNZ. Inavyoonekana, Mawaziri wetu wa Serikali ama hawapeani taarifa au baadhi ya Mawaziri hawasomi *Hansard*, suala la ZNZ liliulizwa katika Mkutano wa Tano kuhusu magari ya ZNZ na Waziri wa Fedha alijibu na *Hansard* ipo kwamba, si ruhusa kuzuia magari ya ZNZ kutokutembea Tanzania Bara. Baada ya jawabu hilo wananchi wote wakafarijika.

Lakini leo Mheshimiwa mwingine wa Serikali anasema kuna utaratibu wa kusajili, Serikali inatupeleka wapi? Tumkubali Waziri wa Fedha, tumkubali Waziri wa Muungano? Nashukuru Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Loo! Nilidhani swali kutoka Mbunge wa CCM litakuwa nafuu kwa Serikali, kumbe! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, ikaangaliwe *Hansard,* Waziri wa Fedha hajasema kwamba, hakuna matatizo ya magari yenye namba za ZNZ.

Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid alileta swali hili, nilimwambia kwamba na yeye alikuwa ni mmojawapo wa kutatua matatizo haya. Nilimwambia kwa uwazi kabisa kwamba, anatozwa fedha zaidi ya zile alizolipa kwa sababu hakulipa fedha zinazohitajika kule, lakini namba za magari ikiwa ni ZNZ au ikiwa yanatoka sehemu nyingine yoyote, usajili lazima ufanyiwe kwa namba za hivi sasa. Nikasema zaidi kwamba, hata Zanzibar

sasa hivi ukitaka kuandikisha gari kwa namba za Bara hizi za TZ 141 au APZ pia unaweza kufanya pale pale Zanzibar bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa ufafanuzi huo. Tunaendelea sasa tunahamia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mbunge wa Karagwe CCM.

Na. 18

**Bei ya vifaa vya Ujenzi**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa bei ya sementi, bati na vifaa vingine vya ujenzi hutofautiana kati ya mkoa na mkoa kutokana na gharama za usafirishaji na kwa kuwa Wilaya ya Karagwe ipo pembezoni mwa Tanzania, mbali na viwanda vinavyozalisha vifaa hivyo, hali inayosababisha bei ya vifaa hivyo kuwa juu sana ikilinganishwa na Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro na Morogoro na hivyo kusababisha wananchi wa Karagwe kushindwa kununua vifaa hivyo: Je, kwa nini Serikali isiweke bei inayolingana na nchi nzima kwa sementi, bati na vifaa vingine vya ujenzi kama ilivyo kwa bei za bia na soda?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba bei ya saruji, bati na vifaa vingine vya ujenzi, hutofautiana kati ya mkoa na mkoa kutokana na gharama za usafirishaji.

Kwa hali hiyo, kadri ya ugumu wa miundombinu ya usafiri na umbali wa eneo unavyozidi kuwa mrefu kutoka kwenye viwanda vya uzalishaji wa bidhaa husika, ndivyo bei inavyozidi kuongezeka. Hali hiyo ndiyo inayoyakabili maeneo mengi hapa nchini ikiwemo Wilaya ya Karagwe.

Mheshimiwa Spika, kufuatia nchi yetu kubadili mfumo wake wa uchumi kutoka mfumo wa uchumi hodhi kwenda mfumo wa biashara huria, bei za bidhaa mbalimbali kwa sasa zinategemea nguvu ya soko. Serikali kwa sasa haipangi bei za bidhaa ikiwa ni pamoja na zile za soda na bia, ambapo makampuni husika yanapanga yenyewe na kufikisha bidhaa hizo karibu na walaji. Kabla ya Serikali kuchukua hatua ya kulegeza mashati ya biashara, bei za bidhaa sehemu mbalimbali zilikuwa zikipangwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kujitoa katika shughuli za biashara, jukumu lake sasa ni la kuandaa sera za kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji na kuimarisha biashara. Ni mategemeo yangu kwamba, juhudi za Serikali zinazoendelea hivi sasa za kuboresha miundombinu ya reli na barabara, zitaleta unafuu wa bei za bidhaa

mbalimbali katika maeneo ya mbali na vilipo viwanda ikiwemo Wilaya ya Karagwe. Serikali pia itaendelea kuhamasisha wawekezaji wa viwanda, kuwekeza kwenye maeneo ya mbali ili bei za bidhaa zitakazozalishwa na viwanda hivyo ziweze kuwa za nafuu.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, vilevile namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba gharama za vifaa vya ujenzi katika Wilaya ya Karagwe zinapanda kutokana na gharama za usafirishaji na mfano mzuri ni kwamba mfuko mmoja wa sementi katika Wilaya ya Karagwe unauzwa kati ya shilingi 22,000 mpaka 25,000, wakati kwa Dar es Salaam na Tanga ni kati ya shilingi 11,000 na 12,000. Kwa kuwa, Serikali inapotoa mgao wa fedha kuhusiana na ujenzi wa sekondari pamoja na vyumba vya shule za msingi, inatoa gharma sawa; je, Serikali inasema nini kuhusiana na hizi gharama zinazoongezeka katika Wilaya ya Karagwe; iko tayari kuongeza fungu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika majibu ya msingi hapa kwamba, bei za bidhaa zinapanda kadri ya umbali kutoka kwenye viwanda na hali hiyo haihusu Wilaya ya Karagwe tu peke yake. Lakini nataka tu niseme kwamba ni miradi mingi ya ujenzi wa majengo mbalimbali inatumia sementi, ikiwa ni pamoja na shule za sekondari. Kwa hiyo, kusema kwamba pengine uwekwe mgao wa ziada kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari na msingi tu wakati kuna miradi mingine ambayo inahusika na saruji, nadhani kwa sasa hivi itakuwa ni vigumu kufanya hivyo ukizingatia kwamba, saruji inatumika katika maeneo mengine ya mbali na vilevile katika miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kushauri hapa, pengine mwombe Mheshimiwa Mbunge, aendelee kushirikiana na vyombo mbalimbali katika upangaji wa miradi hii hasa masuala ya gharama kwa hivi sasa hasa tukizingatia hali ilivyo, wakati tukijiandaa na hayo niliyokuwa nimeshauri katika jibu la msingi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nataka niongezee kidogo tu kuhusu bei za vifaa vya ujenzi hasa kwa upande wa shule za msingi na upande wa shule za sekondari. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kweli imeliona hilo, kuna sehemu nyingine zina matatizo hasa ya usafiri, kwa hiyo, litaangaliwa wakati wa mgao wa fedha katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Na. 19

**Kubinafsishwa kwa Shirika la Bima la Taifa**

**MHE. CHANDE H. KIGWALILO** aliuliza:-

(a) Je, zoezi hili limefikia hatuna gani na ni kwa kiasi gani wafanyakazi wa shirika hilo wameshirikishwa kwenye zoezi hilo?

(b) Je, shirika hilo lina madeni kiasi gani na lina wateja wangapi?

(c) Je, shirika hilo lina rasilimali *(assets)* za thamani gani na ziko wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusu yako, kwanza kwa niaba ya Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma, naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa mapokezi makubwa waliyomfanyia Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chande H. Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Zoezi la ubinafsishaji wa Shirika la Bima limefikia hatua ya utathmini wa zabuni za wawekezaji walioonesha nia ya kununua biashara za bima zinazouzwa. Aidha, Serikali pia inafanya tathmini ya mali zinazoendana na biashara husika ili kuona kwamba, bei itakayopatikana inaendana na thamani ya sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuridhia Mkakati wa Kubinafsisha Shirika la Bima la Taifa, mnamo mwaka 2004, wafanyakazi wameshirikishwa kikamilifu katika zoezi hilo. Hatua zilizochukuliwa katika kuwashirikisha wafanyakazi ni pamoja na:-

- Kuwapa wafanyakazi hojaji (*questionnaire*) kwa ajili ya kupata maoni ya namna ambavyo wao wangependa kushiriki katika zoezi hili. Kati ya wafanyakazi 587, wafanyakazi 539 walijibu na kurudisha hojaji hizo na wengi walipendelea kuuziwa sehemu ya hisa kama wafanyakazi.

- Wafanyakazi wamekuwa wakishirikishwa mara kadhaa kupitia vikao mbalimbali ambapo ubinafsishaji wa shirika umekuwa moja ya ajenda ya vikao hivyo. Moja ya vikao hivyo ni Baraza la Wafanyakazi.

- Shirika liliandaa semina mbalimbali ili kuelimisha wafanyakazi juu ya dhana nzima ya ubinafsishaji, ushiriki wa wafanyakazi na mstakabali wa shirika na ajira, baada ya zoezi zima la ubinafsishaji kukamilika. Watalaam kutoka *PSRC* na *TUICO* Makao Makuu, wamekuwa wakialikwa kutoa mada husika.

- Shirika lina wawakilishi katika Kamati ya Watalaamu inayoishauri *PSRC* kuhusu masuala mbalimbali ya ubinafsishaji wa *NIC.* Kati ya wawakilishi hao, mmoja wao ni mjumbe wa Chama cha Wafanyakazi *(TUICO),* Tawi la *NIC.* Serikali itaendelea kuwashirikisha wafanyakazi kikamilifu, kwenye mchakato mzima wa kubinafsisha *NIC* hadi mwisho wa zoezi hili.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2006, Shirika lilikuwa na madeni yaliyohakikiwa yanayofikia shilingi bilioni 37.3; madeni yaliyopo mahakamani ya kuribu shilingi bilioni 20 na thamani ya bima za wateja *(Policyholders*

*Funds)* zilikuwa shilingi bilioni 30.8. Aidha, shirika lilikuwa na wateja wa bima za maisha wanaofikia 90,000, wengi wao ni walimu na askari.

(c) Mheshimiwa Spika, kufikia tarehe 31 Desemba, 2006, Shirika la Bima la Taifa lilikuwa na rasilimali zenye thamani ya shilingi bilioni 59.3, ambazo zinajumuisha majengo yenye thamani ya shilingi bilioni 35.4 yaliyoenea nchi nzima, hisa katika mashirika mbalimbali shilingi bilioni 14.3 na mali nyingine na madai mbalimbali yanayofikia shilingi bilioni 9.6.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, asante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, miaka miwili au mitatu iliyopita, Shirika la *NIC* lilikuwa namba mbili kiutendaji baada ya *HERITAGE,* lakini hivi sasa limezidi kushuka; je ni sababu zipi zimesababisha liendelee kushuka hadi hivi leo?

Pili, kuna wananchi wengi ambao ni wa kawaida kabisa, baada ya kupevuka kwa insurance zao wanaanza kulipwa kwa *instalment*, kitu ambacho kinaleta usumbufu sana na kero kubwa sana kwa wananchi hao. Sasa ni lini haya majengo ambayo ni *assets* yatauzwa mara moja ili waweze kufidia madeni yote, wananchi wasiendelee kupata tabu kwa pesa ambazo waliziweka katika *insurance*?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, ziko sababu nyingi ambazo zimesababisha shirika hili kuteremka kiutendaji na ndizo hizo ambazo zinafanya sasa Serikali kufikiria toka mwaka 2004, kulibinafsisha kama ambavyo mashirika mengi ya umma yamebinafsishwa, moja wapo ikiwa ni utendaji wa ndani wa shirika hilo.

La pili, majengo hayo yataanza kuuzwa mara baada ya kumaliza tathmini ya mali za Shirika la Bima na kumaliza mchakato mzima wa kumtafuta mtu atakayeweza kununua shirika hilo. Napenda ieleweke wazi kwamba, hatuuzi majengo, bali tunauza biashara ya bima inayohusisha bima ya maisha na bima ambayo si ya maisha.

Na. 20

**Maji yaliyozidi kwenye Bwawa la Mtera**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa, maji ya Bwawa la Mtera ndio chanzo kikuu cha umeme unaotegemewa kwa mji nchini pamoja na Bwawa la Kidatu; na kwa kuwa, bwawa hilo lina uwezo wa kuchukua mita za ujazo 3,700 milioni, sawa na 698.5 milioni kutoka usawa wa bahari; na kwa kuwa mwaka huu kina cha ujazo kimefikiwa mapema kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha kwenye maeneo mengi ya nchi hivyo, kuilazimu *TANESCO* kuyafungulia maji hayo ambayo yanaweza kusababisha mafuriko ambayo ni hatari kwenye Bonde la Mto Kilombero na maeneo mengine, mashamba ya miwa, pamoja na kuharibu makazi ya watu wa sehemu hizo:-

Je, Serikali ina mipango gani endelevu ya muda mfupi na mrefu ya kuhakikisha kuwa maji hayo hayapotei bure kama inavyotokea hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati wa Madini, naomba niungane na wenzangu, kumpongeza Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kwa kuchaguliwa kuwa mwakilishi wa Jimbo la Tunduru kupitia Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia Februari hadi Desemba, 2006 kulikuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa umeme nchini. Hali hii ilisababishwa na ukame ulioikumba nchi yetu kwa takriban miaka mitatu mfululizo na kusababisha upungufu wa maji kwenye mabwawa yenye mitambo inayozalisha umeme kwa kutumia maji, iliyoko katika mabonde ya Mto Rufiji na Mto Pangani. Hata hivyo, mwishoni mwa mwaka 2006 mvua zilianza kunyesha kwa wingi, mabwawa yaliyokuwa yameanza kukauka yakajaa maji na mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia maji ikaanza uzalishaji. Hali hii ilisababisha mgao wa umeme tuliokuwa nao nchini kukoma. Mpaka sasa mvua zinaendelea kunyesha na mabwawa ya maji nchini, yakiwemo mabwawa ya Mtera na Kidatu, yanazidi kupata maji mengi.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Mtera linatumika kuhifadhi maji kwa ajili ya uzalishaji wa umeme wa *MW 80* katika mitambo ya Mtera na baada ya hapo maji hayo hutiririka hadi kwenye Bwawa la Kidatu, ambapo hutumika kuendesha mitambo ya kuzalisha *MW 200*. Mbali na mitambo ya Kidatu, hakuna mtambo mwingine unaozalisha umeme kwa kutumia maji, hivyo maji hutiririka kuelekea kwenye Mabonde ya Kidatu na Rufiji ambapo kuna mashamba, hatimaye maji hayo huingia baharini.

Mheshimiwa Spika, licha ya nia ya Serikali kuwa na mabwawa zaidi ya moja katika mabonde yanapopita maji yanayotoka katika mabwaya ya Mtera na Kidatu ili yatunzwe maji kwa ajili ya matumizi wakati wa ukame, lakini bado Serikali imeshindwa kutimiza azma hiyo kutokana na gharama kubwa za ujenzi wa mabwawa hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mpango Endelevu wa muda mrefu wa kuhakikisha kuwa maji yatokayo katika Bwawa la Kidatu yanatumika kwa matumizi mengine ya kimaendeleo ni uendelezaji wa Mradi wa *Stigler's Gorge* kwenye Mto Rufiji, ambao unakusanya maji kutoka kwenye mito iliyoko katika Bonde la Rufiji. Tukifanikiwa kukamilisha mradi huu tutaweza kuzalisha umeme wa zaidi wa *MW 1000*.

**SPIKA**: Wakati huo huo timu ya wahadisi waangalie Waheshimiwa Wabunge wanawake wanalalamika kuna baridi sana leo hapa. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Nimemsikiliza vizuri Naibu Waziri, lakini mimi mtazamo wangu ni tofauti kidogo na majibu yake. Kutokana na uchunguzi nilioufanya, hivi sasa Serikali inatumia takribani dola za Kimarekani milioni 411 kwa miradi ya umeme ya dharura na inayotumia mafuta na baadhi ni miradi ya kukodi.

Tuna miradi mitano ambayo inatumia pesa nyingi sana na miradi hiyo ni ya dharura na mitatu ni ya kukodi. Mfano kuna Mradi wa *AGRECO*, unaigharimu Serikali *USD* milioni 61 na ni mradi wa kukodi. Kuna Mradi wa *DOWANS*, ambaye ni dada yake *Richmond*, unaigharimu Serikali *USD* 102,600,168 na ni mradi wa kukodi. Kuna mradi wa *WATSILA* ya Finland ambao unaigharimu nchi *EURO* milioni 57, *approximately* ni sawa na milioni 76, kuna mradi mwingine wa Finland vilevile unaigharimu Serikali yetu *EURO* milioni 41, takriban USD milioni 57 na kuna mradi wa tano ambao unaitwa *AL-ASTOM* uko Mwanza, mradi huu unaigharimu nchi *USD* milioni 116 na ni wa kukodi.

Serikali haioni kwamba ingekuwa busara tena busara kubwa sana kutumia pesa hizi za hii miradi ya kukodi ambayo haitatui matatizo ya kudumu ya umeme, ikazielekeza pesa hizi kwenye kujenga mabwawa pamoja na *power stations* kwenye Mto wa Ruhuji, mradi ambao wenyewe walishaufanyia utafiti wakaona kwamba utatoa *MW 318* na mradi mwingine kwenye Mto Rumakali, ambao Serikali yenyewe ilishafanya utafiti ikaona kwamba wanaweza wakatoa *MW 322* kuliko kutumia mabilioni yote haya kwenye miradi ya kukodi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, asante sana. Naomba kumshukuru Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, kwa swali lake la nyongeza na vilevile kumpongeza Naibu Waziri, kwa majibu yake aliyoyatoa kwa swali lake la msingi.

Mheshimiwa Spika, naweza kusema kwamba, namshukuru Mungu aliyetujalia sisi binadamu kuwa wepesi wa kusahau, hicho ndicho Mungu alichotujalia. Katika kipindi cha September hadi Novemba, 2006 nchi yetu ilikuwa taabani na Gridi ya Taifa ilikuwa karibu ianguke. Wakati ule ndipo Serikali iliitaarifu Bunge hili, mikakati gani inaifanya ili kuinusuru Gridi ya Taifa isianguke na ndio tuliingia hii mikakati ya umeme wa dharura. *(Makofi)*

Hii mikakati ya umeme wa dhararu ilikuwa kama *insurance* na hakuna yeyote ambaye alikuwa anajua kwamba mwishoni mwa Januari mvua zitanyesha kama zilivyonyesha. Nina hakika tusingefanya hivyo, Gridi ya Taifa ingeanguka, swali lingekuja Serikali imechukua mkakati gani kulinusuru taifa lisikose umeme. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ule mkakati wa Serikali uliopangwa wakati ule ulikuwa ni sahihi. Ilikuwa ni *insurance* ambayo lazima Serikali ifanye makusudi kuhakikisha kwamba Taifa letu linaendelea kuwepo. Ni kama sisi Waheshimiwa Wabunge tuna magari yetu, huwa nalisema kila wakati ninapopata nafasi, unaweza ukamaliza miaka mitano bila kupata ajali, lakini lazima ulipie *insurance* ya gari. Kwa hiyo na sisi hii ndiyo ilikuwa *insurance* ya kunusuru nchi na ndiyo gharama

tuliyokuwa nayo. Lakini hizo gharama vilevile anazozizungumza na nilikuwa nazungumza kwenye Kamati yetu ya Uwekezaji na Biashara kwamba, gharama ambazo zimewekwa pale zina vitu viwili, zina *component* mbili, *component* ya kwanza ni *energy charge* na *component* ya pili ni *capacity charge*.

Yule anayekodisha analipwa *capacity charge* ile ya mitambo yake kuileta ikakaa, lakini *energy charge* kama ananunua mafuta yatanunuliwa kwenye makampuni ya mafuta, kama ananunua gesi zitanunuliwa kwenye makampuni ya gesi, hiyo hela haiendi kwa yule mkodishaji.

Kwa hiyo, mitambo hii ya kufua umeme iwe ya kwetu au ya mkodishaji, *energy charge* hatuepukani nayo tukitumia hiyo mitambo. Tukikodi *Capacity charge* ndiyo gharama tunakuwa nayo kama *insurance* kwa mwekezaji.

Vile vile nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, mipango aliyoizungumza ya Luhiji, Rumakali na *Stiegler's Gorge*, tunayo katika *master plan* yetu ya kuiendeleza sekta ya umeme. Amezungumzia zile *MW 145*, ambazo 100 ni za pale Ubungo na 45 zitakwenda Tegeta, hizi zitamilikiwa na Serikali. Umilikaji wake umepangwa makusudi kuhakikisha kwamba wakati huo kipindi cha waliokodisha mitambo kinamalizika. Mikakati kwamba tusiingie katika balaa la namna hili, tena pawe na ukame ama usiwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Mbunge utuamini kwamba sasa hivi tumejifunza vya kutosha toka nyuma, mpango ni kutumia mchanganyiko wa uzalishaji ambao tunao hivi sasa wa maji, mkaa wa mawe, gesi na hata upepo. Vyote tunajaribu kuvichanganya kwa pamoja kwa uwiano unaotakiwa ili kuhakikisha kwamba nchi yetu haipati balaa kama ilivyokuwa mwaka jana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, majibu yanatosheleza. Waheshimiwa Wabunge, tuna nusu saa na bado tuna maswali tisa, sasa naomba tuendelee.

Na. 21

**Uendeshwaji wa Makampuni ya Wawekezaji**

**MHE. HALIMA J. MDEE** Aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na usiri mkubwa juu ya uendeshaji wa Makampuni ya Wawezeshaji, hasa yanayojishughulisha na masuala ya Madini:-

(a) Je, Serikali ilinunua hisa ngapi toka kwa *Williamson Diamond*, ikauza ngapi na kwa kiasi gani?
(b) Je, Serikali imepata gawio kiasi gani tangu kuanzishwa kwa mgodi husika?

(c) Kwa kuwa, taarifa za ndani zinaonesha kuwa wamiliki wa mgodi huu wamekuwa wakifanya msukumo wa kuhakikisha wanamiliki asilimia mia moja za hisa zote; je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa jibu la swali la Mheshimiwa Halima J. Mdee, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, suala la usiri kati ya pande zinazohusika katika mikataba ya uendeshaji wa kampuni za wawekezaji ni la kawaida duniani kote na hivyo huwepo kipengele cha usiri *(Confidentiality Clause)* katika mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Almasi wa Mwadui unaendeshwa na Kampuni ya *Williamson Diamond Limited (WDL)* na unamilikiwa kwa ubia na Kampuni ya *Willcroft,* ambayo ni kampuni tanzu ya *De-Beers* ya Afrika Kusini na Serikali ya Tanzania. Kabla ya mwaka 1994 kila mbia alikuwa na hisa za asilimia 50. Ilipofika mwaka 1994 kutokana na *WDL* kuwa katika hali mbaya kibiashara, Serikali iliuza asilimia 25 ya hisa zake kwa Kampuni ya *Willcroft.* Kampuni hiyo ilinunua hisa hizo kwa kulipa Dola za Marekani 180,542 kwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC).* Kiasi hicho ni sawa na shilingi za Tanzania 93,882,542 kwa wakati ule.

(b) Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Williamson Diamonds Limited* ilikuwa ikitoa gawio kwa wanahisa hadi mwaka 1980 wakati kampuni ilipokuwa ikipata faida. Tangu mwaka 1957 hadi 1980 Serikali imepata gawio la Paundi za Kiingereza Milioni 10, Dola za Marekani milioni 31 na shilingi milioni 195.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, wamiliki wa Mgodi huu ni *Willcroft* na Serikali ya Tanzania. Hakuna msukumo kuhusiana na suala la hisa, ila kuna chaguzi za ama Serikali kuendelea kubaki na asilimia 25 ya hisa ilizonazo, kuwa na hisa chini ya ilizonazo kwa sasa au kutokubakiwa na hisa ndani ya *Williamson Diamond Limited*. Serikali inaendelea kuzifanyia kazi chaguzi hizi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba, kampuni husika imekuwa ikipata hasara kwa kipindi cha miaka 27 kwa sababu maelezo yake yanaonesha gawio la mwisho kwa Serikali ni mwaka 1980.

Mimi nina swali dogo; kampuni inaendeshwa kwa hasara katika kipindi chote hicho na bado wamiliki wanaendelea kung’ang’ania kuendesha hiyo kampuni; je, Waziri haoni kwamba ile hasara ya shilingi 1.3 trilioni, ambayo inasemekana kwamba imetokana

na sekta ya madini, haitokani na udanganyifu ambao wenzetu wenye makampuni wanaitoa kwa Serikali?

La pili, mwaka 2006 wakati aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha akijibu swali la Mbunge wa Kahama, alisema kwamba, lile gawio ambalo Halmashauri ilikuwa inatakiwa ipewe la shilingi milioni 240, ambazo kimkataba zilikuwepo lakini wenye madini walikuwa wanazembea kulipa; je, kuanzia lini walikuwa hawajatoa na kama walitakiwa walipe na yale malimbikizo, nataka nipate *clarification* katika hayo mawili?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kampuni ya *Williamson Diamond Limited* imefanya biashara kwa kupata hasara kwa miaka takribani kama ile ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge, lakini si kweli kwamba hasara iliyotokana na hiyo pengine ipo ndani ya kile ambacho kimesemekana ni hasara iliyotokana na makampuni ya madini ya shilingi 1.3 trilioni. Hakuna udanganyifu wowote kutokana na uchunguzi ambao umefanywa na Serikali, pamoja na mshauri ambaye aliajiriwa na Serikali kuisaidia Serikali kubainisha yale ambayo yanaendelea katika kampuni ya madini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika hili hakuna mahusiano yoyote na hakuna udanganyifu wowote unaoendelea na Serikali iko makini kuonesha kwamba kinachofanyika Serikali inakuwa inapata maslahi yanayotatikana.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha pili cha swali lake nilikuwa naomba kujibu kama ifuatavyo:-

Kwa sasa hivi Serikali imekuwa ikijadiliana na makampuni ya madini kuhakikisha kwamba, wajibu ama majukumu yoyote ambayo yako ndani ya makampuni ya madini, yanatimizwa na kutekelezwa kama ambavyo inapaswa iwe. Kwa hiyo, mpaka sasa hakuna matatizo na tunaendelea kutekeleza majukumu ambayo pande zote mbili katika mikataba inayohusika imejiwekea. Kwa hiyo, kuhusu suala la *Williamson Diamond Limited* mpaka sasa hivi tunavyoongea, hakuna mgogoro wowote wa kimajukumu.

Na. 22

**Askari Waliopigana Vita ya Kagera**

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Askari waliopigana Vita ya Kagera mwisho wa miaka ya 70 walifanya kazi nzuri mpaka Taifa linajivunia ushindi huo hadi leo; na kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliieleza Bunge kuwa hadi wakati huo Serikali ya Uganda ilikuwa inaendelea kuilipa Serikali ya Tanzania gharama ya Kagera:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa kifuta jasho mashujaa (askari) waliopigana vita hiyo ikizingatiwa kwamba walipigana ndani na nje ya mipaka yetu?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sheria ya Ulinzi wa Taifa Na. 24 ya mwaka 1966 kifungu cha 20(1) – (2), kinampa Rais mamlaka ya kuyaingiza majeshi vitani na kifungu cha 20(3) kinampa mamlaka ya kutoa tamko la kusimamisha vita na kuyarudisha majeshi majumbani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa vifungu vya sheria nilivyovitaja hapo juu, mashujaa (askari) wote walikwenda vitani kwa kuzingatia sheria za nchi. Kwa mujibu wa kifungu cha 1.02 cha juzulu ya kwanza ya taratibu za Jeshi *(DFR VOL-1)*, yaani utawala, kinatafsiri Majeshi ya Ulinzi kuwa na Muungano wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania au Jeshi la Kudumu *(Regular Force)*; Jeshi la Mgambo *(Volunteer Reserve)*, ambalo linaundwa na wastaafu wa Jeshi la Ulinzi ambao hawajafikisha miaka mitatu toka kustaafu; Jeshi la Mgambo (*Volunteer Reserve*) ambalo linaundwa na nguvu ya wananchi na wanajeshi wanaojitolea kuwa mgambo baada ya kustaafu; na Majeshi mengine ya Taifa *(Other Disciplined Forces)* kama Polisi, Magereza, JKT, Usalama wa Taifa, *PCB*, wanyama pori na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika hali hiyo askari wote walioshiriki kupigana vita vya Kagera, walilipwa kifuta jasho chao bila kubagua aina ya jeshi. Kifuta jasho kilichotolewa kwa askari waliopigana Vita vya Kagera kilijulikana kama ASANTE NYERERE, ambacho kilikuwa ni kati ya Sh.600 hadi 700, ikiwa ni sawa na mshahara wa askari *private* wakati huo na kilitolewa kwa kiwango cha mshahara wa miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, kisheria ni kwamba askari wote waliokwenda vitani, walikwenda kwa utaratibu unaoeleweka na walirudi kwa utaratibu uliowekwa. Kwa maana hiyo, askari wote waliokwenda kwa utaratibu walilipwa stahili zao. Kwa kuwa majeshi ya ulinzi kisheria yanapoingia vitani yanakuwa chini ya amri moja ya kijeshi na chini ya utaratibu mmoja wa utawala wa jeshi.

Kama yupo askari ambaye alipigana Vita vya Kagera na hakulipwa stahili yake, hilo ni suala la mtu mmoja ambaye hakulipwa, huenda ni kutokana na sababu maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa askari ambao walikuwa ni waajiriwa wa jeshi, baadhi yao walipandishwa vyeo, wengine walipelekwa kozi mbalimbali ili waweze kupandishwa vyeo na pia zilitolewa nishani maalum kwa washiriki wa Vita vya Kagera, ikiwa ni pongezi kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kumng’oa Nduli Idd Amin Dada.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mimi kwa mtazamo wangu nilikuwa naona kwamba kifuta jasho kilichotolewa labda pengine kilikuwa si sahihi sana, lakini inawezekana kwamba ilikuwa ni sahihi kwa sababu miezi mitatu ni mingi. Sasa hivi naona mambo ya uvamizi au ujambazi yamezidi, kwenye *briefing* jana ilizungumzwa kwamba watalii walivamiwa, Tanga kuna wavamizi, jimboni kwangu watu wanavamiwa ovyo ovyo, kule Kipatimu watu wamevamiwa, sasa hilo suala nina wasiwasi kwamba kifuta jasho kile hakikuwatosha ndio maana wameamua kuwafundisha hata watu wengine ambao hawajui mambo ya medani za kivita, wakafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili nataka kuuliza hii *Tanganyika Legion* ambao walipigana Vita Kuu ya Kwanza zamani, je, mpaka sasa chama hicho kinaendelea, wanalipwa na nani au wanalipwa vipi na kwa nini na sisi tusifanye hivyo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, utajibu swali la kwanza la nyongeza na la pili ni swali jipya kabisa la *Tanganyika Legion*.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifuta jasho kilichotolewa mwaka 1979/1980 kama nilivyoeleza, kilikuwa mshahara wa *private* wa miezi mitatu, wakati huo *exchange rate* ilikuwa ni shilingi nne kwa dola na zilikuwa ni kama dola 450. Fedha hizo zilikuwa ni nyingi, kiasi ambacho Mwananchi wa Tanzania alikuwa anaweza kununua nyumba hata mbili.

Mheshimiwa Spika, ujambazi hauendani na suala la kifuta jasho, ujambazi ni utamaduni wa mtu mmoja mmoja, hausababishwi na wanajeshi ambao walienda vitani.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kuokoa muda, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa majibu ya ziada.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako, naomba kujibu swali la *Tanganyika Legion*.

**SPIKA:** Sawa, ninaruhusu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Suala la *Tanganyika Legion*, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Samson F. Mpanda kwamba, chama hicho bado kipo, kinalipwa na Serikali ya Uingereza. Tatizo ni kwamba chama hicho kilikuwa kimeingia katika mgogoro mkubwa wa uongozi, ikafika mahali mtu mmoja akawa anachukua hela anawalipa anaowachagua yeye, tukaingilia kati na tukaomba Serikali ya Uingereza isimamishe mpaka mgogoro huu tuumalize. Hivi sasa

tunakutana Wizara tatu; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Usalama wa Raia, kujaribu kuhakikisha kwamba suala hili tunalipatia ufumbuzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Kwa upendeleo maalum Mheshimiwa John Samuel Malecela, Mbunge wa Mtera, uliza swali la nyongeza.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri kutoka kwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kuuliza swali la nyongeza. Suala hili la watu waliopigana katika vita ya pili kudai kwamba wana maslahi fulani wanayolipwa na Serikali ya Uingereza lakini hayawafikii, limekuwa ni tatizo kwa sisi Wabunge wote wachaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila unapokwenda wanauliza pesa zetu ziko wapi? Sasa maadam njia ambayo Waziri ameijibu inaonesha kwamba fedha hizo zipo, mimi naomba katika Bunge hili, atupe utaratibu wa fedha hizo ambazo zilikuwa zikiliwa na mtu mmoja, kwa sababu nina hakika tutakaporudi kwenye majimbo yetu, watu wataanza kutubana fedha zetu ziko wapi? Asante.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa John S. Malecela, Mbunge wa Mtera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zile fedha alizokuwa akichukua huyu mtu mmoja alikuwa anawapa baadhi ya watu na watu wenyewe ni wale wapiganaji wanaokaa Dar es Salaam peke yake. Kwa hiyo, hata nitakapokupatia takwimu zake, hazitakuwa fedha ambazo utasema sasa nipe na mimi nikawalipe wa kwangu. Utaratibu ambao walikuwa wakiutumia kwa jinsi alivyokuwa akitueleza kwa maelezo ya awali ni kwamba, alikuwa anatumia fedha zake kutoka mfukoni, anawalipa na baada ya kuwalipa anachukua na zile *invoice* ambazo sisi tunatumia kuwalipa, anaziwakilisha katika Serikali ya Uingereza na Serikali ya Uingereza wanam-*refund*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kitu cha msingi tunachoomba ni kwamba, tupewe nafasi sisi Wizara tatu, tuharakishe kufikia ufumbuzi wa tatizo hili ili tuweze kuwasaidia hawa wazee wetu ambao wanataabika. Ni kweli hili ni tatizo la nchi nzima, hata juzi Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuja pale Urambo, kuna mzee mmoja alikuja akajitokeza anadai na akasema atasoma hata dua za kuwalaani wale watu wanaokula hela yake wafe. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie kwamba tunajitahidi. *(Kicheko)*

Na. 23

**Usikivu/Uonekanaji wa Redio/TV – Newala na Mtwara**

**MHE. KAPT. GEORGE H. MKUCHIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa vyombo vya habari, hususani Redio na Televisheni ya Taifa ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa kwa sababu vinapasha habari, kuelimisha na kuburudisha; na kwa kuwa usikivu wa Redio Tanzania ni hafifu sana hasa saa za asubuhi kwa Mkoa wa Mtwara na Wilaya ya Newala na vile vile Televisheni ya Taifa haionekani kwa Wilaya ya Newala na mkoa mzima wa Mtwara mpaka kuweka ungo ambao wananchi wengi hawamudu gharama zake:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, kutosikika kwa Redio Tanzania na kutoonekana kwa Televisheni ya Taifa bila kuweka ungo kunawanyima wananchi wa Newala na Mkoa wa Mtwara, fursa ya kupata habari, kuelimishwa na Televisheni na kuona matukio ya kitaifa?

(b) Kwa kuwa kusikiliza Redio Tanzania na kuona Televisheni ya Taifa ni haki ya wananchi wa Newala na Mkoa wa Mtwara na Watanzania wote kwa ujumla; je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba, wananchi wa Newala na Mtwara wanapata huduma za Redio na Televisheni ya Taifa usiku na mchana bila vikwazo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George H. Mkuchika, Mbunge wa Newala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kutosikika kwa Televisheni ya Taifa bila kuweka ungo kunawanyima wananchi wa Newala na Mkoa wa Mtwara, fursa ya kupata habari, kuelimishwa, kupata burudani na kuona matukio ya Kitaifa. Hata hivyo, napenda kusisitiza kuwa Serikali inatambua umuhimu na haki ya msingi na ya Kikatiba ya kila Mtanzania kupata habari, elimu na burudani kutoka vyombo vya habari vya RTD na TVT. Hivyo basi, wananchi wa Newala nao wanastahili kupata haki hiyo.

(b) Serikali imechukua hatua za kujaribu kutoa fursa hiyo ya kusikika Radio Tanzania na Televisheni ya Taifa kwa nchi nzima. Hata hivyo, mtambo wa Televisheni ya Taifa ulioko Lindi na mtambo wa radio ulioko Nachingwea, kwa sasa haina nguvu za kukidhi matarajio hayo. Tunategemea kuwa Serikali kwa siku zijazo, itajitahidi kuongeza nguvu za vyombo hivyo ili Televisheni ya Taifa ionekane na Radio Tanzania isikike Newala.

**MHE. KAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshukuru Naibu Waziri, kwa majibu ambayo mimi sikuridhika nayo. Mawasiliano ni Radio na TV na Waziri amelieleza Bunge hapa kwamba kwenye TV kuna matatizo, Nachingwea kuna matatizo ya radio, sasa nitafarijika sana kama katika haya mawili, walau moja litaboreshwa, hasa la radio, maana inasikilizwa na watu wengi kuliko TV.

Je, Mheshimiwa Waziri kwa kutambua kwamba Mikoa ya kule mpakani Mtwara, Lindi na Ruvuma, radio ya nchi jirani ya Msumbiji inasikika sana kwa sababu wakati wa vita Mreno, aliimarisha radio kwa ajili ya kufanya *propaganda*.

Je, anaweza kuliahidi Bunge hili kwamba Serikali sasa kwa kuzingatia kuwa mikoa ya pembezoni hatuna mawasiliano, itachukua hatua za haraka ili wananchi wa Jimbo la Newala wapate kusikiliza Sherehe za Uhuru na Jamhuri na Sherehe za Mapinduzi zinazofanywa Uwanja wa Taifa kama wanavyosikia wa mikoa mingine ili vijana wa shule za msingi waweze kufuatilia masomo ya historia darasa la sita na hesabu darasa la saba, kama wanavyofanya katika mikoa mingine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kapt. George h. Mkuchika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la vituo vyetu vya *television* hasa anachokizungumzia Mheshimiwa Mbunge katika eneo la Lindi, kina uwezo wa *kilowatts* tano tu na bado nguvu yake si kubwa sana, lakini namhakikishie tu kwamba, Serikali tuna mkakati wa dharura na wa haraka kuhakikisha kwamba radio hii ya Kituo cha Lindi inanasa katika maeneo ya Newala na sehemu nyingine za Mkoa wa Mtwara. Hata hivyo, katika mikoa ya pembezoni (Mtwara, Lindi, Kigoma, Rukwa na Kagera), upo mkakati mahsusi ambao tunautarajia kwamba, utakuwa umetekelezeka itakapofika Septemba, 2007 na harakati nyingine za kuendelea kuboresha *Television* ya Taifa na radio zinaendelea kwa kasi kubwa.

Na. 24

**Tishio la Homa ya *Rift Valley***

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilitangaza kuwepo kwa Ugonjwa wa Homa ya *Rift Valley* ambayo imeingia nchini ikianzia Mkoa wa Arusha, Tanga na baadaye Mkoani Dodoma ambako wangonjwa wengi wamethibitika kupatwa na homa hiyo na kuwafanya wakazi wa mkoa huo kuingiwa na hofu kuu kutokana na hali hiyo:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani za dharura za kulishughulikia tatizo hilo ili lisiendelee kuathiri maeneo mengine ya nchi ambayo hayajaathirika?

(b) Je, Serikali imefanya utafiti wowote kuthibitisha kama mbu anaambukiza maradhi hayo kutoka kwa mgonjwa aliyeathirika kwenda kwa mtu mwingine?

(c) Je, Serikali imeandaa mikakati gani ya muda mrefu ya kupambana na maradhi kama haya kwa siku za baadaye?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, kwanza napenda kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa *(Rift Valley Fever)*, husababishwa na aina ya virusi ambavyo kwa kitaalamu hujulikana kama *Phlebovirus*. Ugonjwa huu huathiri zaidi wanyama kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo na ngamia na mara chache huathiri pia hata binadamu. Aidha, nchi zilizo kwenye Ukanda wa Bonde la Ufa kama vile Tanzania, Kenya, Uganda, Somalia, Ethiopia na Sudan, ndizo ambazo huathirika zaidi na ugonjwa huu, ambao hutokea zaidi wakati na baada ya kipindi cha mvua kubwa na mafuriko ambapo kuna mazalia mengi ya mbu waenezao ugonjwa huu.

Baada ya maelezo haya sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ili kuhakikisha kuwa ugonjwa huu hauendelei kuathiri maeneo ya nchi ambayo hayajaathirika, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imechukua hatua mbalimbali na baadhi yake ni kama zifuatazo:-

- Kutoa taarifa za kuwepo kwa ugonjwa huu nchini katika mikoa yote ya Tanzania kupitia Makatibu Tawala wa Mikoa.

- Kusambaza *Fact Sheet* na Ainisho la Ugonjwa *(Standard Case Definition)* katika mikoa yote ya Tanzania Bara ili utambuzi wa ugonjwa kwa binadamu uweze kufanyika mapema.

- Kupeleka timu ya wataalam kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kufanya ufuatiliaji katika mikoa iliyoathirika.

- Kutoa mafunzo kwa watumishi wa afya kuhusu Homa ya Bonde la Ufa. Mafunzo haya yamefanyika katika Mikoa ya Arusha, Tanga, Dodoma, Iringa na Morogoro.

- Vielelezo mbalimbali vya uelimishaji kama vipeperushi, vimesambazwa mikoa yote ya Tanzania Bara. Aidha, utoaji wa elimu ya afya kwa umma unaendelea kwa njia ya *Television*, Radio na Magazeti.

- Mikutano na wadau mbalimbali imekwisha kufanyika ili kujadili namna ya kukabiliana na ugonjwa huu. Mikutano hii ilijumuisha wadau toka Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Wahisani. Vile vile, wahisani walifanya mkutano na Mheshimiwa Waziri Mkuu na wameonesha nia ya kusaidia katika kutoa fedha. Maombi ya fedha ya *USD* 12,336,964 yameainisha kwa ajili ya mikakati ya muda mfupi na mrefu.

- Mikutano na viongozi wa mikoa iliyoathirika Dodoma, Manyara, Singida, Morogoro na Iringa ili kufanya tathmini na kuweka mikakati zaidi ya kukabiliana na tatizo pamoja na wataalamu wa afya na mifugo.

(a) Tafiti mbalimbali zilizokwisha kufanyika Duniani kote zinaonesha kuwa upo uwezekano wa maambukizi kutoka kwa mgonjwa kwenda kwa mtu mwingine kupitia mbu. Hata hivyo, kiwango kikubwa cha maambukizi ni kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu kwa kula nyama yenye virusi ikiwa mbichi au isiyoiva vizuri au kunywa maziwa yasiochemshwa kutoka kwa mnyama aliyeambukizwa. Aidha, upo pia uwezekano wa kuambukizwa kwa kugusa/kushika damu au maji maji ya mnyama aliyeathirika iwapo mgusaji ana jeraha.

(b) Serikali imeandaa mikakati ifuatayo ili kupambana na maradhi kama haya kwa siku za baadaye:-

- Kuhakikisha kuwa viashiria vya utabiri wa ugonjwa huu vinaboreshwa ili kuweza kujiandaa vyema kabla ya mlipuko wa ugonjwa huu kutokea.

- Kudhibiti mbu waenezao ugojwa *(Vector control)*, pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa ugonjwa huu kwa wanyama *(Animal Surveillance)*.

- Kutoa mafunzo kwa watumishi wa afya na mifugo kuhusiana na ugojwa huu.

- Kutoa elimu ya afya kwa jamii kuhusu ugonjwa huu kwa kushirikiana na sekta zote.

- Kuboresha uwezo wa maabara za hapa nchini (za binadamu) katika kuchunguza na kuthibitisha Ugonjwa wa Bonde la Ufa na magojwa mengine yatakayoweza kujitokeza. Kwa sasa sampuli za wagonjwa hupelekwa Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Kenya *(KEMRI)*, kwa ajili ya uchunguzi. Hadi jana Wizara yangu imeshakaa kuona jinsi ya kufanya *reallocation fund* ya bajeti ya kununulia kifaa kiitwacho *bio-septic cabinet*, chenye thamani ya shilingi za Kitanzania milioni 40. Wataalam wapo na eneo la maabara lipo pale *Muhimbili National Hospital* ambapo maabara hii itafanya kazi.

- Kuendelea na zoezi la uchanjaji wa mifugo pamoja na kuogeshwa kwenye majosho.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba Serikali imekuwa ikihamasisha na ikitangaza ugonjwa huu nchi nzima, lakini kutokana na mazingira ya nchi yetu na kutokana na mawasiliano kutowafikia Watanzani wote, kwa

wale wafugaji wa vijijini ambao maeneo yao hayafikiwi na vyombo vyovyote vya habari au mawasiliano na mfugaji kama mnyama wake akiugua hayuko tayari kumwona anakufa, anaamua kumchinja na kuanza kumuuza na sehemu hizo hakuna madaktari wa kuthibitisha kwamba mnyama yule ana tatizo. Je, Serikali inasema nini katika hili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Njia tunayotumia sisi kuwafikia hao wafugaji walioko kwenye maeneo ambako ni vigumu kupata taarifa au magazeti kufika ni Uongozi wa Wilaya na mpaka sasa hivi tumekutana na zaidi ya viongozi wa wilaya 30 na kesho tuna kikao na viongozi wengine waliobaki.

Mheshimiwa Spika, njia ya pili ni kuzuia ugonjwa usifike maeneo ambako watu kama hao anaowasema Mheshimiwa Mbunge wanakoishi na tunafanya hivyo kuzuia kwa kutumia kuchanja mifugo wanaozunguka maeneo ambako kuna ugojwa ili kuzuia virusi au ugonjwa kuvuka na kwenda maeneo ya mbali zaidi. Ndio njia mbili ambazo tunazitumia na mpaka sasa hivi zinafanya kazi vizuri na tunaomba tushirikiane kwa kupitia Wabunge ili taarifa hizi za tahadhari zilizotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, ziweze kuwafikia Wananchi wote.

Na. 25

**Ujenzi Holela - Dar es Salaam**

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la ujenzi wa nyumba kwa kutofuata mpangilio limekithiri sana katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam kama Mbagala, Kimara, Ukonga Mombasa, Gongo la Mboto, kuelekea Pugu, pamoja na maeneo mengine:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuyaangalia maeneo yaliyojengwa ovyo kama mbinu mojawapo ya kuboresha Miji ili kuepuka ubomoaji wa nyumba wakati inapohitajika kupanua barabara?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Amina C. Mpakanjia, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kwanza kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000, inaeleza kuwa nyumba ambazo zimejengwa katika maeneo ambayo hayajapangwa katika miji yetu hazitabomolewa, bali maeneo hayo yataboreshwa kwa kuwekewa huduma muhimu za kiuchumi na kijamii kwa kushirikisha wananchi, taasisi na asasi mbalimbali, pamoja

na Serikali.  Wizara katika  kutekeleza sera hiyo, itaandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwa maeneo ya pembezoni mwa Miji na kupimwa mapema ili yajengwe kwa mpangilio, hivyo, suala  la ubomoaji  wa nyumba halitarajiwi kuwepo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina C. Mpakanjia, kama ifuatavyo:-

Maeneo yaliyojengwa kiholela katika Jiji la Dar es Salaam ni asilimia 75 na asilimia 25 ndio iliyopangwa.   Asilimia 75 ya wakazi wote wanaishi katika maeneo haya. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuboresha makazi haya na kuongeza usalama wa miliki kwa wakazi wake.  Katika  mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri  za Jiji  la Dar es Salaam, ilitekeleza  mradi  wa kutambua miliki na kuwapatia leseni za makazi kufuatana na sera na Sheria ya Ardhi  Na. 4 ya 1999.  Jumla ya miliki 230,000 zilitambuliwa na wamiliki 65,000 wameshachukua  leseni zao.  Wananchi wameweza kuzitumia leseni hizi kwa ajili ya kujipatia mikopo katika vyombo vya fedha.

Katika  kutekeleza  awamu ya pili ya Mradi huu,  Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam na asasi za miundombinu,  imeandaa  mkakati  kwa ajili ya kuendeleza maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam, wenye lengo la kudhibiti ukuaji  usio wa mpangilio.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji awamu ya pili ya Mradi huu, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam na asasi za miundombinu imeandaa mkakati kwa ajili ya kuendeleza maeneo ya pembezoni mwa jiji la Dar es Salaam wenye lengo la kudhibiti ukuaji wa usio wa mpangilio.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mkakati huu ulishaanza katika mwaka wa fedha 2006/2007, kwa maeneo yaliyopo ukanda wa barabara iendayo Morogoro kati ya Kimara na Kiluvya katika Manispaa ya Kinondoni na maeneo mengine yatafikiwa hatua kwa hatua.  Aidha, maeneo haya yalishaandaliwa mipango ya kina *(Detailed Planning Schemes)*, inayoonesha aina ya huduma zinazotakiwa kuendelezwa, pamoja na matumizi ya ardhi. Kwa kuwashirikisha wananchi, maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya huduma, yataainishwa na kutwaliwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza na kuwaasa wananchi wote kushirikiana na Halmashauri zao, kuandaa mipango ya kusimamia uendelezaji wa maeneo yao na kuacha kujenga kwenye maeneo yasiyopimwa. Ujenzi wa namna hiyo unawakosesha huduma muhimu kama vile barabara, maji, shule na zahanati.  Naomba wananchi wote baada ya kupata maeneo yaliyopangwa na kupimwa, wajenge kwa kufuata kanuni za mipango miji.  Vinginevyo nchi yetu itaendelea kuwa na miji iliyojengwa bila mpangilio.

**MHE.  AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili yanyongeza:-

Kwanza, kwa mujibu wa majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyasema ni kwamba, kwa sasa hivi hawatarajii tena kubomoa nyumba, hiyo ikiwa ni Sera ya Taifa ya Ardhi. Swali langu linakuja kama ifuatavyo: Katika agizo ambalo alilitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusiana na wafanyabiashara ambao walikuwa wakifanya biashara katika Mkoa wa Dar es Salaam, maarufu kwa jina la machinga, ambao wengine walikuwa wamejenga kiholela holela Kariakoo na maeneo mengine, alisema kwamba, watu wale waondolewe na kama kuna vibanda vibomolewe.

Matokeo yake bomoa bomoa ile ikaenda mpaka ndani ikagusa na maeneo mengine kabisa ambayo sidhani kama yalikuwa na tatizo, maeneo kama Mikocheni, Masaki, Kawe na mengine. Watu walibomolewa kabisa maeneo yao na hapa Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba hawatarajii kubomoa, kwa hiyo, naomba anipe jibu ilikuwaje wakabomoa katika yale maeneo mengine ambayo ilikuwa ni tofauti halafu leo ananiambia bomoa bomoa hakuna?

Swali la pili ni kwamba, kwa kuwa ujenzi holela huathiri afya na hali ya maisha ya wananchi wa maeneo ambako nyumba zimejengwa kwa msongamano hata miundombinu ya maji na umeme kuwafikia wananchi huwa inakuwa ni kazi ngumu sana na maeneo haya ya msongamano ambao wakati wa magonjwa ya milipuko kama kipindupindu huwa yanaathirika sana, binafsi ninaamini hiki ni kinyume na haki za binadamu; Je, Serikali inasema nini kuhusiana na hili katika maeneo ambayo yamejengwa kiholela na bado yapo kiholela na wananchi wanaathirika sana kwa hayo ambayo nimeyataja? Naomba majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amina C. Mpakanjia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri mimi ni Mbunge wa Dar es Salaam na ni Mjumbe katika Manispaa ya Kinondoni. Katika Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, ndio tumesema kwamba, tutatambua makazi na tukisema hivyo tunamaanisha makazi ya watu yaliyojengwa kiholela, ikiwa na maana watu waliokuwa wamejenga maeneo kadhaa kwa mfano, Keko, Manzese, Mbagala na maeneo mengine ambayo nina hakika Mheshimiwa Mbunge anayafahamu. Wale hatutawavunjia ila tutaboresha kwa kuwapa leseni na kutengeneza miundombinu kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha. Lakini wale waliokuja kufanya biashara katika maeneo yasiyohitajika ni uvunjaji wa sheria na ndio sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliagiza kwamba kuanzia hivi sasa maeneo hayo tuyaondoe na vile vile tuboreshe na kuwatafutia wafanyabiashara hao maeneo ambayo tumekwisha watafutia katika manispaa zote tatu za Dar es Salaam. Vile vile nikizingatia swali la Mheshimiwa limeonesha maeneo ya Kata mbalimbali za Dar es Salaam, ambazo siyo katikati ya miji, akatoa mfano wa Mikocheni, nako pia katika mpango mzima wa Jiji la Dar es Salaam ilihusika siyo kwamba ilikuwa ni pale katikati kwenye Kata ya Kivukoni na Kata ya Mchikichini.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la hali ya msongamano katika maeneo ya jiji ambayo inasababisha magonjwa mbalimbali, Serikali imejitahidi na imeanza kutumia *pilot project* katika maeneo kadhaa kama Manzese, Hananasifu na tumeonesha wananchi

kama tunaweza kuboresha maeneo yale ambayo yamejengwa kiholela kwa kubomoa baadhi ya majengo lakini kwa kushirikiana na wananchi kuweza kupata miundombinu mbalimbali kama njia ili itokeapo dharura yoyote kama moto, maji machafu na madhara kama hayo ya kipindupindu, tuweze kunusurika na pia tuweze kuwafikia wananchi kwa urahisi. Tumepata fedha kutoka *HABITAT* na tumeweza kufanya maeneo ya Manzese na Hananasifu, wamechanga wenyewe kwa Mpango wa Benki ya Dunia na tunazihamasisha Manispaa nyingine zilizobaki, wafanye mipango hiyo kwa kushirikiana na Serikali.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Kanuni Namba 50(8) ambayo inasema kwamba ni marufuku kwa Mbunge yeyote akiwemo na Waziri kutumia lugha ya kuudhi.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, kuhusiana na fedha za miradi ya umeme, alitumia ya lugha ya kwamba binadamu tuna tabia ya kusahau, kwa maana ya kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge tunapoihoji Serikali kwa matumizi ambayo inayafanya, haina maana kwamba tunasahau ni katika kutimiza jukumu letu la kuhoji ambalo ni jukumu la Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kuhusiana na suala hili. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jibu kuhusu swali alilolisema Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto ni kwamba, yeye mwenyewe amekosea kwa sababu kilichosemwa ni kweli. Alichokisema Waziri ni kwamba, binadamu tuna tabia ya kusahau, alikuwa anahusisha tatizo lililotukumba mwaka 2006, ambapo chanzo cha maji na mabwawa kwa ajili ya umeme kilikuwa kimekauka na nchi ikapata tabu. Sasa swali la Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, lilikuwa linakwenda katika kusema kwamba ukombozi wetu tena ni mabwawa, mimi nilivyomwelewa, Waziri alikuwa anatukumbusha kwamba mabwawa hayawezi kuwa ndio ukombozi wa kudumu mbona tumesahau ya mwaka 2006? Kwa maana hiyo kama umekereka basi hilo ni tatizo lako, wenzio tumeelewa na kwa hiyo, sasa naendelea na hatua inayofuata ambayo ni kusoma matangazo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika *Speaker's Gallery* tunao wageni wafuatao na nitaomba kila nimayemtaja asimame; tunaye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya *NMB*, Bwana Misheck Ngatunga, tunaye Afisa Mtendaji Mkuu, Bwana Ben Christias, *welcome to Dodoma and specifically to Parliament, many of your depositers are here and I know today we are going to a function together with you, thank you very much*, tunaye Meneja wa Uhusiano wa *NMB*, Bi Shairose Bhanji. Kumekuwa na uvumi kwamba Bi Shairose Bhanji hivi karibuni atafunga ndoa, kwa hiyo, kama uvumi huu ni kweli, napenda kwa niaba ya Bunge, kumwombea heri na mafanikio katika shughuli hiyo, pia tunaye Meneja wa Kanda ya Magharibi Benki ya *NMB,* Bwana Abraham Agustino na tunaye mgeni mwingine, mama Noni karibuni sana. *(Makofi)*

Naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba, leo hii tuna hafla iliyogawanyika sehemu mbili; hafla hii ya *NMB* inahusu kufungua kituo cha malipo cha

Benki ya *NMB* katika Jengo la Utawala. Sasa utaratibu ni kama ufuatao, mara baada ya Shughuli za Bunge kusitishwa hapo saa 7.00 mchana, Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuelekea kwenye eneo lililoandaliwa kwa ajili ya chakula hapa chini kwenye ule ukumbi wetu wa hapa katika Jengo Jipya tunaouita ukumbi wa sherehe. Nendeni moja kwa moja kwa sababu *NMB* imeandaa chakula cha mchana na kutakuwa na hotuba ya Naibu Waziri wa Fedha na kadhalika, ni jambo rasmi kabisa, wote mnakaribishwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Makamishna wa Tume ya Huduma za Bunge na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, wataongozana nami na Waziri wa Fedha, twende kwenye eneo kuwawakilisha Waheshimiwa Wabunge kufungua kile kituo. Kwa hiyo, badala ya kwenda moja kwa moja kwenye sherehe, Makamishna wa Tume ya Huduma za Bunge na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, tutafuatana na Waziri wa Fedha au Naibu Mawaziri wa Fedha wale wawili twende kule. Shughuli ni fupi sana, tunakata utepe na kuweka sahihi kwenye kitabu, baada ya hapo tunarejea kwenye ukumbi wa sherehe kuungana na Wabunge wote kwa ajili ya chakula cha mchana. Sasa hilo ndio linahusu hafla ya leo saa 7.15 mchana.

Nafurahi sana kuwakaribisha wageni wengine ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Kiislam cha Al-haramain kilichopo Dar es Salaam, nadhani wamekuja na walimu wao, tafadhali wasimame pande zote mbili. Karibuni sana vijana wetu kwani kila mara tunafurahi sana walimu mnapowaleta vijana hapa pahala ambapo ndipo kitovu cha demokrasia katika nchi yetu, waone jinsi Bunge linavyofanya kazi yake. Karibuni na mtakaporejea, basi tunawatakia safari njema na kama Rais wetu anavyosema, mfanye bidii sana kwenye masomo kwani Tanzania inawahitaji. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Said Amour Arfi, ameniomba nitangaze wageni wake ambao ni watatu; Binti yake anaitwa Sabra Arfi, ambaye amefuatana na rafiki zake, yaani Eva na Happy. Hawa ni wanafunzi wa Chuo cha Uuguzi Kilimatinde – Manyoni, ambao wamekuja Dodoma kuongeza idadi ya wauguzi katika Hospitali na Mkoa na wanashughulika sasa na mlipuko wa Homa ya Bonde la Ufa. Poleni sana na kazi ngumu, Dodoma tuna wagonjwa wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Haroub Said Masoud, ameniomba nitangaze kuwepo kwa wageni wake kama ifuatavyo: Ndugu Silima Hassan ni Mwalimu kutoka Mwera Zanzibar, naomba asimame, Ndugu Issa Haroub ni mwanafunzi kutoka Mwera na Ndugu Juma Hassan, ambaye ni Msaidizi wa Mbunge. Karibuni sana na poleni kwa safari kutoka Zanzibar kwani ni safari ndefu mpaka ufike hapa Dodoma lakini nadhani mnafurahi kuwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka, ameniomba nimtangaze mgeni wake, anaitwa Bw. Herma Pius, ambaye anatoka *Umbwe Secondary School.* Karibu sana kijana, wosia wangu ni uleule kwamba, mfanye kazi kwa bidii kwani nchi hii inahitaji msome mpaka ukomo wenu na mipango ya Serikali ya Awamu ya Nne ni mizuri mtafika popote mtakapoweza, karibuni sana.

Kuna taarifa hapa ya kikao, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, ameniomba nitangaze kuwa kutakuwa na mkutano leo tarehe 11 Aprili, 2007 saa 07:00 mchana, lakini napendekeza Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba, kikao kiwe baada ya chakula, tukitoka kwenye chakula basi Kamati ya Maliasili na Mazingira ikutane pale katika Ukumbi Namba 432, Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, nina shughuli nyingine nje ya ofisi, kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Naibu Spika, aje ili aweze kuendelea na shughuli za miswada. Natoa taarifa tu kwamba, hapa Mezani tumepokea wachangiaji watatu. Miswada ni mitatu na sidhani kama wasemaji wanaweza kuwa ni watatu tu, kwa hiyo, tunaomba wale watakaoweza waweze kuleta majina ili tuweze kufaidika na mjadala wa sekta hiyo ya ardhi. Asanteni.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwasalimia na ninaomba tuendelee na kazi.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara wa Mwaka 2007 *(The National Bank of Commerce (Re-organisational and Vesting of Assets and Liabilities) Bill, Cap. 404)*.

Muswada wa Sheria ya Watalaam wa Mionzi wa Mwaka 2007 *(The Medical Radiology and Imaging Professionals Bill, 2007).*

*(Miswada ya Sheria iliyotajwa hapo juu, ilisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

Muswada wa Sheria ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa na Kutekeleza Masuala Mbalimbali yanayohusu Mipango Miji *(The Urban Planning Bill, 2006).*

Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Usajili ya Mipango Miji wa Mwaka 2006 (*The Town Planners (Registration) Bill, 2006).*

Muswada wa Sheria ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa, Kuendesha na Kutekeleza Sheria ya Mipango ya Ardhi *(The Land Use Planning Bill, 2006).*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunayo Miswada mitatu chini ya Wizara ya Ardhi, mtoa hoja ataiwasilisha Miswada hii kwa pamoja, hivyo hivyo Kamati iliyoshughulikia Miswada hii, itatoa maoni yake kwa Miswada yote mitatu kwa pamoja na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, naye atatoa maoni yake kwa Miswada yote mitatu, halafu Waheshimiwa Wabunge mtakapokuwa mnajadili, mtajadili Miswada yote mitatu, isipokuwa wakati wa kufanya maamuzi, tutafanya maamuzi kwa Muswada mmoja mmoja. Kwa hiyo, naomba tukiendelea tuzingatie hilo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha tena kuhudhuria kikao hiki cha Bunge.

Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, kwa michango yao iliyowezesha kuwasilisha Miswada hii Bungeni. Pia napenda kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuandaa Miswada hii. Aidha, shukrani za pekee, ziwaendee wadau wote walioshiriki kujadili Miswada hii kwa kina na kuleta mapendekezo ya kuiboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niichukue nafasi hii kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Mututura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Miswada ya Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi *(Land Use Planning Bill)* ya mwaka 2006, Sheria ya Mipango Miji *(Urban Planning Bill)* ya mwaka 2006 na Sheria ya Usajili ya Wataalam wa Mipango Miji *(Town Planners Registration Bill)* ya mwaka 2006, kama ilivyopangwa kwenye shughuli za leo, pamoja na marekebisho yake *(Schedule of Amendment),* zilizoambatanishwa sasa, isomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya ni mchakato wa kutekeleza Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, ambayo utekelezaji wake ulihusisha kuandaliwa kwa Sera ya Maandalio ya Makazi ya mwaka 2000 na kutungwa kwa Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999 na Sheria ya Mahakama ya Ardhi Namba 2 ya mwaka 2002, lakini Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 haijatungiwa Sheria ya Utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabili na kutatua matatizo na changamoto zilizobainishwa kwenye sera zilizotajwa, imependekezwa hatua mbalimbali zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kutungwa Sheria za kusimamia masuala ya mipango ya matumizi ya ardhi na taaluma yake. Baadhi ya maeneo yanayohitaji Sheria ni pamoja na taratibu za kuweka mipango ya matumizi bora mijini na vijijini kwa kutumia mbinu shirikishi, kuweka vigezo vya kuanzisha ngazi za makazi kwa ajili ya kijiji, miji midogo, miji, manispaa, jiji na jiji kubwa na kukasimu madaraka ya kuandaa na kutekeleza mipango na makazi kwa mamlaka za mitaa, kwa kadri ya uwezo wa mamlaka hizo utakavyoongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mengine yanayohitaji kutekelezwa kisheria ni kuhuisha mamlaka ya mahusiano ya mamlaka mbalimbali zinazohusika katika kupanga na kutekeleza mipango na matumizi ya ardhi, kuboresha mamlaka ya usimamizi wa Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi, kwa kutoa uwezo zaidi wa utekelezaji kisheria, kushirikisha Sekta Binafsi na kuweka kisheria taratibu na maadili ya wanataaluma wa mipango ya matumizi ya ardhi na kuendeleza taaluma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya yanalazimu kufuta na kurekebisha baadhi ya Sheria zilizopo hususan Sheria ya Mipango Miji na Vijiji, Sura Namba 378 ya mwaka 1956 na Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Namba 3 ya mwaka 1984.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mipango Miji Namba 378, pamoja na kuwa na mamlaka ya kusimamia upangaji wa matumizi ya ardhi mijini na vijijini, maudhui yake ni ya upangaji wa matumizi ya ardhi mijini tu. Aidha, Sheria ya Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Namba 3 ya mwaka 1984, inaipa Tume mamlaka ya ushauri tu bila kuwa na nguvu za kuratibu, kukagua na kudhibiti shughuli za upangaji wa matumizi ya ardhi zinazofanywa na asasi mbalimbali katika ngazi za Vijiji, Wilaya, Mikoa na Taifa.

Mapendekezo ya kuundwa kwa Sheria mpya ni kuwezesha kuunda Tume yenye nguvu za kiutendaji, kuanzisha mamlaka za upangaji matumizi ya ardhi na kuainisha taratibu, wajibu na madaraka ya vyombo hivyo kuanzia ngazi za vijiji, Wilaya, Mikoa na hadi Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya udhaifu wa Sheria zilizoelezwa hapo juu ni chimbuko la migogoro na migongano ya ardhi, ukosefu wa usalama wa milki za ardhi, kuibuka kwa matatizo yasiyo endelevu na rasilimali zake na uharibifu na uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua matatizo hayo, naileta Miswada hii mbele ya Bunge lako Tukufu kwa malengo ya kuhakikisha mipango ya matumizi ya ardhi inawezesha upatikanaji ardhi kwa watu wote ndani ya jumuiya wakiwemo wanawake, vijana, wazee, wenye ulemavu na makundi maalum yote ya jamii. Pia inapendekezwa kuzingatia masuala ya kulinda na kuhifadhi mazingira, kutoa fursa ya ajira ili kuondoa umaskini na kujenga uwezo kwa wote wanaohusika na mipango ya matumizi ya ardhi na kuhakikisha Sheria, Kanuni, viwango na udhibiti unaozingatia uwezo, mahitaji na malengo ya kila sehemu ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi *(Land Use Planning Bill, 2006)*, una ibara 68 zilizogawanyika katika sehemu tisa kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza ni utangulizi, inahusisha Jina la Sheria, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika.

Sehemu ya pili, ni msingi na malengo makuu ya sera yanayokusudiwa kutekelezwa na Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya tatu, yenye ibara ya 5 - 13 inahusu muundo wa utawala unaojumuisha majukumu mbalimbali kama Tume ya Matumizi ya Ardhi na kuteuliwa Mkurugenzi Mkuu wa Tume. Ibara ya 8 inapendekeza Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iwe na mamlaka ya kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na kushtaki Mahakamani ili kuhakikisha kuwa maagizo na maelekezo yake yanafuatwa kikamilifu.

Sehemu ya Nne, inahusu upatikanaji wa fedha za Tume na utungaji wa kanuni mbalimbali mfano ibara ya 14 – 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 5 yenye ibara 18 – 38 inaunda mamlaka ya upangaji, pia inaweka mchakato wa kutayarisha na kuhitimisha mipango.

Ibara ya 18 inapendekeza kuanzishwa kwa mamlaka za upangaji *(Planning Authority)*, mamlaka hizo ni Halmashauri za Vijiji, Halmashauri za Wilaya na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Ibara ya 20 inapendekeza Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ipewe mamlaka ya kitaifa ya upangaji wa matumizi ya ardhi yatakayojumuisha kuandaa Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi, Mipango ya Kanda na kuratibu utayarishaji wa mipango ya ardhi kutoka Wilaya kupitia sekretarieti za mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 6 inatoa mamlaka maalum kwa mamlaka za upangaji ikiwa ni pamoja na uwezo wa kutoa ardhi kwa makusudio ya kuipangia matumizi, kuiwekea mipaka, kuigawanya, kuipangilia upya na kuifanyia marekebisho. Afisa anayeruhusiwa na mamlaka ya upangaji kuingia ndani ya ardhi inayokusudiwa na kupangiwa matumizi, kutoa haki za matumizi ya ardhi na uhifadhi wa majengo ya kumbukumbu za kihistoria iko katika ibara ya 39 – 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 7 inajumuisha ibara ya 46 – 61, sehemu hii inaweka ulazima wa kuzingatia Sheria hii, udhibiti na utaratibu wa kazi za upangaji, hii ikiwa ni pamoja na utoaji ardhi wa lazima kwa kuzingatia mipango iliyoidhinishwa, pamoja na madaraka ya Mamlaka ya Upangaji katika kudhibiti matumizi ya ardhi. Sehemu hii pia inaelezea uwezekano wa kuweka mfumo ambao unaweza kutumiwa na mamlaka za upangaji, kutoa motisha kwa watekelezaji wa mipango kwa hiari. Sehemu hii vilevile inatoa uwezo wa mamlaka za upangaji kutoa ilani ya kuzuia uendelezaji unaofanywa kinyume na mipango. Aidha, inatoa nafasi ya rufaa kwa mtu anayejisikia kuathiriwa na ilani hiyo.

Ibara ya 51 inapendekeza kumpa Mkurugenzi Mkuu, madaraka ya kumteua afisa au mkaguzi wa kuendesha mashtaka, ambaye kwa idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka, ataendesha mashtaka yote dhidi ya kosa lolote litakalofanywa chini ya Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya 8 inabatilisha makosa, adhabu na faini, kwa waendelezaji wanaovunja masharti ya mpango ulioidhinishwa ibara ya 62 – 63.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 9 yenye ibara ya 64 – 68, inatoa maelezo ya jumla ikiwa ni pamoja na utungaji Kanuni kuhusu utoaji, urekebishaji wa utoaji wa mpango wowote ulioidhinishwa, Kanuni za kutoa ada, viwango vya upangaji, amri na maagizo mengine yoyote. Sehemu hii inawapa uwezo Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Upangaji, mtu yeyote aliyeruhusiwa kutoa ilani ya kupata taarifa kutoka kwa mtu yeyote kuhusu ardhi na maendeleo yake yanayohusika na mpango. Ibara ya 66 inapendekeza kufuta Sheria ya Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, sura namba 116.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Mipango Miji *(Urban Planning Bill of 2006),* una Ibara 81 zilizogawanyika katika sehemu saba kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza ni utangulizi, inayohusisha Jina la Sheria, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri ya baadhi ya maneno yanayotumika.

Sehemu ya pili, ni misingi na malengo makuu ya sera yanayokusudiwa kutekelezwa na Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya tatu, inatoa muundo wa utawala wa kitaasisi ukionesha majukumu na wajibu wa kila muhusika katika suala zima za ardhi.

Ibara ya 5 inapendekeza mwenye mamlaka ahakikishe kuwa misingi mikuu ya Sera ya Ardhi, Sera ya Taifa Makazi na Dira ya Maendeleo ya Taifa inazingatiwa katika mchakato mzima wa upangaji.

Ibara ya 6 inapendekeza kuajiriwa kwa Mkurugenzi wa Maendeleo ya Makazi, ambaye atakuwa Mshauri Mkuu na Msimamizi Mkuu wa Masuala ya Mipango Miji.

Ibara ya 7 inapendekeza Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Miji Midogo, ziwe na Mamlaka za Upangaji kwa mujibu wa Sheria hii. Ibara hiyo pia inapendekeza kutangaza chombo au taasisi kuwa na mamlaka ya upangaji, vilevile inapendekeza vigezo vya kuzingatiwa na Waziri Mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa katika kuweka ngazi za makazi kuanzia ngazi za kijiji, mji mdogo, miji, jiji, jiji kubwa na kadhalika katika jedwali namba 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 4 inaweka taratibu na mchakato wa upangaji ikiwa ni pamoja na utangazaji wa maeneo ya mipango, uandaaji wa mipango ya jumla na kina na mipango ya kurasimisha maeneo yaliyojengwa kiholela. Inatoa pia makusudio na mambo yanayotakiwa kuwepo kwenye mpango wa jumla, utaratibu wa uaandaji na kuidhinishwa marekebisho na kuhuisha ibara ya 8 – 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 5 inazipa uwezo Mamlaka za Mipango Miji, haki ya kununua ardhi kwa ajili ya kutayarisha mpango wa jumla, utoaji na ulipaji fidia. Pia inatoa haki ya Mamlaka za Upangaji kutoza ada za kuboresha eneo kutokana

na kutekelezwa kwa mpango. Aidha, inaweka taratibu za kusuluhisha migogoro inayohusu madai mbalimbali na hii iko katika ibara ya 61 – 72.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 6 inatoa mamlaka kwa ofisa au mtu yeyote aliyeruhusiwa kisheria, kuingia kwenye eneo la mtu kwa madhumuni ya kugawanya ardhi katika matayarisho, mpango au shughuli nyingine yoyote ya muda kwa lengo la kufanikisha utelezaji wa mpango au jambo lingine lolote linalohalalishwa kisheria. Hii ni pamoja na ibara ya 73 – 77.

Sehemu ya 7 na ya mwisho katika Muswada huu inahusu mambo ya jumla ikiwa ni pamoja na kutunga Kanuni, kufanya marekebisho na pia inahusu utayarishaji wa taarifa za mwaka na kufuta Sheria za Mipango Miji na Vijiji, Sura Namba 378. Aidha, Sheria mpya itaendelea kuheshimu vibali vyote vilivyotolewa na vitakavyotolewa kabla ya kufutwa kwa Sheria ya sasa ibara ya 78 – 82.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muswada wa Sheria ya Usajili wa Wataalam na Wana Mipango Miji *(Town Planners Registration Bill, 2006).* Muswada huu una ibara 31 zinazogawanyika katika sehemu 9 kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza, ni utangulizi inayohusisha Jina la Sheria, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika.

Sehemu ya pili, ni misingi na malengo makuu ya sera yanayokusudiwa kutekelezwa na Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya tatu, ni vifungu vya kuundwa kwa Bodi ya Maofisa wa Mipango Miji, kazi za Bodi na ukomo wa mamlaka yake hii ipo katika ibara ya 4 – 6.

Sehemu ya nne, inaruhusu kuteuliwa Msajili na kazi zake na ibara ya 8 inapendekeza kuwepo na Daftari la Usajiri la Wataalam wa Wana Mipango Miji, pia cheti cha usajili ibara ya 11 inapendekeza sifa na masharti ambayo mwombaji wa usajili anapaswa kuwa nazo.

Pia utaratibu wa kutuma na kujadili maombi hayo. Hayo yote yamefafanuliwa vizuri katika ibara ya 7 – 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya 5 yenye Ibara ya 15 – 20 inaweka taratibu za kufuta au kusimamisha usajili wa mtaalamu ikiwa ni pamoja na kuipa Bodi uwezo wa kumfutia na kumsimamisha usajili Mtalaam wa Mipango Miji, kufanya marekebisho ya usajili na kumrejeshea mtu usajili wake.

Sehemu hii pia inatoa utaratibu wa kuchunguza na hatua za kuchukua dhidi ya mtalaam atakayekataa wito wa kutoa ushahidi juu ya tuhuma yoyote itakayojitokeza. Mwisho, inatoa fursa ya kukata rufaa kwa mtaalam asiyeridhika na maamuzi yoyote dhidi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita inajumuisha ibara ya 21 – 25 zinazoweka mazingira ya kumzuia mtu asiye mtaalam wa Mipango Miji kufanya kazi za Mipango Miji.

Ibara ya 24 inapendekeza masharti kuhusu mtu ambaye hajasajiliwa kujiita msajiliwa ama kujifanya kuwa anazo sifa za msajiliwa, mtu huyo atafunguliwa mashtaka na endapo atathibitika kuwa ni kweli atapigwa faini ama atatozwa faini na kifungo cha kati ya miaka 3 – 5.

Aidha, Afisa Mipango Miji aliyesajiliwa anaweza kufanya kazi za Mipango Miji kwa ajili ya kupata faida. Pia makampuni yenye mtaalam wa Mipango Miji kama mshirika wake, yanaweza kufanya kazi za Mipango Miji.

Ibara ya 25 inataja makosa yanayohusiana na usajili ambayo ni pamoja na mtu au kampuni kuingiza jina kwa hila ndani ya daftari la usajili, kununua au kujaribu kununua usajili, kutoa taarifa za uongo kwa ajili ya kujipatia faida.

Ibara hii pia inapendekeza kiwango cha adhabu kwa atayepatikana na hatia kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi 500,000 au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 7 ni mambo ya jumla ikiwa ni pamoja na vyanzo vya mapato ya Bodi, utungaji wa Kanuni zitakazowawezesha kurahisisha utendaji kazi wa Bodi na hayo yote yamefafanuliwa vizuri katika ibara ya 26 – 31.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo heshima kuwasilisha Miswada ya kutungwa Sheria ya Matumizi ya Ardhi *(Land Use Planning Bill of 2006),* Sheria ya Mipango Miji *(Urban Planning Bill of 2006)* na Sheria ya Usajili ya Wataalam wa Mipango Miji *(Town Planners Registration Bill of 2006)* na kufuta Sheria ya Mipango Miji na Vijiji Sura Namba 378 na Sheria ya Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Sura Namba 116, pamoja na marekebisho yaliyofanywa katika Miswada hiyo, Bunge lako Tukufu lijadili na kuipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, hoja imetolewa na kuungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti au mwakilishi wa Kamati iliyohusika na Miswada hii.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA (k.n.y MHE. GIDEON A. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni Na. 70(2), Toleo la mwaka 2004, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, kuhusu Miswada ya Sheria kama ifuatayo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi *(The Land Use Planning Act, 2006);*

(ii) Muswada wa Sheria ya Mipango Miji *(The Urban Planning Act, 2006);* na

(iii) Muswada wa Kodi ya Usajili ya Mipango Miji *(The Town Planners (Registration) Act, 2006).*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote Kamati inaungana na Waheshimiwa Wabunge wote kutoa salaam za rambirambi kwa misiba iliyotokea miongoni mwetu, Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi, *Amin!*

Aidha, tunawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliopata nyadhifa mbalimbali katika Umoja wa Mataifa na Serikali yetu. Tunawatakia mafanikio mema. *(Makofi)*

Mwisho, Kamati inawapongeza na kuwakaribisha Waheshimiwa Wabunge wapya akiwemo Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Mbeya kupitia Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge kutoka Chama cha Mapinduzi, Jimbo la Tunduru, Mkoa wa Ruvuma, tunawatakia uwakilishi mwema. *(Makofi)*

Namshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kwa uwasilishaji wake mzuri kwa Miswada yote mitatu. Tunamshukuru Mheshimiwa Spika kwa kuruhusu kufanyika Semina ya Waheshimiwa Wabunge wote kuzungumzia Miswada hii. Natumaini baada ya kushiriki kwenye semina na kwa kuzingatia maelezo ya Mheshimiwa Waziri hivi punde, maudhui na madhumuni ya Miswada yote mitatu yatakuwa yameeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata nafasi ya kujadili Miswada hii mitatu katika vikao vitatu. Vikao viwili tarehe 15 na 19 Januari, 2007 vilikuwa kati ya Kamati na Uongozi wa Wizara na kikao kimoja tarehe 16 Januari, 2007 kiliwashirikisha wadau mbalimbali *(public hearing).* Baadhi ya wadau waliohusishwa ni Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo *(UCLAS),* Shirika lisilo la Kiserikali la Kituo cha Haki za Binadamu, HAKIARIDHI, Vyombo vya Habari na kadhalika. Kamati inawashukuru wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao ambayo yamezingatiwa katika mabadiliko ya Miswada hii na mengine yatazingatiwa katika utayarishaji wa Kanuni ya Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kamati imeridhika na maudhui na madhumuni ya Miswada yote mitatu. Itakumbukwa kwamba Serikali ilikamilisha na kupitisha Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi *(National Human Settlements Development Policy)* ya mwaka 2000. Tangu wakati huo hakuna sheria iliyotungwa kwa lengo la kutekeleza sera hiyo. Miswada hii mitatu ina lengo la kutekeleza sera hiyo, kwa kufuta Sheria zilizopo ambazo zimepitwa na wakati na kutunga Sheria hii mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** pamoja na kuunga mkono Miswada yote mitatu, Kamati ilitoa maoni ya mabadiliko katika baadhi ya vifungu vya Miswada yote mitatu na kuunga mkono baadhi ya maoni ya wadau na kumshauri Mheshimiwa Waziri ayazingatie. Nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba maoni ya Kamati pamoja na yale ya wadau yamezingatiwa katika mabadiliko ya Miswada yote mitatu iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri katika orodha ya shughuli za leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa ushauri na mapendekezo kwa Miswada yote mitatu kama ifuatavyo:-

(i) Serikali kupitia Wizara yake ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iendelee kuelimisha wananchi juu ya Sera zilizokwishapitishwa pamoja na sheria hizi zinazopitishwa.

(ii) Serikali imepitisha sera ya Ardhi ya mwaka1995, sera ya makazi ya mwaka 2000, lakini mpaka sasa haina sera wala sheria ya upimaji na ramani. Kamati inapendekeza itungwe sera na sheria ya upimaji na ramani ili kupunguza malalamiko ya wananchi hasa kuhusu gharama za upimaji.

(iii) Ili usimamizi na utekelezaji wa sheria hizi uweze kufanyika katika ngazi za Wilaya, Serikali iziwezeshe Halmashauri za Wilaya kwa kuzipatia rasilimali za kutosha, wataalamu, vifaa na fedha. Kamati inashauri kuwa vilevile Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iongezwe ili iweze kukidhi mahitaji yanayojitokeza.

(iv) Kamati pia imeona kwamba sekta ndogo ya nyumba haijatungiwa sheria. Kwa mfano, makazi ya watu kama nyumba yanaweza kutumika kama dhamana kwenye vyombo vya fedha ili kuweza kuwainua wananchi. Aidha, Kamati inashauri kuwa na vyombo vya fedha mahsusi kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba. Tunashauri sekta ndogo ya nyumba sasa itungiwe sheria yake.

(v) Wataalamu wazingatie sheria katika utekelezaji wa majukumu yao. Tunaiomba Wizara pamoja na TAMISEMI wasimamie sheria hizi ili wataalamu hao waweze kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

(vi) Kamati imepitia marekebisho chini ya Miswada yote, imejadili na kuyakubali mabadiliko ya Miswada hii kama Mheshimiwa Waziri alivyowasilisha katika shughuli za leo. Aidha, Kamati inashauri kuwa Wizara husika iandae Kanuni mapema pamoja na kutafsiri Sheria hizi kwa lugha ya Kiswahili chepesi kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kamati yangu inamshukuru sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa ushirikiano katika kujadili Miswada hii pia inamshukuru Mheshimiwa Ritta Mlaki, Naibu Waziri na wataalamu wao kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati hii kukamilisha kazi zake vizuri. Vilevile Kamati inawashukuru wadau wote walioshiriki katika kikao cha tarehe 16 Januari, 2007 kwa michango yao mizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuishukuru Ofisi yako kwa ushirikiano na uwezeshaji katika kushughulikia Miswada hii. Kwa kumalizia napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka na Katibu wa Kamati hii Ndugu Frank Mbumi, kwa kuhakikisha kuwa maoni ya Kamati hii yanakamilika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwatambua Wajumbe wa Kamati waliochambua Miswada hii, nao ni kama wafuatao: Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe,Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda na Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani napenda kuwasilisha maoni ya Kambi kuhusu Muswada wa Sheria ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa mwaka 2007 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Na. 43(5)(c) na 70(2), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru wadau wote ambao walipata nafasi ya kutoa michango yao ili kuuboresha Muswada huu, aidha, nawapa pongezi watendaji wote wa Wizara pamoja na Mawaziri wao kwa utendaji wao kazi kama timu moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muswada wa *Land Use Planning*, Kifungu cha 6(1) kinachohusu uundwaji wa Tume ya Taifa ya Kupanga Matumizi ya Ardhi, mapendekezo ya Muswada ni kuwa wajumbe wateuliwe kutoka asasi mbalimbali.

Kiutendaji kulingana na hali halisi ya shughuli za Tume inatakiwa wajumbe wanaotoka katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wawe ni wengi zaidi kwani takriban nyanja zote zilizotajwa kiutendaji zipo ndani ya TAMISEMI. Kutokana na wanawake kuathirika sana katika umiliki wa ardhi tunashauri kuwa ushirikishwaji wa wanawake uongezwe na si vibaya idadi iliyopendekezwa iwe nusu kwa nusu kati ya wanawake na wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu haionyeshi wajumbe wa Tume wanatakiwa wawe wajumbe wa Tume kwa kipindi cha muda gani pindi wanapoteuliwa. Hivyo ni bora ukawepo muda wao wa utendaji kazi. Aidha, Muswada huu hauelezi kama

ikitokea kuna mgongano wa maslahi miongoni wa wajumbe wa Tume na utendaji wa shughuli za Tume, nini kifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 10(2) kinachohusu sifa atakazokuwa nazo Mkurugenzi Mkuu wa Tume, ni muhimu pamoja na sifa zilizoainishwa katika Muswada kikaongezwa kipengele kingine kinachosema kuwa Mtendaji Mkuu awe na ufahamu wa masuala yanayohusu Serikali za Mitaa. Hii inatokana na ukweli kuwa kwa njia moja ama nyingine shughuli zote za Tume zinazunguka katika TAMISEMI, aidha hii itaondoa migongano ya kiutendaji ambayo ingeweza kutokea baina ya Tume na TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 33(2) kinachosema kuwa; “mamlaka ya mipango ya ardhi ya Wilaya inaweza kupendekeza mabadiliko ya matumizi ya ardhi,” na katika Kifungu cha 33(3)(4) kinachosema; “mipango ya matumizi ya ardhi na mamlaka za mipango za vijiji ndizo zitakuwa na mamlaka kamili.”

Kambi ya Upinzani inadhani kuwa hapa kifungu cha 33(2) cha Muswada huu kinaweza kutumiwa vibaya na watendaji wasiokuwa na maadili katika utendaji na kusababisha migogoro mikubwa ya ardhi. Hivyo ni bora mamlaka za ardhi za Wilaya zisipewe uwezo wa kubadilisha mapendekezo ya matumizi ya ardhi yaliyotoka katika ngazi za chini bila ya kutokuwepo na muafaka baina ya pande hizo mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa undani mamlaka ya ardhi ya Wilaya yenyewe inatakiwa kufanya *compilation* ya matumizi ya ardhi kama ambavyo mamlaka zilizo chini yake zilivyopendekeza. Kwa njia hii dhana nzima ya *decentralization* itakuwa na maana, vinginevyo sheria hii itakuwa ni kiini macho kwa Watanzania wengi kuwa wamepanga jinsi ya matumizi ya ardhi yao na baadae wanakaa watu wachache wanaojiona wanaelewa zaidi mipango ya ardhi ya vijiji bila ya kuwauliza wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona pia kuwa kwa kutumia mamlaka hizi za ardhi kuna uwezekano mkubwa wa kuwafanya Watanzania kunyimwa haki ya umiliki wa ardhi na badala yake kikundi cha wajanja wachache kinaweza kuhodhi ardhi kubwa kwa kigezo kuwa ipo katika mipango ya matumizi maalumu na kuwaacha wananchi wengi wakiwa hawana ardhi inayofaa kwa matumizi yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ninalolisema limeshatokea hata kabla sheria hii haijaanza kutumika kwani kuna maeneo makubwa wajanja wameyatenga kwa kigezo cha matumizi maalumu kulingana na *potentiality* ya eneo husika huku wananchi wengi wakipigwa marufuku kutumia ardhi hiyo kwa kupata riziki zao za kila siku. Aidha, ni muhimu upangaji wa matumizi ya ardhi uanzie kutoka katika ngazi ya chini. Tume ya kupanga matumizi ya ardhi isiwe mamlaka ya upangaji wa matumizi ya ardhi kuanzia ngazi ya Taifa, japokuwa inaweza kuishauri Serikali kuhusu sera, sheria na kanuni tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo Tume iwe na mamlaka ya uratibu na udhibiti tu. Hivyo basi, Tume inaweza kuunganisha mipango ya Halmashauri na ikawa ndio mpango wa jumla wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kuwa upangaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ni kazi inayohitaji taaluma. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ili kuwa na mipango endelevu ni vyema mamlaka za vijijji au mamlaka za mihimili za chini zenyewe zikapendekeza ni kwa jinsi gani au ni matumizi ya aina gani wanahitaji yawemo katika mpango wa matumizi na baadae wanataaluma wa mipango ya ardhi wakafanya kazi hiyo kulingana na matakwa ya hizo mamlaka husika. Ardhi tunayo lakini kitu kinachozidi kutuletea umaskini ni jinsi ya kutumia ardhi yetu na kwa maendeleo yetu, badala yake watu wanatoka nje kuja kutumia ardhi yetu kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, habari njema kuhusu Muswada wa Matumizi ya Ardhi Mjini uhusuo usajili wa bodi ya wataalamu wa mipango miji ambayo pamoja na mambo mengine watakuwa na taaluma juu ya mipango na matumizi ya ardhi. Tunaitaka Serikali itumie vizuri wanataaluma hao kwa manufaa ya Watanzania ambapo suala la matumizi ya ardhi linaweza kuleta mambo ambayo siyo jadi yetu sisi Watanzania, japokuwa mtafaruku wa matumizi ya ardhi ulishaanza kujitokeza kwa wananchi wanaoishi Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muswada wa *Town Planners,* ni vyema kuundwa kwa bodi ya usajili ya mipango miji kama ambavyo itaangalia vitendo na mwenendo mzima wa kusajili wana mipango miji ili kusaidia katika kuleta maendeleo na kufanya tafiti mbali mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na maudhui ya Muswada huu inaonyesha kuwa kama Serikali kwa ujumla wake itakuwa na nidhamu ya kuheshimu taaluma za watu wetu, ni dhahiri sasa miji yetu ambayo inapanuka kwa kasi kulingana na ongezeko la watu itakuwa katika mkondo mnyoofu kimpangilio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 7(1) kinachohusu uteuzi wa Msajili wa Bodi ya Mipango Miji, hapa kinasema kuwa Waziri atamteua afisa yeyote wa umma kuwa msajili wa maafisa mipango miji. Kambi ya Upinzani inadhani kwa kuwa hii ni bodi ya wanataaluma, hivyo ni bora hata msajili asiwe ni mtu yeyote bali awe ni miongoni mwa hao wanataaluma. Kwa msingi huo tunamtaka Waziri afanye uteuzi wa mtu ambaye atakuwa anaelewa maadili ya taaluma husika na ambaye ataweza kuyasimamia ili kuleta heshima ya taaluma husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ni bora ikaangaliwa mifano ya bodi za usajili kama vile Wahandisi, Wafamasia,Wasanifu Majengo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 12(2)(5) hakionyeshi kuwa usajili ni kwa mtu au kampuni, hivyo ni bora kikafanyiwa marekebisho ili kuonyesha huo usajili ni kwa ajili ya mtu au kampuni kwani mtu anaweza kusajiliwa kama Afisa Mipango Miji, lakini akashindwa kufanya kazi kutokana na kutotimiza masharti yanayomwezesha kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kambi ya Upinzani haina tatizo na Muswada huu, ila inataka ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri japokuwa hii ni ya maafisa mipango miji lakini *policy framework* yao ina mahusiano makubwa na *Land Use Planning*.

Kwa kuwa matatizo yetu makubwa yako katika mipango na matumizi ya ardhi na tumeambiwa katika Muswada huu kuwa huduma ya hawa watu sio bure, na kwa kuzingatia uhalisi wa Watanzania wengi waishio vijijini ikiwa ni pamoja na mamlaka za vijiji za mipango ya matumizi ya ardhi; je, ni kweli watu hawa watakuwa na faida kwa Watanzania wanaohitaji huduma yao? Zingatia hali halisi ya kipato katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kambi ya Upinzani inaona itakuwa ni bora Serikali ikatoa ruzuku kwa hawa watu katika utendaji kazi wao kwa watu ambao wanahitaji huduma yao lakini uwezo wao wa kumudu gharama zao ni mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muswada *Urban Planning*, Maudhui ya Muswada huu ni kutoa mwongozo wa kuandaa na kutekeleza sheria ya mipango miji na pia kutoa changamoto ili kuweka mazingira ya kuinua hadhi ya miji yetu kulingana na hali halisi ya maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano inazipa mamlaka za mipango haki ya kufanya manunuzi, kujipatia na kulipa fidia. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia kwa makini kipengele hiki cha kuwalipa wahusika fidia zinazohusu ardhi yao. Ni ukweli usiopingika kuwa watu wengi wamekuwa maskini baada ya kupatiwa fidia isiyoendana na hali halisi/thamani ya wakati wa soko *(market value)* na badala yake ardhi huthamanishwa kwa kutumia vigezo na sheria ambazo ni vigumu kwa wahusika kuzielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mtu ametunza shamba lake la minazi au michungwa na mwisho fidia inakuwa kila mnazi ambao ameutunza kwa miaka zaidi ya 20 fidia yake ni shilingi elfu sita wakati mnazi huo unampatia zaidi ya shilingi 50,000 kwa mwaka kwa muda wa miaka 40 na mchungwa ni hali hiyo hiyo; je, huu sio uporaji wa mchana ambao unawaweka Watanzania katika ufukara?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaitahadharisha Serikali kuwa ili sheria hizi zifanye kazi ilikusudi kusiwepo na uonevu unaoweza kusababisha kufunguliwa kwa kesi na kusimamisha shughuli zilizokusudiwa ni bora manunuzi ya ardhi yatakayofanywa na mamlaka za mipango miji yaendane na bei halisi ya soko.

Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inapendekeza pawepo na mkataba maalumu kati ya mwekezaji na mmiliki wa ardhi ili mmiliki apate malipo endelevu ya ardhi yake kwa muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetubidi kusema hili kwa kuwa Muswada huu hauko wazi kuhusiana na mauzo na manunuzi ya ardhi ya wananchi zaidi ya kutoa waraka wa manunuzi *(purchase notice).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyojifunza wakati wa semina ilioandaliwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hapo jana kwamba zipo sheria nyingi zinazohusiana na masuala ya ardhi, makazi na mazingira. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa kwa kuwa utajiri wa Watanzania upo katika raslimali kuu, nayo ni Ardhi, ni vyema sheria hizo zinazohusiana zikaunganishwa na kutafsiriwa kwa lugha rahisi ili zieleweke kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa tunao wachangiaji, idadi yao ni nzuri. Kwa hiyo, naanza na Mheshimiwa Peter Serukamba atafuatiwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Gosbert Blandes, ajiandae. Mheshimiwa Peter Serukamba!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa kwanza. Lakini nami pia niungane na wenzangu kumpongeza Mbunge aliyeshinda wa Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada hii yote mitatu ni mizuri sana imekuja kwa wakati na kwa kweli inakuja kutekeleza Sera ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia Sheria, kwanza ningeomba nianze kwa kusema ni matumaini yetu kuwa sheria hii itapita, tumekuwa na sheria nzuri sana na ambalo limekuwa tatizo, ni utekelezaji wa sheria zetu. Tuna sheria nzuri sana, linalokuja sasa ni utekelezaji. Leo hii ukitembea katika miji yote ya Tanzania, ukienda kwenye Mji wangu wa Kigoma unaweza ukaona jinsi ambavyo sheria hazifuatwi. Watu wametoa vibali tumejenga nyumba mahali ambapo hapakupaswa kujengwa, lakini hao watu wa *Planning* walikuwepo, mamlaka zilikuwepo haya yote yakitendeka. Sasa leo tunapitisha sheria hii basi niwaombe wenzetu wa Serikali watusaidie tuweze kuondoa matatizo ya ardhi ambayo yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia nzuri ya Sheria hii kuna mambo ambayo mimi nilitaka nitoe kama angalizo. Ukienda Kifungu cha 61 cha Sheria ya Mipango Miji, kinaleta dhana mpya ya mmiliki kulazimika kuweza kutoa ardhi yake kwa mamlaka za mipango pale ambapo wao wakiona kwamba wanahitaji ardhi yake, anaweza akaitoa.

Sasa maana yake nini, maana yake ni kwamba dhana hii kuna kitu kinaitwa *lack of security of tenure*. Mmiliki wa ardhi asipokuwa na ile *security* uwezekano wa kuifanyia ile ardhi kuwa na thamani au afanye nini inaanza kupungua kwa sababu anajua watu wa Serikali za Mitaa kwa muda wowote wanaweza wakaichukua ile ardhi

yao na sheria imekubali. Lakini ili waichukue lazima waithaminishe kuangalia gharama gani angeweza kulipwa. Ninachoomba katika hili watekelezaji wajitahidi sana, pale ambapo watahitaji kuchukua ardhi ya mtu basi kwa haraka sana mtu huyo apewe fidia yake. Lakini tusipokuwa waangalifu itakuwa watu wa Mipango Miji unapeleka, unataka kufanya nini kwa ardhi yako wanakataa na wanakwambia leta ardhi hii kwa sababu hujaiendeleza na hupewi fedha zako unaanza kusumbuka. Ninaomba sana hili tuwe waangalifu sana katika hii Ibara ya 61. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilikuwa najaribu kuangalia hii sheria. Sheria hii inampa Waziri na Mkurugenzi wa Mipango Miji mamlaka makubwa sana. Ukiangalia kifungu cha tano, sita na saba Waziri na Mkurugenzi wa Mipango Miji wanapewa madaraka makubwa sana katika kubatilisha au kukataa mamlaka zilizowekwa na Serikali za Mitaa. Sasa mimi ninachokiangalia hapa ukiisoma vizuri kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 145 na 146 tuliamua kwa dhati kupeleka madaraka kwenye Serikali za Mitaa, ukisoma na zile sera za maboresha. Lakini kwa sheria hii sasa ninachokiona mimi sera za maboresho za Serikali za Mitaa zinasisitiza umuhimu wa kuachia madaraka kwa wananchi. Lakini sheria hii inarudisha nguvu kwa Waziri mhusika na Mkurugenzi wa Mipango Miji.

Kwa hiyo, ninachokiona hapa sasa nguvu za Serikali za Mitaa hapa zinapokonywa. Sasa sijui ningeomba hili Waziri aniambie vizuri na kama inawezekana hili tulibadilishe. Sioni sababu kwa nini, maana yake hii itakuwa inapingana na sera ya maboresho, itakuwa inapingana na sera ya kupeleka nguvu nyingi kwenye Serikali za Mitaa, hii Ibara ya tano, sita na ya saba. Kwa sababu imefika sehemu hata vibali vya kujenga anaweza akakataa hata kama Halmashauri zimeamua *otherwise*. Sasa tunataka kupitisha sheria kuendelea kumpa nguvu. Hili mimi ningeomba tuliangalie upya ili kuona namna ambavyo mambo yataweza kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiona kutatokea malalamiko kwa kuzipa nguvu Halmashauri zikawa na uwezo wa kutoa hizo *permits.* Tumeanzisha Mahakama za Rufaa za kushughulikia mambo ya ardhi. Kwa hiyo, mimi nadhani mambo haya yote tuyaondoe kwa hawa kuwapa hizo nguvu nyingi. Lakini kama kutatokea malalamiko yataenda kwenye Mahakama za Ardhi zilizoanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lilikuwa ni kifungu namba 6(2)(a) cha Sheria ya Mipango Miji kinatoa mamlaka kuidhinisha maombi ya mmiliki wa ardhi ile kugawa, anaweza akaamua ku-*subdivide* kama ana *land* yake akafanya *sub-division* inatoa mamlaka hayo. Lakini anayestahili kuidhinisha ugawaji wa *sub-division* wa Sheria ya Upimaji Ardhi ukisoma Sura ya 324 ni Mkurugenzi wa Upimaji wa Ramani ndio wenye haya mamlaka. Lakini leo tunaanza kuona tunataka kubadilisha kupeleka kwa mtu mwingine. Hili nalo ningependa liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Kifungu namba 7(4) kwenye hii Sheria, Waziri mwenye dhamana amepewa uwezo wa kuangalia hizo *monuments, historical and Architectual designs*. Lakini jambo hili lipo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Kwa hiyo, ningeomba libaki kuendelea kuwa huko Wizara ya Habari,

Utamaduni na Michezo kwa  mtu anayeshughulika na mambo ya kale ili kuondoa mgongano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi haya ndiyo yalikuwa ya kwangu kwamba tuangalie katika hizi sheria kifungu cha 61 na hizi nguvu anazopewa Waziri mimi ninaziona ni kubwa sana na zinakinzana na ile sera ya kupeleka madaraka kwenye Serikali za Mitaa na kwa jinsi hiyo zinapingana na maboresho ambayo tunahangaika nayo ya Serikali za Mitaa.

Mwisho, nilitaka kuomba tuanzishe *register* ya watu wa Mipango Miji.  Wakati tunataka kuanzisha hiyo tayari hali ya miji yetu ni mbaya sana.  Tunagawa viwanja vipya kila siku, basi viwanja hivi tufuate taratibu za ujenzi maana unakuta umegawa huku huyu amejenga ghorofa inaangalia upande huu, huyu amejenga nyumba hii inaangalia upande huu *at the end of the day* ukiangalia huo mji haupendezi.  Lakini unajiuliza miji mingine wanafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda duniani kote ukiangalia nyumba zilivyojengwa na mipango unatamani kweli kitu hiki kingefanyika na nyumbani kwetu. Lakini angalia kule ambako tunapima sasa ningesema kule kwa zamani kulikuwa labda mambo hayafuatiliwi vizuri, lakini hata ambapo tunapima sasa ukienda leo wanavyojenga unashangaa kinachoendelea.  Hizo *building permit* hawa wanaozipitisha wajaribu kuangalia sasa tunaamua hapa kujenga nyumba za namna gani?  Zijengwe nyumba ambazo kuna *uniformity* na kwa kufanya hivyo hata miji yetu sasa itapendeza na ni rahisi sasa kupeleka hizo *social services*.  Lakini tukishaanza huyu ameangalia huku, huyu ameingia kwenye kiwanja huku nusu kidogo, haya yote yanaleta mkoroganyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi nilikuwa na hayo kulingana na hii sheria na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:**  Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi kuwa mchangiaji wa pili asubuhi hii katika Miswada mitatu ambayo imeletwa na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.  Nina michango yangu kadhaa katika kuboresha sheria hizi. *(Makofi)*

Kwanza kabisa, suala la kuwa na sheria ya kuweza kufanya *regulation* ya jinsi gani ambavyo miji yetu imepangwa na jinsi gani ambavyo tunapanga kutumia ardhi yetu ni suala zuri sana.  Kwa kweli sheria hii imejaribu kwa kiasi chake kuweza kuendana na hali ilivyo sasa hivi ingawa sioni ni jinsi gani ambavyo inaweza ikawa ni *collective mechanism* kwa ajili ya ile miji ambayo tayari imepangika vibaya.  Lakini bahati nzuri ni kwamba kuna miji mipya ambayo inatokea na iwapo sheria hii ikitekelezwa kwa dhati naamini kabisa kwamba miji na matumizi vile vile ya ardhi yanaweza yakapangwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza naona nimeanza haraka sana na mimi sikuchukua utamaduni wa kumkaribisha Mbunge mpya, Mheshimiwa Mturura Abdallah Mtutura napenda kukukaribisha katika Bunge.  Hili ndilo Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pale itakapobidi tutafanya kazi kwa ushirikiano kwa sababu

sote hapa tupo kwa ajili ya kujenga na nilikuwa Tunduru kwenye kampeni nimeona hali ya Tunduru kwa kweli kukuacha kufanya kazi ile peke yako hutaweza, ni lazima tukupe ushirikiano ili uweze kuhakikisha kwamba maisha ya Watanzania wenzetu wa Tunduru yanaweza yakaenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo ambalo nilikuwa nimelisahau, kwanza kabisa sheria hizi ambazo Mheshimiwa Waziri amezileta zimejaribu kuweka misingi ya kisera ndani ya sheria, kwa kweli hili ni jambo ambalo linapaswa kupongezwa sana. Kwa sababu mara nyingi sheria zinazokuja zinakuwa tu zinakwenda kwenye sheria moja kwa moja ile misingi ya kisera inakuwa haiwekwi. Lakini katika hizi sheria tatu ambazo tunazijadili hapa leo mwanzoni kabisa *articles* za mwanzo kabisa wameweka misingi ya kisera maana hapa ni sera ya ardhi na sera ya maendeleo ya makazi kwa kweli ni suala zuri sana.

Sasa mimi ningeanza na ile Ibara ya 6, Ibara ndogo ya (1)(b) ambapo imeorodheshwa ni watu gani wanaweza wakaingia kwenye ile *Commission.* Msemaji wa Upinzani amezungumzia jinsi gani ya kuweza kuhakikisha kwamba idadi ya wanawake na wanaume angalau katika hili iwe sawasawa, hakuna sababu ya kusema theluthi katika hili, idadi ya wanawake na wanaume na kwa sababu hiki kitu kipo chini ya mamlaka ya Waziri anaweza akahakikisha kwamba idadi ya wanawake na wanaume inakuwa sawa sawa kama jinsi ambavyo Msemaji wa Upinzani amechangia. Lakini pia hii ibara imeorodhesha hawa wajumbe watoke kwenye vyombo gani, lakini haijasema hawa wajumbe wawe na *qualification background* zipi?

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani la msingi zaidi wawe na *qualification background* zipi kwa sababu vile vyombo ambavyo mmeviorodhesha pale na idadi yenyewe ya wajumbe haviendani. Kwa sababu vile vyombo ni vingi sana, asasi zile ambazo wameziorodhesha ni nyingi sana tofauti na idadi ya wajumbe wenyewe. Kwa hiyo, ingekuwa ni vizuri ili kuweza kuondoa migogoro kwa kila chombo kingetaka kiwe na mwakilishi ni vyema ungeweza kuweka zile *qualification background* ili kuweza kujua ni watu gani ambao wanaingia katika hiyo *Commission.*

Mheshimiwa Naibu Spika, *article 18* pamoja na *schedule of amendments* ambayo Mheshimiwa Waziri ameileta imeonyesha zile *land planning authorities* na mojawapo ni *Village Council* na *District Council*. Sasa katika hili mimi nilikuwa na mawazo kwamba sheria ingetaja tu *local authority* kama jinsi ambavyo imetafsiriwa na Sheria za Serikali za Mitaa. Kwa sababu ndani ya *Local Authorities* kuna ngazi mbalimbali na moja ya ngazi ambazo ningependa niizungumzie hapa ambayo naiona sasa kwamba inaweza ikaleta matatizo ni ngazi ya *Township Authorities*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana wakati tunabadilisha Sheria za Serikali za Mitaa katika Muswada ambao tulikuwa tumepewa Waheshimiwa Wabunge ilikuwa *Township Authorities* ilikuwa zipandishwe daraja kuwa chini ya *Districts Councils* ziwe chini ya *Urban Authorities*. Sasa bahati mbaya ile *provision* ilikuwa imeondolewa katika *amendments* mbalimbali ambazo zilikuwa zimeletwa, kwa *Township Authorities* zilikuwa zimebaki ziko chini ya *Districts Councils*. Sasa *trend* inayokwenda sasa hivi hapa nchini

ni kwamba hii miji midogo inakuwa kwa kasi sana, naamini kabisa kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi mnapokuja kutoka Dar es Salaam mnapita Kibaigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kibaigwa katika hali ya sasa imekuwa *declared* kama *Township Authority* ingawa mpaka sasa bado ile mamlaka ya mji mdogo haijaanza kufanya kazi kwa sababu haujafanyika uchaguzi na wala hamna Mwenyekiti wa Mji Mdogo kama jinsi ambavyo ilivyo miji midogo sehemu nyingine mbalimbali za Tanzania. Lakini sasa unakuta Kibaigwa inakuwa zaidi ya Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya kama Kongwa. Kwa hiyo, matokeo yake unakuta kwamba jinsi gani ambavyo Kibaigwa ilivyopangwa hakuna. Kwa hiyo, unakuta Kibaigwa unakuwa ni mji ambao umepangika vibaya vibaya.

Hivyo, mimi nilikuwa nashauri, najua halitawezekana kulibadilisha sasa hivi kwa sababu huwezi hata kulileta katika *schedule of amendments* kwa sababu linahusika na Sheria ya Serikali za Mitaa. Lakini nilikuwa nakuomba uongee na Mheshimiwa Waziri wa Nchi wa Serikali za Mitaa kuangalia uwezekano wa kurejesha ile *provision* ambayo ilikuwa imefutwa katika Muswada uliokuja mwaka jana wa kuhakikisha kwamba hizi *Township Authorities* zipewe ile hadhi ya kuwa ndani ya Sheria ya Halmashauri za Miji kwa maana ya Miji, Manispaa na Majiji ili ziweze kuzi-*govern* zenyewe kutokana na jinsi ambavyo miji hii inakuwa.

Mimi katika jimbo langu la Kigoma Kaskazini nina Miji Midogo mitano ambayo imekwishatangazwa lakini bado haijaanza kufanya kazi. Mji wa Mwandiga, Kagunga, Bitale, Mahembe na Kalinzi. Mji wa Kalinzi ni mmoja wa miji ambayo inakuwa kwa haraka sana, lakini ukuaji wake unabanwa kwa sababu ya mazingira haya ya kisheria. Sasa hivi sheria hii itakapoanza kufanya kazi, Sheria ya Mipango ya Ardhi, ule Mji Mdogo wa Kalinzi hautakuwa kama sehemu ya *Urban Plan,* utakuwa sehemu ya upangaji wa ardhi ya kijiji. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba tutashindwa kuupanga ule mji ili unavyozidi kukua uweze kuwa mji mkubwa ambao umepangika na huduma zote ambazo zinatakiwa. Kwa hiyo, tutajikuta kwamba Kalinzi inaendelea kupangwa kama kijiji wakati tayari ina *characteristic* zote za mji kama jinsi ambavyo ilivyo Kibaigwa.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili suala tuweze kuliangalia kwa mapana ili kuweza kuhakikisha kwamba huko mbele hatuhitaji kuja kuanza kubadilisha sheria kwa sababu sheria hizi zinaingiliana. Nitatoa mfano mdogo kuhusiana na suala hili la sheria kuingiliana katika *Urban Planning Act* ambayo inakuwa *proposed* hapa kuna *fifths schedule*, kipengele namba mbili, baada ya *minor supplement* ile *Trading Centre* inayofuata ni *Township.* Sheria hii imetoa tafsiri ya *Township* kwa mujibu wa hii *schedule* kwamba *Township* ni nini. Sina uhakika kwa tafsiri hii, nitamwomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie hii tafsiri ndiyo tafsiri ambayo inatolewa kwenye Sheria ya Serikali za Mitaa. Lakini la pili, *schedule* hii imezungumzia *Trading Centre* na hii ni Sheria ya *Urban Plan, Trading Centre* kwa mujibu wa Sheria zetu za Serikali za Mitaa ipo kwenye *Districts Authorities* ambayo inazungumzia vijiji. Kwa hiyo, kuna

mchanganyiko kati ya miji na vijiji ambayo ni michanganyiko ambayo nilikuwa napenda muiangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawili ya mwisho, Sheria hii imeongeza *concept* mpya ambayo sio mpya kwa maana ya upya kwa sababu imeigwa kutoka nadhani Jeshi la Polisi, *concept* ya *zone* ambayo mimi nakubaliana nayo kabisa. Kwa sababu kuna baadhi ya maeneo ambayo mkoa peke yake hauwezi kupanga ardhi. Mkoa peke yake lazima ushirikiane na mkoa mwingine, ndiyo maana tunasema tujaribu kufikiria ambavyo nchi yetu inavyoongozwa, tujaribu kufikiria kwa makini sana. Kama tumekuja kukuta hata katika ngazi ya upangaji wa ardhi, jinsi gani tunatumia ardhi yetu tunaona umuhimu wa *zone* na tuna *defined zone* katika sheria zetu mpya zinazokuja na tayari mkoa wa Dar es Salaam umeshafanywa kuwa ni *zone* yenye mikoa ya Kipolisi mitatu. Kwa nini hatufikirii hoja ambayo CHADEMA wanaileta ya Majimbo, kwa nini hatufikirii hoja hii? Tujaribu kuwa *progressive* kwa sababu leo hii unatengeneza *zone* kama *Planning Authority* ya matumizi ya ardhi lakini hatuna ngazi yoyote ya Kiserikali katika ngazi ya *zone.(Makofi)*

Kwa mfano, leo ukichukulia kwamba Kigoma na Rukwa kwa mfano, au Kigoma na Kagera kwa mfano wa-*share,* baadhi ya maeneo kwa ajili ya upangaji wa ardhi kuna kikao gani ambacho kitafanya hii kazi. Kwa hiyo, lazima tujaribu kuangalia ni jinsi gani ambavyo tunaweza tukaubadilisha mfumo wa kiutawala wa nchi yetu ili uweze kuendana na hali ya sasa. Hivyo, nilikuwa naomba kwamba na kufuatana na hii changamoto ya ardhi na pia changamoto ya Polisi ambayo imeletwa, tujaribu kufikiria jinsi gani ambavyo tunaweza tukaitengeneza *structure* katika ngazi ya katikati kabla ya Taifa ambayo inaweza kutusaidia kupunguza *bureaucracy* na hata mambo kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Mbunge aliyepita aliyezungumza ya kwamba Waziri anatoa, tunaweza tukayashusha yakaenda katika ngazi ya *zone.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho *installation order article 54,* inazungumza kwamba *planning authority* inaweza ikaamua kuichukua ardhi. Mheshimiwa Peter Serukamba ameizungumza hii kwa undani sana, lakini tunaweza tukaanza kupata matatizo. Mimi juzi juzi hapa nilikuwa nafuatilia Mkutano wa *Petroleum* wa *East Africa*. Kampuni ya *Tullo Oil* ambayo imegundua mafuta kule katika pembezoni mwa Ziwa Albert, Uganda imeomba kibali cha kufanya *exploration* ya mafuta Kaskazini mwa Ziwa Tanganyika ambao takriban vijiji nane vya ndani ya Jimbo langu vinakuwa sehemu ya *exploration. Exploration* inaweza ikachelewa kuanza tukawa tumefanya vile vijiji ni *planning authority,* vikapanga ardhi yao, havijui kama mle chini kuna mafuta. Wamepanga ardhi watu wamegawiwa ardhi yao, anakuja Waziri wa Nishati na Madini, anatoa kibali *Tullo Oil* anakuja kuna mafuta Kagunga, Mwamgongo, Kiziba na kadhalika mnafanya *restoration. System* ya *compensation* ambayo imewekwa katika sheria hii haiwezi kutosheleza kulingana na thamani ya *natural resources* ambayo itakayokuwa imepatikana. *(Makofi)*

Nimeona katika *schedule of amendments* imezungumzwa masuala ya madini na masuala ya *water resources* lakini ni vipi ambavyo hizi *planning authorities* katika ngazi

za chini zitakuwa zinafahamu kwamba hapa tuna *resources* kwa sababu hawapati *information* za kuhusiana na *mapping natural resources* katika nchi nzima.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba tujaribu pia kuliangalia hili suala la *restoration order* ili wakazi wa maeneo ambayo raslimali zinapatikana waweze kufaidika na zile raslimali zinazopatikana na isiwe tu kwamba *planning authority* inaamua tu inachukua hii, inawapa watu wa mafuta na bila ya wale watu kupata *compesation* ambayo inafanyika. Hii pia tuliangalia kutokana na sheria ya madini hili suala la *article 54, Restoration order* kwa sababu kuna maeneo vijiji vinaanza kulalamika dhidi ya Makampuni ya Madini ni jinsi gani ambavyo sheria hii tumeweza kuilinda na sheria yetu ya madini nayo pia linanipa matatizo kwa sababu sijaona sehemu yoyote katika sheria hii ambayo inagusia *Mining Act* ambayo pia ni sehemu ya sheria za nchi yetu.

Mimi hayo ndiyo ambayo nimekuwa nimepanga kuyazungumza na naamini kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri kwa kusaidiana na Mheshimiwa Naibu Waziri, wataweza kutoa maelezo katika haya ambayo tumeyasema. Nitaamua kwamba naunga mkono hoja *or not* baada ya kuwa nimepata majibu hayo ambayo nimeweza kuyaelezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia. Ya kwangu kwa leo yatakuwa ni machache na nitapenda kugusia Sheria ya Mipango Miji *(Land Use Planning Act* ya mwaka 2006). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umeletwa wakati muafaka katika Bunge letu hili kwa sababu hali halisi ya miji yetu tuliyonayo kwamba tunahitaji miji yetu ikae katika mpango ambao kwa kweli unaendana na hali halisi ya miji ya wenzetu duniani. Kwa maana hiyo nimefarijika sana kuona Muswada huo unakuja hapa kwa wakati huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwenye kifungu cha 6, Ibara ndogo mbili, utakuta kwamba *section* hii imezingatia kwa makini sana kitu tunachoita *gender balance*, ni kwamba *establishment* ya *National Land Use Planning Commission* ambayo inamtaka Waziri kuteua si chini ya wanawake watatu katika ile *composition*. Mimi imenifariji sana kwamba kina mama tumewapa uwezo mkubwa sana wa kufanya maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie kipengele Namba 39 (1) ambacho kinazungumzia habari ya *Acquisition of Land Planning* na hasa Ibara ya (iv). Hii sehemu ya Muswada huu inatoa nguvu kwa *Planning Authorities* kuweza kufanya mambo fulani fulani na mojawapo katika haya ni ile namna ya kuweza kupata ardhi ambayo itafanyiwa *planning.* Matakwa ambayo yako humu yanaitaka *Planning Authority* iweze kupata idhini ya mmiliki wa ile ardhi inayotaka kuchukuliwa. Lakini inasema hivi kwamba iwapo yule mtu hakuweza kupatikana kutoa idhini haielezi vizuri ni kwamba kuna njia

ipi sasa itatumika kama yule hakuweza kupatikana. Inaishia pale na haionyeshi ni namna gani *Planning Authority* itatoa taarifa.

Kwa mfano, inaenda kwenye ardhi ya mtu ni vema ionyeshe ni lazima itangaze kwamba ardhi fulani itakuwa *subjected* katika *Land Use and Planning*. Itangaze kupitia magazeti, televisheni, redio na vile vile iweke muda wa kutosha, tangazo hilo lidumu kwa muda gani. Labda pengine miezi miwili au miezi sita ile taarifa iweze kumfikia mmiliki wa ile ardhi. Kinyume cha hapo tutakuwa tumeacha mwanya mkubwa sana wa wale watendaji kuchukulia kwamba yule mtu hakupata taarifa basi na wao wakaamua ku-*act* bila ya kumpa taarifa ya kutosha na hali hii italeteleza migogoro mikubwa sana, watu watakwenda Mahakamanim watapinga sana na itakuwa inaturudisha nyuma katika mipangilio yetu ya utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii vile vile imenifurahisha katika kipengele *Section 42(1), (2) and (3).* Pale inapozungumzia namna ya kuweza ku-*re-adjust land.* Hapa kikubwa sana ambacho imeonyesha ni jinsi gani ambavyo inajali haki ya yule mmiliki. Inasema kwamba ni lazima *consent* ipatikane, yaani lazima idhini ya yule mmiliki ipatikane kabla ya haya maamuzi. Inasema pale ambapo idhini ya mmiliki haikupatikana basi kuna utaratibu mwingine utatumika ambao upo chini ya Ibara ya 43 ya Muswada huu. Lakini la kujiuliza hapa ni kwamba kwa nini sheria isiweke utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba ile idhini au *consent* namna inavyoweza kupatikana. Utaratibu lazima uwe wazi na vile vile lazima uonyeshe kwamba ni kwa njia ipi mtu anaweza kuwa *approached* na akatoa idhini yake. Vile vile sheria lazima i-*provide* nafasi ya kuonyesha kwamba je, kama mtu amekataa hakutoa idhini ya ardhi yake kuweza kuchukuliwa na kufanyiwa *Town Planning* sasa *what next?* Kwa sababu kwenye sheria hii utakuta kwamba mtu yeyote ambaye atakuwa hajaridhika na maamuzi ya *authority* ana haki ya kwenda Mahakamani lakini kabla hatujafika huko ni hatua gani inaweza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *first schedule* ya Muswada huu ina-*provide for* Wajumbe wa Bodi ambao kwa kweli mimi imenivutia vizuri na inaeleza kwamba watakuwepo Wajumbe wa Bodi nane tofauti na ile *composition authority*. Kwenye Wajumbe wa Bodi Muswada haujatuonyesha kwamba akina mama watakuwa wangapi mle. Mimi nadhani ingekuwa ni vizuri ikaonyesha basi angalau watatu wawe Wajumbe wa ile Bodi ya watu wanane.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nimeliona katika *schedule* na hasa *section 5(6)* ni kuhusiana na maamuzi ya Bodi. Hapa ningependa Waziri mhusika anisikilize kwa makini. Kwenye maamuzi ya Bodi nitaomba kwa ridhaa yako Naibu Spika nisome kwa kiingereza. Inasema kwamba; "*The validity of any proceedings of the Board shall not be affected by any vacancy among the membership or by any defect on the appointment of the member of the board.*" Nime-*underlined by any defect on the appointment of the member of the board*. Maana yake hii ni kwamba maamuzi yote ya Bodi hayatabatilishwa na yataendelea kuwa sahihi na kutumika bila kujali kama Mjumbe wa Bodi hakuwepo katika kile kikao cha Bodi. Lakini vile vile ni kwamba yataendelea kuheshimika na kuwa na uzito bila kujali kwamba yule Mjumbe wa Bodi aliyeteuliwa

mle aliteuliwa kimakosa. Nilitaka kusema kwamba hii tukiiruhusu ni kuachia mwanya kumpa mtu ambaye hana mamlaka ya kisheria kuweza kufanya utekelezaji wa sheria hii. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba Ibara hii ifanyiwe marekebisho kwamba si sahihi mtu ambaye ameteuliwa kimakosa, hana uwezo kisheria wa kufanya maamuzi ya Bodi na yakaheshimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleze kwamba kwa ujumla Muswada huu nilivyouona, ni mzuri na kikubwa zaidi kama nilivyosema una-*promote gender balance*, lakini vile vile ni mzuri kwa uhifadhi wa mazingira yetu. La kufurahisha zaidi ni kwamba unatoa mwanya wa *any aggrieved party*, mtu ambaye hakuridhika na maamuzi ya *planning authority* kuweza kuwa na *hiarachy* ya kupanda kwenda kukata rufaa na kudai haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nisisitize kwamba Muswada huu utakapopita basi ni vyema ujikite, uende hata huko mikoani, ufanye kazi, sio ubaki tena kufanya kazi kwenye miji mikubwa tu. Nitafurahi sana nikisikia na nikiona Muswada huu unafanya kazi kwenye Mji Mdogo wa Kayanga, pale Wilayani kwangu Karagwe pamoja na Kasulu, Kibondo, Newala na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi niliyopewa kuweza kuchangia Muswada uliopo mbele yetu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwanza, niipongeze Wizara chini ya Waziri, Mheshimiwa John Magufuli na Naibu Waziri dada yetu Mheshimiwa Ritta Mlaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitazama maendeleo ya dunia na jinsi miji ya watu au miji ya wenzetu ilivyopangika tukilinganisha na sisi Tanzania tulivyo, wenzetu wanakimbia, sisi tunatambaa. Tuna ardhi nzuri, tuna hali ya hewa nzuri kuliko nchi nyingi duniani, hatuna budi sisi kama Tanzania tutumie nafasi hii kwa uwezo wote kupendezesha nchi yetu, miji yetu na hatimaye maeneo haya tuyatumie kwa fursa za kiuchumi kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii haikuchelewa, bado tuna nafasi kubwa kwa sababu miji yetu bado haijapangika vizuri, kwa hiyo, sasa tuna nafasi kubwa ya kuhakikisha kwamba tunafuata sheria ili miji iweze kupangika. Hii Sheria ya *Urban Planning Bill* ambayo inakuja katika kuandaa na kutekeleza masuala mbalimbali yanayohusu mipango miji. Hata ile miji ambayo kwamba imekwishajengwa sasa hivi hatuna budi katika maeneo mbalimbali mingine tufanye mabadiliko ya mipango ya miji yetu. Sura au kioo cha nchi yetu ni Dar es Salaam. Dar es Salaam sasa hivi inajengeka kwa kasi kubwa lakini bila ya kuwa na mipango mizuri ya kujenga Jiji la Dar es Salaam. Jana tulipata semina tukaonyeshwa maeneo mbalimbali jinsi watu walivyojenga katika maeneo mazuri tu lakini hakuna mipango ya upangaji wa mji wetu au jiji letu la Dar es Salaam. Lakini nasema tukiachia Halmashauri ya Jiji peke yake kwamba waendeleze upangaji wa Jiji la Dar es Salaam inaweza ikachukua muda mrefu bila kupata ushirikiano

na Serikali Kuu. Yapo maeneo ya jiji sasa hivi yanatakiwa *totally* yabadilishwe, aidha, kuvunjwe yale majumba na *activities* zingine zihamishwe hatimaye kuleta picha mpya ya jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano sasa hivi tunapanua barabara ya kutoka Ubungo kwenda barabara ya *Old Bagamoyo*, tunaita Sam Nujoma. Tunapanua barabara ya Kilwa, basi hizi barabara zifanane sasa na hadhi ya *infrastructure* zilizopo pembeni kwa maana ya majengo na barabara za *feeder* ambazo zitaingia kutoka barabara kubwa kuingia ndani, angalau hizi barabara kubwa zimewekwa kwa ajili ya kusaidia *traffic* lakini vile vile zitoe huduma mbalimbali nyingine ambazo ujenzi wa hoteli, kuwe na *open space*, kuwe na *parking areas* ambazo zitalingana na hadhi ya miji yenyewe ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mwingine wa majengo ambayo yamejengwa katikati ya Jiji la Dar es Salaam ambayo ni majengo ya Shirika la Reli. Shirika la Reli sasa hivi na zile nyumba za *staff* zilizojengwa katika barabara ya Nkrumah kwenda barabara ile ya mwisho kule inayopita *Central Police* ambayo barabara hii kila siku tunaizungumza lakini imenitoka lakini Mheshimiwa Waziri ananielewa naizungumzia barabara gani Nkrumah na huku nyuma utakuta pale Nkrumah kwa ndani kidogo bado kuna karakana ya Shirika la Reli. Nyuma kidogo kuna Wizara kubwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hebu watafute utaratibu wa kubadilisha ile picha au ile mandhari, majengo mengi yale ni ya Msajili wa Majumba na yapo chini ya Wizara yako. Tatizo la *compesation* hapa halikupi shida, mnazungumza Serikali kwa Serikali. Lakini sisemi kwamba Serikali ndiyo ijenge hayo majengo. Wanayojenga majengo mazuri ni watu binafsi. Tuweke mipango ambayo kwamba *investors* mkimpa, mkimuuzia, mkiweka *master plan* nzuri itavutia *investment* na hatimaye itabadilisha picha ya Jiji la Dar es Salaam, tutakuwa na barabara nzuri zaidi, pana zaidi lakini kuwe na *plan* nzuri kwa ajili ya kubadilisha Jiji la Dar es Salaam. Huo nimetoa mfano tu wa katikati ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huo huo kama inavyosema sheria sasa hivi twende huko vijijini na mikoani haina maana kwamba miji mizuri basi iwe Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na miji mikubwa kama Tanga. Lakini pia vijijini, Pangani na Wilaya nyingine kuna maeneo mazuri tu ambayo tunaweza tukabadilisha kijiji kuwa ni mji na wenzetu wanafanya na hasa katika yale maeneo niliyozungumza jana katika semina. Kwa kifupi kuna miji ambayo au vijiji unaweza ukaandaa mipango mizuri ya kupanga ikawa ni miji mizuri ya kuvutia kabisa ya utalii na kukawa na *investment* kubwa sana hatimaye ikaweza kuwasaidia wananchi walioko katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mmetupa mamlaka sisi Wilaya na vijiji kupanga mipango yetu hatimaye sasa mtusaidie vizuri na wataalamu kutoka Wizarani wakija katika maeneo tuwaeleze nini mipango yetu na hatimaye watuchoree mipango mizuri ya kuendeleza maeneo yetu katika maeneo mbalimbali. Siku zote tumezoea kupanga mashamba ya wananchi lakini hakuna shule, barabara nzuri, hospitali nzuri na sasa hii yote inarudisha maendeleo na kule ndiko kwenye wananchi wenyewe. Sasa tufike

mahali mnapopima vijiji vyetu lakini vile vile tutoe na mapendekezo vijiji vyetu tunataka viwe vipi na Wizara mtusaidie kwa wataalam ili tuweze kupanga mipango mizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumza jana katika semina kwamba maeneo ya utalii sasa hivi yamekuwa na thamani kubwa hasa ardhi. Fukwe za bahari kutoka Tanga mpaka Mtwara. Lakini nisemee eneo hili la kwangu la Pangani limekwishachukuliwa na watu mbalimbali ambao nia yao labda ni kuwekeza au pengine waje wauze kwa bei kubwa zaidi, Dar es Salaam *beach* zote hupati nafasi.

Sasa katika Wilaya ya Bagamoyo, kumekwishaanza kujaa, wamekwishahamia Wilaya ya Pangani. Lakini je, Wizara sasa inasemaje kwa sababu haya maeneo yapo katika vijiji na wale wamenunua maeneo yale kama mashamba katika vijiji na watu binafsi mashamba yao wameyauza kwa sababu yana thamani wamepewa hela ndogo lakini kwa sababu tu yapo katika fukwe za bahari wamewapa hela ndogo basi *at least* kutokana na sheria hii tuwalazimishe wale wanaokuja ku-*invest* katika yale maeneo kuwe na mipango mahsusi ambayo mnaona kwamba maeneo haya majengo yake au hoteli zake au *activity* zozote zitakazojengwa katika maeneo hayo yawe ni maeneo *very prime areas* ambayo yanavutia na hatimaye yaweze kuingiza fedha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni wajibu kabisa wetu sisi katika Halmashauri tunaweza tukatoa mwongozo kama huo tukaweka taratibu nzuri na tukapitisha sheria *(by-laws)* kuhakikisha kwamba haya maeneo kuwe na *standards* fulani ya majengo, *standards* fulani za hoteli sio anakuja mtu anasema ni *investor* halafu anakuja anatujengea vibanda vya makuti hali ya kuwa pale mahali panahitajika kuwe na majengo au hoteli nzuri ambazo zitaweza kuhudumia wananchi na wananchi wenyewe wa maeneo yale waweze kunufaika na uchumi ambao utakaoletwa katika yale maeneo. Haya ni ya msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Sheria za Ardhi Na. 4 na Na.5, zimempa mamlaka mwananchi kumiliki ardhi na unapotaka ile ardhi kwa sheria hizi sasa ni kwamba lazima alipwe fidia ambayo yeye mwenyewe atakuwa ameridhika kwa sababu kuna masuala ya mimea, kuna masuala ya miti mbalimbali ya matunda lakini, ile ardhi yenyewe sijui Serikali itaweka kiwango kwa thamani ya ardhi. Kwa mfano, iliyopo *beach* heka moja ina thamani ya kiasi gani ardhi tupu? Mwananchi hajui anazungumza na mtu anamletea begi la pesa ndani mna noti za shilingi elfu moja moja. Lakini ni pesa kidogo sana ukilinganisha na thamani ya ardhi iliyopo pale. Sasa Serikali itusaidie vile vile katika kuweka viwango vya thamani ya ardhi ambayo zipo katika *prime areas*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hilo ni la msingi, nilitaka kusema kwamba tufike mahali sasa kwamba tunapopanga miji yetu, vile vile tuchukulie sasa na huko vijijini katika maeneo ambayo yanavutia kuwa sasa ni miji mizuri, kuwe na mipango mizuri ambayo tutabadilisha sura ya nchi yetu ili iweze kupendezesha na hatimaye kuweza kuleta uchumi mzuri sana katika miji yetu. Mimi nilikuwa nataka kusisitiza hilo. Sina tatizo na hii sheria, ni sheria nzuri na sasa hivi tutakuwa na mpango mzuri sana wa kuwabana hawa *Planners,* tena hiyo kuwafunga miaka mitano mimi naona ni kidogo kwa sababu sasa hivi wameharibu kabisa mipango ya nchi yetu katika ujenzi holela. Mtu

anapata madaraka, anatoa kiwanja anakwambia wewe jenga hapa, wewe jenga hapa, wewe jenga hapa. Nani amempa mamlaka? Nani amechora hiyo mipango, hakuna! Sasa hii sheria imetusaidia ili tuweze kupanga miji yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi naunga mkono sheria hii na nakutakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri ili tuweze kutekeleza kwa pamoja na upate msaada kutoka katika Bunge hili. Ahsante sana! *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa na mimi fursa hii niweze kuchangia mawili, matatu katika sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nataka kumpongeza Ndugu yangu Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge katika Jimbo la Tunduru na kupata ushindi mkubwa kabisa na ninaamini kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba hali ya Tunduru watu wameiona na Serikali itamsaidia na sisi watu wa Mafia itatusaidia katika kuhakikisha kwamba hali zetu wote zinaboreka kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nasema nimefurahi sana kwa kuja sheria hii hasa baada ya kupata maelezo mazuri kabisa na ya kina jana katika semina ambayo Mheshimiwa Waziri alitueleza akiwa kama mtoa mada na ninaamini tumeielewa na ni vizuri zaidi kwamba leo yale marejeo ya maelezo yake katika kujibu baadhi ya hoja za Waheshiniwa Wabunge, basi angeyasema ili wananchi nao waweze kupata taarifa hii kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa katika sheria hii nilichokuwa nimekiona, ni kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na nguvu ya kumiliki ardhi yao kisheria na wawe na kauli ya kusema bila ya kufuatiliwa au mtu mwingine kuja na kuchukua madaraka katika ardhi ya mtu mwingine. Hili ndio jambo kubwa ambalo mimi nimeliona na zaidi katika kuwabana hawa Wapimaji, hawa Maafisa Mipango Miji kusema kwamba anajipimia bila ya kuchukua taratibu yoyote, bila ya kupata ushauri katika vijiji, wanavijiji wenyewe, Serikali ya kijiji na hatimaye migogoro ndipo inaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lingine nililokuwa nataka kusema nataka nitoe mfano hai wa Wilaya yangu ya Mafia na bahati nzuri jana katika maelezo ya semina ya Mheshimiwa Waziri hili suala lilitolewa mfano mzuri sana wa Kisiwa cha Mafia. Mafia imegawanyika katika Kata saba, miongoni mwa kata zile, kata mbili ndizo zimechukuliwa kama kigezo cha kupima Mji au Mji Mdogo katika hali ya kueleza kwamba yaani kila kitu kipimwe katika hali ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilichokuwa nataka kusema, nataka niulize kupitia sheria hii inasema nini juu ya watu wale wenye mashamba ya asili ambayo mfano Mafia ndio hali ya maisha yetu, ndiyo yanayotuendesha, mashamba ya minazi na mashamba ya mikorosho. Baada ya Wapimaji kwenda kupima na kuwaeleza wale wenye mashamba kwamba Bwana wee, hili eneo linachukuliwa na linataka kupimwa viwanja. Baada ya kupimwa, yule mwenye shamba huwa analipwa fidia ya mnazi mmoja shilingi 6,800/= au

7,000/=. Lakini ukiangalia hali ya mnazi ule ambao yeye ndio umemlea pengine kabla hajazaliwa yeye na baba yake, gharama yake tangu kuupanda inakaribia shilingi 80,000/=. Lakini matokeo yake Serikali au Halmashauri husika inalipa shilingi 6,000/= na yule mwenye eneo lile la shamba badala ya kupimiwa eneo moja kusema katika eneo hili tunapima kiwanja, na wewe kiwanja chako hiki, afadhali ingekuwa inampa kiwanja bure, inamwambia nunua! Sasa ukiangalia fidia ni ndogo anayolipwa, gharama ya ununuzi wa kiwanja, ardhi yenyewe haithaminiwi! Sasa hii sheria inatuambia nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atuweke wazi labda ndani ya sheria kwa kuwa haiwezi kuandika hayo, lakini kwenye kanuni zake ambazo sheria imempa kwamba ataweza kutunga kanuni ambazo zitaweza kuisaidia sheria hii kuboresha haya ambayo tunazungumza, basi utasema nini, gharama ya fidia ya mazao ya mnazi, mkorosho au mazao mengine ambayo wananchi wanalima yale mazao ya kudumu na hali ya thamani ya ardhi ikoje katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, sasa hivi fukwe ni mali na sasa hivi wananchi wengi hasa wenye kipato wanapenda kuja kununua ardhi katika maeneo ya pwani. Hali ya Visiwa vya Unguja na Pemba, ukikaa na Waheshimiwa Wabunge, utawasikia jinsi wanavyolalamika jinsi ardhi ilivyotolewa na kumilikiwa kwa kiwango kikubwa kabisa na wawekezaji hasa hawa wenye hoteli. Lakini, athari zao sasa zinaanza kujionyesha hata wao wenyewe hawapati wasaa wa kwenda kupumzika katika baadhi ya maeneo ya jirani ya vijiji vyao mpaka inabidi wakati mwingine wasafiri waende mbali kwenda kupumzika na familia zao. Sasa hali hii isije ikatutokea katika maeneo ambayo yananza kuvamiwa na hawa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri ajitahidi katika kuwaelekeza hasa hii *commission* ambayo anaiunda japokuwa katika hao wajumbe mimi nafikiria angekuwepo basi japo mjumbe mmoja kama mwakilishi wa wananchi kwa maana ya Mheshimiwa Mbunge atoke ili awe mjumbe au katika zile nafasi tatu ambazo yeye atateua, basi tafadhali namwomba Mheshimiwa Waziri, hao Waheshimiwa Wabunge wawepo ili waweze kutoa ushauri kwa wananchi kwa sababu wao ndio wapo karibu na zile athari zinazowapata wananchi, basi wao ndio waweze kuwa watetezi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi migogoro imezuka sehemu nyingi sana, lakini Mafia kuna migogoro tena mikubwa na jana nilimwomba sana Mheshimiwa Waziri ajitahidi yeye na ikiwezekana hata awachukue na baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Ardhi na Kilimo waweze kuja Mafia kukaa na wananchi wawasikilize, wakae na wataalamu wawasikilize maoni yao ili waweze kuondokana na migogoro hii. Kuna migogoro katika maeneo ya Kata ya Kegeani, kijiji cha Utende. Kuna mgogoro ambao Mheshimiwa *DC* amejaribu kuutuliza katika Kisiwa cha Chole na kuna baadhi ya migogoro ambayo sasa inaanza kuibuka katika upimaji wa Mji Mdogo wa Kilindoni. Mle ndani yake kuna mashamba, sasa haya hata katika mambo yetu ya kisiasa huwa tunavurugana kwa kupitia matatizo haya madogo madogo ambayo yanajitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa nafikiria kwamba naomba sana sheria itamke wazi, kanuni zitamke wazi kabisa kwamba thamani ya ardhi ikoje na thamani ya zao, thamani ya mti, mazao yale ambayo yapo sasa hivi, naomba Mheshimiwa Waziri atutamkie ili waelewe sasa hivi wale watu ambao wanachukuliwa mashamba yao kwa kupimwa viwanja itamkwe ni kiasi gani, mnazi kiasi gani, mkorosho kiasi gani ili tuweze kufahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu, Mheshimiwa Waziri hivi maeneo ya Mipango Miji ambayo tunaizungumza tujiulize kwa nini watu wanavamia zaidi Mjini, kuna nini na matokeo yake ndio wanakwenda kupima. Ninaomba sana kama Wizara ihakikishe inaboresha zaidi vijijini hali ya vipato vya wananchi, mimi nafikiria watu wengi watakuwa hawavamii. Lakini leo ukiangalia katika matatizo haya utakuta migogoro hii ipo katika Kanda hizi za Pwani hasa sehemu za bahari na baadhi ya maeneo ambayo yapo mashamba ya asili katika Mikoa hii yetu ya Pwani kwa maana ya Tanga, Lindi, Mtwara. *(Makofi)*

Lakini, ukiangalia mimi juzi nimetembelea maeneo ya Mombasa watu kule wanalia, fukwe zote zimechukuliwa, mtu hakuna sehemu za kwenda kupumzika mpaka Rais alitoa eneo linaitwa eneo la Mheshimiwa Kenyatta yaani hilo marufuku pale Mombasa kujenga jambo lolote na hata hivyo kuna tajiri mmoja ambaye tayari alikuwa kaanza kupaletea maelezo ya kwamba amepanunua kwa matapeli. Lakini sasa kwa kuwa hilo siyo la kwetu halituhusu kulizungumzia hapa isipokuwa nasema na sisi lazima tujihadhari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hii Mipango Miji ambayo inapangwa ukiangalia katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, mbona wenzetu wamepanga mipango yao vizuri sana. Pale wenzetu wamefaidika nini, wamefanya nini na sisi huku tunashindwa! Lakini pia utakuta kuna mashamba ambayo yapo mle mle jirani kabisa ya mji. Mbona yale mashamba hayagawiwi wakapewa watu viwanja mpaka wanaachiwa wanatoka huku wanakuja huku sehemu za Dar es Salaam na sehemu zingine kuja kununua halafu watu wa Arusha na Moshi wanahangaika kwamba sisi hatuna maeneo ya kukaa, maeneo yote yameuzwa. Lakini utakuta yale maeneo hayapimwi na kuna mashamba ya mibuni ipo mpaka pale karibu kabisa na mji ule wa Arusha utayaona, lakini hayapimwi wakapewa watu viwanja. Huku kwetu kwa kuwa ni mnazi, basi utaambiwa huku pima tu, gawa gawa! Wanakuja watu kutoka kila maeneo wanakuja kupewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu hili nataka Mheshimiwa Waziri atuambie kule Arusha na Moshi kuna nini? Kwa nini mashamba hayo hawagawiwi wakapewa wananchi? Sisi wenye mashamba ya minazi na mikorosho inapimwa ovyo na matokeo yake wale wale wenye mashamba wanapewa pesa duni ambayo badala ya kumsaidia, ndio inazidi kumdidimiza na kumfanya awe maskini maradufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili nataka Mheshimiwa Waziri atueleze kwa nini wenzetu hawapimiwi mashamba yao, sisi huku watu wananyang’anywa mashamba na kuweza kupimiwa ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu hii *TIC*, wakati wa kutoa maeneo, naomba wasije wakafikia kwetu sisi viongozi wa Wilaya peke yake, ipate ushauri kutoka kijijini. Wale wenye ardhi ambayo wanataka kuitumia, wapate maelezo yao, wakubaliane na Serikali ya kijiji, halafu ndio *process* za kumpa mwekezaji katika eneo lile zianze baada ya kujua yule mwekezaji aweze kulipwa hiyo hiyo fidia na kwa nini alipwe! Kwa nini ninyi kama Serikali msimshawishi yule mwanachi akaingia ubia awe na *share* kwa yule mwekezaji mpaka auze? Kwa nini mnalazimisha wauze mashamba yao wale watu? Kwa hiyo, tunaomba sheria hii iangalie badala ya kumwambia mwananchi auze, basi imshawishi na impe maelekezo imsomeshe ili awe mbia wa ile kampuni itakayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu Namibia wameendelea, mwekezaji yeyote katika Namibia anapotaka kujenga hoteli, kwanza, Serikali ya kijiji inakwambia, jenga eneo hili hapa, lakini asilimia 10 ya mapato yako kabla ya kodi lazima yaende kijijini. Mambo ya *VAT*, sijui nini, utajijua wewe mwenyewe na vijiji vya kwao vimeendelea na watu wanafaidika na vijiji vipo katika hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini na sisi tusitumie mfumo? Kama sera haikubali, basi sera iletwe hapa na wataalamu tuweze kukaa na kuipitia ibadilishwe. Lakini wenzetu wanaendelea kwa utalii. Sisi Pwani utalii ndio umekuja kuwa sumu na fitina. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hii mipango miji ambayo inaletwa kwa Wilaya ya Mafia, mwanzo ilikuwa ni fitina kubwa sana. Kama *pilot project* mliifanyia Mafia, basi imeleta madhara makubwa sana. Lakini, madhali leo tunaipitisha hii sheria na *Inshalah* ninaamini itapita bila kipingamizi chochote kwamba sasa hivi Mheshimiwa Waziri ataweza kutusaidia ili ile migogoro iweze kupungua, wawekezaji wakae kwa amani na sisi viongozi tukae kwa amani na wananchi nao wafaidike na matunda ya ardhi yao ambayo Mwenyezi Mungu kawatwalia pale kama Watanzania.

Mheshimiwa Naibu spika, sina zaidi, naomba niunge mkono hoja hii mia kwa mia na nawaomba wenzangu pia waipitishe bila kipingamizi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Muswada huu ambao ni muhimu sana kwenye masuala ya maendeleo ya ardhi. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza Ndugu yangu Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Tunduru, karibu sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajikita zaidi kwenye Muswada wa kwanza kati ya hii Miswada mitatu ambao umelenga zaidi kwenye mipango na matumizi ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa Naibu Waziri na pia kwa wataalamu na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri sana waliyoifanya. Nina uhakika kazi ilikuwa ni ngumu, lakini hiki ambacho wametuletea hapa hivi leo kwa kweli kinaridhisha kwa kiwango kikubwa sana. Nasema

ninawapongeza! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyoiangalia ina mabadiliko mengi sana, mabadiliko ambayo yatakuwa na manufaa katika upangaji wa matumizi ya ardhi katika nchi yetu. Matumizi ya ardhi katika maeneo yote kinyume na hivi sasa ambapo zaidi tulikuwa tunajikita kwenye maeneo ya Miji. Sasa hivi kutokana na sheria hii, kazi ya kupanga itaanzia huko huko vijijini na itakuja hadi mijini. Sasa hili ni zuri, wenzangu waliopita walishagusia matatizo ya Miji Midogo ambayo inaibuka na mpaka wakati inafikia kuwa miji ambayo sasa lazima ipangike, mambo yanakuwa yameshaharibika. Unakuta watu wameshatumia pesa nyingi sana, rasilimali nyingi sana za nchi hii kujenga majengo ambayo ni ya kudumu, lakini yapo katika mpangilio ambao si sahihi. Kwa hiyo, tunasema hii sheria inakuja wakati muafaka na tunaiunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho kimenifurahisha katika sheria hii au Muswada huu ni kwamba ni sheria ambayo ni shirikishi, kama tutaifuata hii sheria ilivyowekwa, kwa kweli tutawashirikisha wananchi wetu katika mipango ya matumizi na maendelezo ya ardhi yao, hii ni kutoka katika ngazi ya kijiji, miji midogo, miji yetu na hadi kwenye Majiji. Kwa hiyo, nasema hiki ni kitu kizuri na kwa upande mwingine, sheria iliyopo hivi sasa imejitahidi kwa kiasi kikubwa kushirikisha watu katika upangaji wa miji ingawaje upangaji wenyewe haukuwa wa ufanisi sana. Manispaa zetu, Majiji yetu yana Mabaraza ya Madiwani ambao wamekuwa wakishiriki katika kuhakikisha kwamba ardhi ambayo ipo chini ya maeneo yao inasimamiwa kufuatana na sheria iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, kufuatana na sheria iliyopo hivi sasa manispaa zina mamlaka juu ya ardhi ambazo zipo chini ya maeneo yao nasema Manispaa na Majiji. Lakini kwa bahati mbaya sana hapa kwetu Dodoma, Manispaa ya Dodoma haina mamlaka yoyote juu ya ardhi ambayo ipo Dodoma. Hili ni jambo la kihistoria na wakati uamuzi huo ulipofanyika, nia ilikuwa ni njema kabisa. Nia ilikuwa ni kuleta maendeleo ya haraka katika ujenzi wa Makao Makuu Dodoma, hiyo ilikuwa takriban miaka 30 iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana ujenzi wa Makao Makuu kwa kiasi kikubwa sana umebakia kuwa kama ndoto tu, mambo yamebakia kwenye makaratasi. Lakini madhara yake ambayo tunaweza tukasema kwamba wananchi wa Dodoma kwa kunyang’anywa ile haki ya kufanya mipango yao wenyewe kama wenzao Manispaa nyingine, ni kama vile walijitoa mhanga ili wapate chochote katika ujenzi wa Makao Makuu. Lakini miaka yote hiyo imepita hakuna ambalo limefanyika na pia haki zao zimeendelea kushikiliwa na chombo kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *CDA* ilipoundwa, lengo ilikuwa ni hilo kwamba isaidie kuharakisha ujenzi wa Makao Makuu. Lakini kwa bahati mbaya kama nilivyosema hilo halijafanyika na ile haki ya mwananchi wa Dodoma Mjini ya kujiamulia mambo yake yeye mwenyewe sasa hivi inakuwa *excercised* na *CDA* na *CDA* kama mnavyojua ni chombo cha Serikali na maamuzi yake mara nyingine anaweza kuwa ni mtu mmoja akaamua na ikapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya *CDA* kuhodhi mamlaka hayo kama nikiyazungumzia kwa kifupi tu ni kwamba kama nilivyosema wananchi wa Manispaa ya Dodoma na wananchi kinyume na wananchi wengine wote katika miji mingine ya Tanzania, kimsingi wamenyimwa haki yao na kwa hakika ni haki ya Kikatiba ya kujipangia mambo yao wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka yote hiyo, Manispaa ya Dodoma imekosa mamlaka ya kujiamulia mambo yake yenyewe. Sasa madhara yake mara nyingine ni makubwa.

Nikitoa mfano wa hivi karibuni, mwaka jana wakati tunahangaika katika kuharakisha ujenzi wa shule za sekondari, kuna Kata moja ya Kilimani yenyewe ni Kata ambayo wakazi wake wana uwezo na ni watu ambao kuchangia ujenzi wa shule ya sekondari isingekuwa tatizo kwao. Lakini hadi hivi leo hawajaanza kujenga shule ya sekondari kwa sababu juhudi zao zote za kuomba kiwanja ambacho ni muafaka kwao ziligonga mwamba na juhudi zote za sisi viongozi kupitia Manispaa pia ziligonga mwamba kwa sababu tu uwezo wa kuamua kwamba hiki ni kipaumbele cha Manispaa haukuwa chini ya Manispaa yenyewe, ulikuwa chini ya *CDA*. Kwa hiyo, hii ni hali ambayo kwa kweli siyo nzuri na kilio cha wananchi wa Manispaa ya Dodoma ni kwamba warudishiwe haki zao kama vile Manispaa zingine za hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya *CDA* tungeomba, siyo kwamba iwe ni mwisho, hapana. Sisi tunaamini kabisa kwamba *CDA* ina nafasi yake katika kuleta maendeleo hapa Dodoma. Lakini utaratibu ambao ni mzuri, utaratibu ambao hautamnyang’anya mwananchi wa Dodoma haki yake ya kimsingi utafutwe na nina uhakika unaweza ukapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, mimi ningemwomba Waziri auangalie ule Muswada upya tena hasa katika Kifungu cha 18(1)(b). Mimi naamini kwamba kifungu hicho ndicho kilichotumika hapo mwanzoni kuinyang’anya Manispaa ya Dodoma uwezo wa kuamua mambo yake yenyewe. Kifungu hicho kinamruhusu au kinampa uwezo Waziri kuunda Mamlaka yoyote ile nyingine baada ya zile ambazo zimetajwa katika Muswada. Sasa sisemi kwamba kifutwe, hapana, ni kwamba kifungu hicho kirekebishwe ili pale ambapo inabidi kitumike, kisiingilie haki za msingi za wananchi hasa wale ambao wako katika Manispaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuunga mkono hoja kwa matumaini. Ahsante! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani Mheshimiwa Spika, alipokuwa anaondoka alisema kwamba tunayo shughuli ya ufunguzi *Paying Centre* ya Benki ya *NMB*. Kwa hiyo, ningependa Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, nimnyime dakika hata kama tano. Kwa hiyo, atakuwa msemaji wa kwanza mchana, atafuatiwa na Mheshimiwa Clemence Lyamba na Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi

ndio watakuwa wasemaji wa mwanzo na kuna wengine watakaofuata. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.59 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Muswada huu. Lakini kwanza, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura na Mheshimiwa Florence Kyendesya, kwa kujiunga na Bunge hili. *(Makofi)*

Vile vile naomba nimpongeze Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwanza, kwa kuendesha semina iliyokuwa na mafanikio mazuri sana jana. Vile vile kwa kuwasilisha kwa umahiri kweli kweli Miswada mitatu kuhusu Mipango Miji na Mipango Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutolea maoni Miswada hii mitatu, naomba kwa ruhusa yako na kwa niaba ya wananchi waishio Wilaya ya Kyela, kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri John Magufuli na Naibu wake, Mheshimiwa Ritta Mlaki kwa kuitikia kilio chetu cha muda mrefu wana Kyela cha kutaka angalau vijiji vyetu vyote 101 vipimwe. Tulipomlilia tu katika miezi mitatu/mine, kwa kweli kwa kasi na viwango, vijiji vyote 101 vimeweza kupimwa, namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada hii mitatu iliyopo mbele yetu ni muhimu sana. Nakubaliana na wenzangu kwamba haina budi tuipitishe. Lakini utekelezaji wake unaweza ukawa na madhara makubwa sana ikiwa hatutazingatia masuala ambayo wenzangu toka asubuhi wameweza kuyaongelea. Mimi nilitaka kuyasisitiza mawili tu ili yaweze kueleweka zaidi. *(Makofi)*

Kwanza, Sheria ya Mipango Ardhi *(Land Use Planning Bill)* inatoa mamlaka kwa *planning authorities* katika ngazi ya vijiji na ngazi ya Wilaya kutangaza eneo lolote kuwa ni *planning area* na vile vile kulitwaa eneo hilo chini ya Ibara ya 39 halafu na kwa kuzingatia masharti ya sheria zingine kama *Land Acquisition Act* ya mwaka 1997 na *Land Act* ya mwaka 1999. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuzitaja sheria hizi zingine *Land Acquisition Act* na *Land Act* kama inavyotaja ibara ya 39, Muswada huu kwa kweli ulitakiwa uwe wazi sana katika suala la fidia na suala la haki za wananchi ambao ardhi yao inachukuliwa, mashamba yao yanachukuliwa. Hili limeongelewa sana na wenzangu toka asubuhi. Lakini pengine nitolee mfano lieleweke zaidi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa kweli akisikie hiki kilio cha wananchi. Nitoe mfano wa mradi wa viwanja 20,000 vya Bunju. Mimi najua wenzangu wengi ambao walikwenda huko wakanunua mashamba kwa shilingi 500,000/=, 700,000/= na 1,000,000/= na eneo la

Bunju likawa *declared planning area,* likachukuliwa. Serikali bila kuzingatia wamenunua kiasi gani, wakalipwa fidia ndogo kwa sababu hakuna walichoweka pale, ilikuwa ni ardhi. Serikali imewalipa shilingi 50,000/=, wengine shilingi 70,000/= na 100,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, tena laki moja ni hela nyingi sana, halafu baada ya muda mfupi tu baadaye wakati Serikali haijaweka chochote pale imepima tu wananchi wakapewa *first priority* waliochukuliwa mashamba kwamba sasa wanunue viwanja kwa shilingi milioni 1.2 katika wiki tatu. Sasa huyu mtu muda wote alikuwa hajajenga, haja-*develop* hiyo sehemu, utampaje wiki mbili tu. Wewe umewekeza nini *as government* kuweza kuruka kutoka shilingi 50,000/= iliyomfidia mpaka milioni 1.2 baada ya muda si mrefu na pale hakuna kitu vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vinavyotumika leo kama fidia ya mimea kwa kweli kuna umuhimu kabisa wa kuvipitia upya. Nilikuwa naongea na baadhi ya wenzangu kutoka Mikoa wanayolima ndizi. Kiwango kinachotumika kufidia mti mmoja wa ndizi ni kile kile cha mwaka, nafikiri arobaini na kitu. Mimi nadhani kuna umuhimu sasa hivi tuwe *realistic*. Ama tunachangia katika kuwadidimiza wananchi wetu sisi wenyewe. Sheria za *Compulsory Land Acquisition* nchini na vile vile maamuzi ya Mahakama zetu yamekuwa yanasisitiza kwamba mtu anayeondolewa kwenye sehemu yake, lazima vitu viwili vitokee. La kwanza alipwe fidia ya mwendelezo wowote ambao umefanyika juu ya ardhi hiyo, wanaita kitaalamu *compensation for unexhausted improvements. (Makofi)*

Lakini ya pili, lazima atafutiwe sehemu mbadala, lakini Serikali haizingatii yenyewe hilo. Mtu anapewa shilingi 50,000/= inaangalia upande wa pili. Kwa hiyo, hatuzingatii sheria. Hivyo, nilikuwa naomba katika hii *Bill* hebu tuwaonee huruma Watanzania hawa, wasije wakawa *squatters* kwenye nchi yao wenyewe. Tuweke wazi haki za mtu ambaye ardhi yake imechukuliwa hata kama *land acquisition* imegusia, lakini hii sheria itaje wazi. *(Makofi)*

Vile vile suala la tatu, nilikuwa nasisitiza kuwa mkataba ambao mtu aliingia katika kununua shamba, lazima uzingatiwe. Mtu hawezi kuwa amenunua shamba kwa shilingi milioni mbili unakuja wewe, lakini *as a government* na una pesa, unatoa fidia shilingi 70,000/=, 120,000/= lakini baada ya muda mfupi linauzwa hilo eneo kwa hela nyingi sana. *(Makofi)*

Suala la nne, utekelezaji wa sheria hizi mimi naomba uende sambamba na hatua zingine za makusudi za kuwainua wananchi kuwasaidia. La sivyo miji yote Tanzania itakuja sasa kutawaliwa na wageni; wazungu, wahindi, sijui watu gani. Kwa sababu miji yetu imejaa makovu ya historia ya Kikoloni. Kila mji kuna eneo la Uzunguni, kuna eneo la Uhindini, kuna eneo la Uswahilini na eneo la Uzunguni ni Uzunguni kweli unaona wazi kuwa kuna *investment* ilifanyika pale, eneo la Uhindini vile vile. Lakini eneo la Uswahilini ndiyo lile ambalo hata kwenye mlango wako kuna mfereji wa maji machafu unapita, hakuna *investment* imetokea pale. *(Makofi)*

Lakini siyo kwamba sisi Waswahili tulitaka hiyo hali, ukoloni ulituweka sisi tufikie hapo. Mkoloni alipitisha sheria mwaka, sikumbuki vizuri, mwaka 1932. Ilikuwa inaitwa *Credit to Natives Prohibition Ordinance,* (Sheria ya Kuzuia Mswahili asipewe mikopo), lakini wengine wote wana-*enjoy* mikopo. Kwa hiyo, tumefika mpaka mwaka 1960 miji yote ina-*reflect* hali hiyo kwamba Waswahili hawana uwezeshaji wowote. Wao ni kukaa kwenye *squatters* za miji. Ndipo ikatokea hali hiyo. Hapa ni kwa Wazungu, huku Uzunguni, huku Uhindini kule kwa Waswahili. Tumepata Uhuru, bado mabenki yetu kichwani mwao yana hiyo sheria ya *Credit to Natives Prohibition Ordinance.* Imo kichwani. Kwa sababu sasa hivi, Mswahili hata kufungua *bank account* ni kama unataka kuomba kazi. Sasa kukopa je? Kwa hiyo, tuna hali ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasema leo hii tusipokuwa waangalifu baada ya kupitisha hii sheria kuhakikisha kwamba tunabadilisha mazingira ya huyu Mswahili ili vile vile naye aweze akawa sehemu ya mwendelezo wa miji yetu na vijiji vyetu, tutajikuta sisi Waswahili tunasogezwa nje ya miji tunawaachia wageni pale, kwa sababu gani. Hizi sheria zimekuja na viwango, hivyo viwango tutaviweza sisi Waswahili wakati bei ya *cement* inapanda kila siku, bei ya mabati inapanda kila siku? Utajenga nyumba wapi? Kwa hiyo, itabidi Waswahili kazi yao iwe kusukumwa pembeni mwa Miji kama Gongolamboto kule. Unawaacha wenye fedha, wageni wanakuja kukaa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu katika kuipitisha hii sheria tuelewe kabisa tuna mtihani mkubwa mbele yetu. Mimi nashukuru sana kwamba ukifungua hii sheria mwanzoni kabisa, inatoa busara kwa Waziri mwenyewe kwamba haita-*come into operation* mpaka tarehe ambayo Waziri ata-*appoint by notice published in the Gazette*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningemwomba Mheshimiwa Waziri John Magufuli, ambaye naelewa ni mtu wa watu, ni mtu ambaye sikio lake lipo kwa watu wa kawaida sana. Hebu tuangalie utekelezaji huu usije ukatufikisha Waswahili tukawa *squatters* kwenye nchi yetu sisi wenyewe. Kwa sababu sheria itaweka viwango ambavyo Mswahili hawezi kuvitekeleza, vinaweza vikatekelezwa na wazungu wanaokuja kwenye uwekezaji na wageni. Kwa hiyo, Miji yetu yote katika sehemu zote nzuri itakuwa imetawaliwa na wageni. Sisi Waswahili tutazidi kusogezwa pembeni ambako unafungua mlango, mfereji wa maji machafu unapita mbele yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kuuliza Waheshimiwa Wabunge, ambao wameshatembelea India. Ukifika *Bombay* ambako wana sheria yao nzuri kama hii tunayopitisha leo; unapotua tu upande wa kulia wa Uwanja wa Ndege ni vibanda vya makaratasi na *plastic* tupu. Ni Mji mkubwa kabisa wa *plastic.* Huku umepangwa Mji mzuri kweli kweli ambapo wanakaa watu wenye nacho. Hawa wenye India wenyewe, wako upande wa kulia, ni maboksi matupu na ni mji mkubwa kweli kweli nao. Tusije tukafikia huko tukapitisha hii sheria ikawa kitanzi chetu na sisi cha kutupeleka huko huko kwenye maboksi bila kuangalia bei zinazopanda kwa nguvu sana za *cement,* za mabati. Na sisi Waswahili tuweze kujenga hizo nyumba, tukashiriki katika utekelezaji wa hii sheria vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo na ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri hili alizingatie na naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa natoa shukrani kwa kunipa nafasi hii ya pili kuwa mchangiaji wa Miswada hii jioni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo machache kuhusiana na Miswada mitatu iliyowasilishwa kwa mpigo kwa makini sana na Mheshimiwa John Magufuli, nampa pongezi kwa umahiri wake. Naomba niungane na Wabunge wenzangu waliotangulia kuchangia mada katika Miswada hii kwa kumpongeza ndugu yetu Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kwa kushinda na kunyakua kiti cha Ubunge Jimbo la Tunduru. Hongera sana Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kukiri kwamba sina tatizo lolote kubwa sana dhidi ya Miswada iliyowasilishwa. Lakini naona kuna mambo machache ambayo nafikiri ni ya msingi kuyatamka. Wote tunajua thamani ya ardhi inavyoongezeka na jinsi inavyojulikana duniani kote na Watanzania si tofauti. Tatizo letu nafikiri linajitokeza katika masuala ya utekelezaji kwa watendaji wetu. Tuna mipango mingi, tuna Miswada mingi, tuna sheria nyingi, lakini mara kwa mara udhaifu wa usimamizi au upotoshaji wa utekelezaji unaotakiwa ndiyo mara kwa mara unatuletea matatizo.

Kauli hii nina maana ya kusema, pamoja na kwamba maana yake ni kuboresha sheria zilizotungwa awali katika matumizi bora ya ardhi, lakini ipo mifano ambayo inaonyesha kidogo kupwaya kwa watendaji kuchelewesha maamuzi. Mfano mdogo nilionao ni mji mdogo wa Mikumi kwa hivi sasa, lakini kwa miaka mitano/sita/saba na iliyopita kilikuwa ni kijiji. Mwaka uliopita mwishoni sisi Madiwani wa Wilaya ya Kilosa, tulipata *bill* ya Serikali ambayo ilitungwa mwaka 2004 lakini sisi tukaipokea mwaka 2006 ikiteua Kijiji cha Mikumi kuwa ni Mji mdogo, miaka minne tangu kutungiwa sheria na mpaka tunavyozungumza sasa hivi utekelezaji kuufanya Mikumi kuwa Mji Mdogo bado. Maelezo kuhusu ucheleweshaji huu ni nini? Hii ndiyo inayoleta hisia kwamba huko mbele pamoja na sheria nzuri lakini bado kama utekelezaji hausimamiwi vizuri inavyotakiwa; bado tunakwenda kwa *speed* ambayo ni ya pole pole sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, langu kubwa katika matamshi haya ni kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba Miswada mipya hii iambatane na yeye kuwadai uwabijikaji wa uhakika wa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya katika utendaji ili yote yaliyomo katika Muswada yasimamiwe na kutekelezwa vizuri. Tusione *que* (msururu)tena zinaendelea kule Makao Makuu ya Ardhi katika ofisi mbalimbali huku tukiongozwa na miongozo mipya. Si Makao Makuu tu lakini katika Mikoa mbalimbali ambako wananchi wengi wanatumia muda mwingi siku hadi siku na pengine hata miezi kufuatilia mambo mengine ambayo si ya lazima sana kuchukua muda lakini yanacheleweshwa na kuwanyanyasa wananchi. Kwa hiyo, tunategemea ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya na utekelezaji kwa *speed* mpya siyo ya zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee mimi nina furaha sana Miswada hii imewasilishwa kipindi hiki kwa kuwa kule Mikumi, hivi sasa tulivyo humu Bungeni

kuanzia tarehe 7 Februari, 2007 wapimaji kutoka ardhi wanaendelea na zoezi la kuainisha mipaka baina ya Mji Mdogo wa Mikumi, Lumango, Ruhembe, Kitete Msindazi, siyo Msindai, kielezo na kidogo basi na Hifadhi ya Mikumi. Ni jambo la busara na muhimu na wananchi wote wamelifurahia. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kupanga utaratibu wa kuwawakilisha au kuwashirikisha wananchi katika zoezi hilo. Lakini kwa bahati mbaya sana nasikitika sana kueleza kwamba baadhi ya Vijiji vimeligomea zoezi hili hususan Kijiji cha Mikumi na pia sehemu ya Kijiji cha Lumango. Tatizo, kuna maelezo na maelekezo bayana kwenye *Government Notice* namba 121 ya tarehe 13 Juni, 1975 ambayo inaeleza kinaga ubaga mipaka ya vijiji hivi na Hifadhi ya Mikumi inaanzia wapi. Inaeleza bayana nafikiri mstari wa tatu katika *Government Notice* ile kwamba mpaka *point* ya kuanzia ni pale ambapo lipo jiwe la barabarani, limeandikwa k.m 115 kutoka Morogoro kuelekea Iringa. Lakini wapimaji wamekataa kuanzia pale na wakaamua kuanzia sehemu tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuanzia sehemu tofauti na walivyoendelea ikaonyesha mipaka inaingia katika maeneo ya Mji Mdogo wa Mikumi, unaingia kumaanisha kuna nyumba za watu ambazo zipo katika hifadhi na mashamba ya wananchi katika ukanda ule unaoelekea Lumango mpaka Ruhembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali za Kijiji zikaona haitakuwa vema wao wawe sehemu ya kushiriki kuambatana na upimaji ule katika mazingira ambayo yanakiuka na yanakataa kufuata elekezo la *Government Notice* niliyoitamka hapo awali. Haya ndiyo ninayozungumza matatizo ya watendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hii hatujui kitatokea nini lakini ninachoomba kwa nia nzuri kabisa ni kwamba, kwa sababu zoezi hili linaendelea sasa hivi, ingekuwa busara sana kama tungewaalika au Mheshimiwa Waziri, angefanya utaratibu wa kutumia ofisi yake kuomba kuwaalika viongozi wa Serikali wa vijiji husika na hawatakuwa wengi. Kwa ujumla ukiunganisha na watu wa Maliasili pamoja na Wizara yenyewe pengine watakuwa 25 hivi. Ili zoezi hili na muafaka ufikiwe haraka, tukutane Mikumi haraka iwezekanavyo wakati viongozi waliopo kule wanakopima wapo na hatimaye tuzungumze na kuwekana sawa ili tatizo hili liwe limemalizika *once and for all*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu jimbo la Mikumi lilipoanzishwa mwaka 1995 tatizo hili limekuwa likiendelea bila ufumbuzi. Nitaona fahari na furaha kubwa endapo fursa hii itatokea na kama jinsi sisi Wabunge tulivyopewa semina jana, naamini kuwa wadau hao wakipewa semina elekezi ya watu hawa wachache tutafikia mahali na kwenda wote pamoja kulimaliza tatizo la mipaka *once and for all*. Namwomba sana Waziri alikubali hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile sasa hivi zoezi la kupima vijiji ndiyo limeshika hatamu na kwa kuwa angalau kwa upande wangu, lakini naamini na Wabunge wengine pia, sijapata kuona ramani maalumu ambayo inaonyesha majimbo yote yalivyo nchini. Kwa kuwa mara kwa mara unapotetea na kujenga hoja za kuwatetea wananchi

waliopo majimboni, tunapojenga hoja za kuomba miradi mahali fulani au kwa wafadhili fulani, takwimu na *data* tunazozitumia Wabunge ni zile zinazohusu majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ramani ya kila mmoja kwa Jimbo lake ingefaa kutolewa ingawa Wilaya inaweza kuwa ni ile ile. Kwa hiyo, kuchapisha ramani kimajimbo ingekuwa ni wakati muafaka, iachwe. Hivyo ninamwomba Waziri John Magufuli aangalie uwezekano kwa wapima mipaka na ramani kwenye vijiji waainishe mipaka ya Majimbo ya uchaguzi na wachapishe ramani inayoonyesha mipaka Kijimbo ili itusaidie katika *planning work* katika shughuli zetu za kujenga hoja za kuwatetea wananchi katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema nilikuwa na machache tu ya kuchangia katika Miswada hii. Kadri nilivyoeleza sioni la ziada, naomba tu tatizo hili lililopo na haya niliyopendekeza kama yatakubalika yatakuwa yamefunua ukurasa mwingine katika kuboresha utekelezaji wa Miswada hii itakayozaa sheria ambazo ninaamini kwa utekelezaji wa Mheshimiwa John Magufuli atazisimamia ipasavyo na sisi tupo nyuma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii nami kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote na mimi nimpongeze Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kwa kushinda vizuri na kukipa Chama cha Mapinduzi heshima kwa ushindi mkubwa uliotokea kule Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nimshukuru Mheshimiwa Waziri mtoa hoja, Naibu wake na watalaamu wake, kwa kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka lakini kwa namna ambayo ilikuwa kwa umahiri mkubwa sana ambao kila mtu unauelewa. Kuwasilisha Miswada mitatu kwa mpigo siyo kazi rahisi lakini Mheshimiwa huyu ameweza kufanya hivyo kwa umahiri mkubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ni-*declare* tangu mapema kwamba wachangiaji wa Muswada huu ambao ni mahiri sana katika maeneo mbalimbali ni wengi na mimi ningependa kujichimbia kwenye eneo dogo ambalo nadhani pengine wengi hawalisaidii sana ambalo ni eneo la mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufanya hivyo kwa sababu naamini baada ya kusoma Miswada yote mitatu kwa kweli na hasa ule wa kwanza wa *Land Use* ambao ningependa kuuzungumzia, kwa kweli umeainisha vizuri masuala ya mazingira *(environment)* na nawapongeza sana jana kwenye semina nilikuwa nina wasiwasi kidogo na Muswada huu, lakini baada ya kuupitia nimeona kwa kweli mazingira yametendewa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata hivyo ningependa kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja nawashukuru sana kwamba Muswada huu katika mchakato utakaokuwa unatumika umezingatia sana uwakilishi wa wadau mbalimbali. Taratibu zetu nyingi za kufanya mara nyingi huwa tunapuuza sana masuala ya wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona watoa mada hii au Muswada huu kwa kweli umeliangalia hili kwa makini sana na katika sehemu zote nilizozipitia suala la kuwahusisha wadau hilo limezingatiwa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile niendelee kusema kwamba nimeangalia ni vipi suala la *environment* ni *broad,* wanasema mtambuka na kwa kweli tunapozungumzia mazingira tunahusisha *interest* za binadamu, tunazungumzia ekolojia hata masuala ya *economics* tunaangalia huko na kwa kweli haya yote yamezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilipokuwa naangalia kwenye Ibara ya 28(1)(m) wanazungumzia kuhusu *creation or maintenance of migration corridors for wildlife*. Nilipenda kuzungumzia kuhusu suala la *creation*. Ku-*create* ni ku-*develop* (kuanzisha) upya. Sasa wanyama huwezi ukawalazimisha wewe wapite kwenye *corridor* au eneo ambalo wewe umeli-*create, they will never follow that.*

Kwa hiyo, hatuzungumzii suala la ku-*create.* Huwezi uka-*create* eneo jipya, wanyama wana akili, wana sababu zao kwa nini wanapita katika maeneo fulani. Kwa hiyo, *corridor* inakuwa *defined* na wanyama wenyewe kwa sababu ambazo wao wanazijua. Badala ya kuzungumzia suala la *creation* tungeweza kuzungumzia kidogo neno kama *designation,* kidogo kwangu linakuja, lina maana nzuri zaidi kuliko kuzungumzia ku-*create.* Ku-*create* ni kuunda upya. Huwezi ukaunda *corridor* ukawalazimisha wanyama kama ng’ombe lazima wapite hapo, hawatapita. Naomba Mheshimiwa Waziri aangalie kipengele hicho.

Ya pili, kwenye ile Ibara ya 29 kifungu kidogo cha (iii) ambapo ni yale masuala ya *Preparation of the National Framework Plan,* ukisoma kwenye kifungu kidogo (f) ambacho wanasema kina-*include* ku-*identify actual or likely problems*. Ukienda kwenye kifungu (i) anazungumzia kuhusu ku-*investigate specific as well as general adverse impacts.* Sasa kwangu mtazamo wao hapa ni *very negative.* Hii ina-*paint* mbaya sana kwenye masuala ya e*environmental assessment* kana kwamba *environmental impact assessment* huzingatia *negative effects,* masuala mabaya tu. Lakini kwa kweli *environmental assessment* inazingatia hata masuala yaliyo *positive,* namna ya kuboresha mambo mazuri yakawa mazuri zaidi, *best practices.* Kwa hiyo, tusiwe *very negative* katika kuangalia mambo ya mazingira, lakini vile vile tuangalie namna ya kufanya mambo mazuri yakawa mazuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo kwenye Ibara ya 41 na 42 ambako Muswada unazungumzia juu ya *re-adjustments* na *adjustments* kwamba unaweza ukairekebisha *plan* kama kuna sababu za kufanya hivyo. Iwapo *Land Use Plan* ilikuwa

*subjected* kwenye *environmental assessment* kwa kawaida *any re-adjustment,* mabadiliko yoyote tutakayoyafanya yanakuhitaji uainishe tena suala la mazingira na nilipokuwa nasoma Muswada huu unaruhusu kufanya mabadiliko kwenye *Land Use Plan* bila kuzingatia masuala ya *environment.* Nilikuwa naomba sana, suala hili ni muhimu kwa sababu mabadiliko tutakayoyaweka yanaweza yakaleta athari kubwa sana kwenye mazingira, kwenye maisha ya binadamu hata na viumbe vingine. Kwa hiyo, ni bora tukaangalia upya kuhakikisha kwamba mazingira hayaathiriki kwa mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Ibara ya 58 ambayo inazungumziwa suala la *monitoring* na *evaluation,* kwanza, nilifurahi sana kwamba Muswada huu unazungumzia hata ku-*monitor*. Suala la ku-*monitor* kwa kawaida tunaangalia baada ya kujiwekea malengo hata tume-*identify impacts whether positive or negative* tunataka kuangalia: Je, *are they being dealt with?* Zinashughulikiwa au hapana? Kama hazishughulikiwi, hatua gani ichukuliwe? Sasa ni suala zuri sana ku-*monitor* na kufanya *evaluation* lakini sikuona mahali ambapo Muswada unazungumzia. *So what!* Baada ya kufanya *evaluation* na una-*carry out monitoring,* napata *monitoring results: What you do with that? Results* hizi unazitumiaje? Ni nani afanye hiyo kazi? Kama ni ku-*plough back* katika *plan* ili kuboresha nani afanye hilo? Niliona hilo suala halikuzingatiwa katika mpango huu.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba vitu hivi vichache ambavyo nimevisema viangaliwe na kama nilivyosema, kama mwanamazingira, nimeridhishwa sana na Muswada huu, umezingatia vizuri masuala ya mazingira. Niliomba hivyo vitu vichache Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha, tafadhali ningependa kusikia watazingatia kwa namna gani. Baada ya kusema hivyo, bila matatizo yoyote, bila kinyongo, nauafiki Muswada, nauunga mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Miswada hii mitatu muhimu sana kwa wananchi wetu wa Tanzania kuhusu mipango ya ardhi na matumizi ya ardhi. Naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mtutura, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na kuapishwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada hii mitatu narudia kusema kwamba ni muhimu sana kwa maendeleo ya Tanzania huko tunakoelekea. Nasema ni muhimu kwa sababu inaweka utaratibu na msingi mzuri wa kupanga Miji ili kutoa huduma muhimu zinazohitajiwa katika maendeleo wanamoishi wananchi, kwa mfano, maji, umeme, miundombinu mbalimbali, majitaka na kadhalika. Ni nafasi muhimu kwa wananchi inayowezesha kubadilisha sura ya Miji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Sheria hii itasaidia sana katika kuwezesha mipango ya kisasa kufanyika. Hivi leo yapo magari ambayo yameundwa na yakishaanza kutumika, yana programu maalumu ambapo ukiiweka programu hiyo gari itakuelekeza na kukupeleka mahali unakotaka kufika. Sasa kama huna Mji mzuri wa kisasa, hivi magari haya kweli yanaweza yakafanya kazi Tanzania? Maana yake lazima uwe na eneo maalumu, kwa mfano, barabara, namba za nyumba na uhakika wa *destination,*

ukiiprogramu gari yako hiyo itakwambia na itakuelekeza sasa tunakaribia mahali unapotaka kufika, mita 200 baadaye kata kushoto, gari litakwambia ukifika mita nyingine 100 sasa kata kulia na unapokaribia kwenye eneo la *site* gari linakwambia sasa tunakaribia kufika na linapofika linakuambia sasa tumefika mahali nilipokusudia kufika. Haya yanawezekana tu kama mji umepangwa vizuri katika mfumo wa kisasa.

Kwa hiyo, ni vyema Watanzania tukafahamu kwamba huko ndiko tunakoelekea na sheria hizi ndizo sheria ambazo zitawezesha haya kufanyika na yakawawezesha Watanzania kunufaika na teknolojia mpya ambazo sasa zinaendeshwa duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetazama kwa makini vile vile mambo kadhaa. Nimetazama uwezo wa Mheshimiwa Waziri na katika fomu hii ya marekebisho *(amendment)* yapo mambo mengi sana ambayo kweli yamewekwa mikononi mwake, ana uwezo nayo na anaweza akayatungia sheria. Ni mengi kiasi kwamba yamechukua *alphabet* zetu zote kuanzia (a), (b) mpaka (x), (y), (z) na yamevuka hata (x), (y), (z), yalivyokuwa mengi tumeanza *alphabet* mpya *double (a)* nadhani vile vile baada ya maelezo mengine yanaweza yakaongezeka. Ni mengi kweli. Lakini yote ni muhimu sana.

Lakini jambo moja ambalo pengine mimi nimeliona katika haya yote ni katika kifungu hicho hicho sehemu ya 78. Vile vifungu (a), (b), (c) na (d) tukienda mpaka kwenye kifungu (k) pale, Mheshimiwa Waziri anakuwa na uwezo wa kutunga Sheria zitakazohusu urefu na upana wa barabara. Sasa urefu wa barabara, upana wa barabara vile vile ni mambo ambayo majukumu yake yapo katika Wizara nyingine ya Miundombinu. Sasa leo Waziri huyu anayo majukumu hayo ya kutazama urefu wa barabara na upana wa barabara.

Ningeomba basi angalau tuongeze kifungu kidogo kwa kusema kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana ya Miundombinu. Tukimwachia peke yake na hasa sisi tunavyomfahamu Mheshimiwa Magufuli, ana uwezo mkubwa, anajua urefu wa barabara zote nchini, sasa tukiweka madaraka yote mikononi mwake anaweza akamsaidia sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kufanya kazi ambazo pengine angepaswa kuzifanya yeye, ningeomba Mheshimiwa Waziri tufikirie kuongeza kifungu kidogo hicho ili haya yaweze kwenda sambamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mategemeo makubwa ya wananchi sasa hivi ni kuelekea katika Jumuiya au Shirikisho la Afrika Mashariki. Ni vyema tukatafsiri kwa vitendo na tukaangalia: Je, ni kwa kiasi gani sheria hizi tatu zinamwandaa mwananchi na kumjengea mazingira mazuri ya kuweza kuingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki? Je, Sheria hizi zinatulinda? Je, Sheria hizi zinatoa haki kwa Mtanzania kwanza, kipaumbele kabla ya wageni?

Maana yake baada ya kufungua mipaka, hatua ambayo inaweza ikafikiwa hivi karibuni ni kutumia sarafu moja basi Wakenya, Waganda watakuwa na haki. Kama ambavyo Watanzania watakuwa na haki ya kuingia Kenya na Uganda pia watakuwa na haki ya kuingia Tanzania. Je, watakapoingia Tanzania sheria yetu inasema nini kuhusu mwenye ardhi Mtanzania halisi mwenyewe? Tunawapa madaraka na mamlaka hawa

waweze nao kama wakati huo katika Shirikisho nao wawe na haki ya matumizi ya ardhi hii sawasawa na Watanzania? Watakuwa na haki ya umiliki wa ardhi sehemu hii ya Tanzania kama Watanzania wenyewe? Hayo ni mambo muhimu sana ambayo lazima tuyaangalie.

Ni vyema tukaangalia na tukaongeza mambo mawili makubwa yafuatayo:- Kwanza, hii sheria sasa kwa kuzingatia huko tunakoelekea kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki, basi sheria yetu hii na miongozo hii tunayotoa sasa iseme waziwazi kuhusu umiliki wa ardhi kwa wageni. Hatuna sababu ya kuona haya katika hilo, tuseme waziwazi, wageni watakuwa na haki gani ya kumiliki ardhi? Lakini ili kuwasaidia Watanzania kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Mwakyembe, ni vyema tukaweka waziwazi katika sheria hii.

Jambo lingine moja muhimu la kusema, ni kwamba Sheria hii ilenge katika kuwaelewesha wawekezaji kwamba wanapotaka kuwekeza katika ardhi ya Tanzania kwa mfano, katika viwanda, basi tunasema waziwazi katika maeneo hayo, wananchi waliokuwa katika eneo linalokusudiwa kuwekeza wanapata nafasi ya kuwa na hisa katika viwanda vitakavyovyojengwa. Hakuna sababu ya kusubiri sheria nyingine, hii ndiyo sheria yenyewe. Sasa tuweke msumari hapa hapa mapema kabisa ili mwekezaji ajue kwamba licha ya kulipa fidia, bado mwananchi mwenye eneo ambalo linakusudiwa kuwekezwa atakuwa na haki ya kupata hisa katika uwekezaji unaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni muhimu sana. Lakini vile vile tunafanya *land planning*, tunafanya upimaji wa Miji. Kuna jambo ambalo mara nyingi tunalisahau, tunapima Miji lakini hatutengi maeneo maalumu kwa ajili ya viwanda. Ni vyema tukahakikisha katika upimaji wetu kila Mji tujenge maeneo maalumu kabisa kwa ajili ya viwanda. Hili litatusaidia kwamba hata tutakapofikia tunapata wawekezaji, wanahitaji maeneo ya uwekezaji katika viwanda, basi tuna maeneo maalumu kabisa ambayo tunawaelekeza kwenda kuwekeza kule. Badala ya mtindo uliopo sasa ambapo tunaanza kuwahamisha watu, watu wanalalamika kuhusu fidia, wanaleta migogoro na wawekezaji lakini sababu kubwa ni kwa sababu sisi wenyewe katika mipango yetu hatutengi maeneo maalum kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Waziri wa Viwanda alitukumbusha kuhusu hili na mimi leo hapa namsaidia kuhakikisha kwamba ndani ya sheria hizi, mpango wa kupima maeneo maalumu ya viwanda unatekelezwa. Kwa kiasi gani? Ni kwa kutazama maendeleo na upeo wa mbele wa zaidi ya miaka 40 mpaka 50 mahitaji yatakuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kufahamu hayo, basi tunaweza tukasema tutatenga maeneo ya kiasi gani na ya ukubwa gani. Kwa sababu kutenga vile vile maeneo makubwa sana na yakakaa wazi kwa muda mrefu sana bila kutumika yamekuwa yakileta matatizo na migogoro kwa wananchi. Watu wanayavamia kwa sababu wanayaona yamekaa kwa muda mrefu bila kutumika. Hivyo lazima tutumie busara za kutosha wakati tuna-*determine* kiasi cha eneo tunalotaka kupima kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kwamba sheria hii itatusaidia sana katika maeneo ambapo tumeanza kukuza au kuteua Miji midogo kama Muheza na Wilaya ya Mkinga ni maeneo ambayo miji midogo sasa inajengwa. Ni vizuri miji hii ikajengwa kitaalamu kabisa kwa kuzingatia haya yote ambayo tumeyazungumza hapa. Maeneo yakapimwa vizuri, wale ambao mpaka sasa katika baadhi ya maeneo ya miji midogo ambayo sasa imepewa hadhi kama Muheza bado kuna watu wana mashamba ndani ya maeneo yanayofikiriwa kuwa maeneo ya miji midogo.

Ni vizuri tukaangalia utaratibu mzuri wa kuwalipa fidia wale ambao walikuwa na maeneo yanayogeuzwa kuwa Miji midogo na lazima kwa mujibu wa sheria hii yatapimwa. Kiwango cha fidia lazima tuangalie upya hali ya sasa hivi ya kiuchumi ili tuweze kuwalipa wananchi fidia halali itakayoweza kuwatosheleza kuacha shughuli ambazo wamekuwa wakifanya katika ardhi waliokuwa wakimiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja la mwisho ambalo ningependa kuliongeza katika haya ni kwamba tuweke kifungu ambacho kitasaidia katika utekelezaji wa mabadiliko yanayotolewa na viongozi wa Taifa. Mheshimiwa Rais anaweza akaamua kwa mfano, muda wa miaka michache tu iliyopita Manispaa, Miji, zilikuwa bado mpaka sasa hivi wanayo sheria ya majengo kwamba kila nyumba inayojengwa ndani ya maeneo ya Mji wanalipa kodi ya majengo. Lakini zipo nyumba ambazo ni za hali ya chini sana, za tope, fito na miti. Mheshimiwa Rais alisema, basi wakati Manispaa na Miji inafikiria hayo hizi nyumba za tope na fito zisihusishwe na kodi hiyo ya majengo.

Sasa Manispaa na Miji wana sheria zao ndogo ndogo ambazo zimekwishapitishwa. Tunasema nini kuhusu mabadiliko haya na mapendekezo yanayotolewa na viongozi wa kitaifa ambayo yanakwenda kutengua kwa kiasi fulani sheria ambazo zipo katika Halmashauri na Miji yetu midogo? Basi tuweke *provision* hapa ambayo inasema vile vile tutatoa nafasi ya kutekeleza maagizo yatakayotolewa na viongozi wa kitaifa kama Mheshimiwa Rais, katika maeneo ambayo tunadhani ameona ni muhimu kupunguza ukali wa sheria hiyo kwa ajili ya wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zote hizi, mmiliki wa sheria hizi zote ni Mheshimiwa Rais. Kwa sababu licha ya kwamba Wabunge tutaipitisha hapa, lakini haitaanza kutumika bila Mheshimiwa Rais mwenyewe kuikubali. Kwa hiyo, ni vyema tukaiweka *provision* ya kuruhusu pale atakapotoa mapendekezo, basi yaweze kuingizwa na kuheshimiwa yaweze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kusema sasa kwamba ninaunga mkono Miswada yote hii mitatu. Nafahamu ipo chini ya Wizara ya viongozi ambao kwa kweli ni makini, wanaijengea heshima Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na ninaamini heshima hiyo itadumu na ninawatakia kila la kheri katika kazi yao hiyo ya kuijengea Wizara ile heshima ya kiutu na nidhamu ya utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie machache katika Miswada miwili

inayohusiana na Mipango ya Miji na ardhi kwa ujumla. Lakini nianze kwa kuungana na wenzangu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mtutura na wale wote walioshirikiana naye kwa ushindi mkubwa uliomwingiza katika jengo hili. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tuanze kuujadili Muswada huu mara nyingi imedokezwa kwamba, tatizo linaelekea sio sheria, kwa sababu Sheria zimekuwepo. Kumekuwepo sheria zinazotawala masuala haya haya tunayoyazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana sheria hizo zina upungufu ambao tunataka kuurekebisha sasa. Lakini jambo muhimu sana ni utekelezaji wa sheria hizo na mimi nahofu kwamba tunaweza tukatunga sheria nzuri sana za matumizi ya ardhi za Mipango Miji, lakini kama hatutaweka utaratibu mzuri wa kuzitekeleza tutaendelea kubaki hapa hapa tulipo na hali hii mbaya iliyopo itaendelea kuwepo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tungeomba Waziri atakapokuwa anajumuisha atuhakikishie kuwa pamoja na mambo atakayofanya ni kuweka utaratibu utakaohakikisha kwamba haya mambo mazuri tunayopitisha hapa yanatekelezwa, vinginevyo huu muda tunaoutumia tungeweza kuutumia kwa shughuli pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelezwa hapa na Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba miji yetu, hasa Jiji la Dar es Salaam asilimia kati ya 70 na 75 ni makazi ambayo hayakupangwa. Mimi nataka niseme kwamba kwa Jiji la Dar es Salaam ni zaidi ya asilimia 75. Hivi tukiwa hapa, wananchi wanaendelea kujenga katika maeneo ambayo hayakupangwa. Naomba tutofautishe mambo mawili, tunachozungumzia hapa ni kupanga mji ili ujengwe kama mji. Hatuzungumzii unajenga nini katika eneo lile lililopangwa. Hilo ni suala tofauti na linatawaliwa na mambo tofauti kwamba unajenga nini katika eneo, inatawaliwa na kanuni za ujenzi katika eneo lile.

Lakini eneo lile linapangwa, barabara zinaonyeshwa. Maeneo ya huduma yanaonyeshwa, kwa hiyo, kila kitu kinawekwa mahali pake, halafu ndipo mtu anapokuja sasa na yeye anaweka na yeye anachotaka kuweka katika eneo hilo kwa utaratibu na misingi iliyowekwa. Hilo ndilo lililokosekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu niseme kwamba, kuishi katika mji wowote ni lazima kuzingatia masharti ya kuishi mjini. Usipozingatia masharti, hatari zake ni kubwa kweli kweli. Zile picha tulizoonyeshwa kwenye semina jana, hebu ungefikiria ungetokea moto katika eneo kama lile!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, huwezi kupita kati ya Spika na Msemaji. Endelea!!

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kumkumbusha. Katika baadhi ya maeneo, kama ungetokea moto hata pa kukimbilia hakuna, magari ya Zimamoto hayawezi kufika na kama yakitokea mafuriko ni balaa. Katika baadhi ya miji ilikuwa imepimwa maeneo yasiyofaa yakaachwa bila kupimwa kwa sababu hayafai kukaa. Lakini wamekuja wananchi wamejenga na mengine ni njia

ambazo ni za kupitisha maji ili yaelekee baharini na ni matatizo kila mvua zinaponyesha. Ukienda leo Msimbazi karibu bonde lile litajaa kwa kujengwa.

Sasa tunachosema ni kwamba, lazima hii miji ipimwe, isipopangwa ni hatari kweli kweli kwa maisha ya wananchi, lakini ni hatari pia kwa sababu mambo tunayotaka kufanya ya maendeleo hayawezekani kufanywa. Mheshimiwa Mntangi sasa hivi amezungumzia mambo ya kujenga viwanda. Hivi viwanda vinajengwa wapi kama hamkutenga maeneo ya kujenga viwanda? Sasa hivi Dar es Salaam tuna tatizo kubwa sana la maeneo ya kujenga shule kwa sababu maeneo yote yamejengwa, hakuna maeneo yaliyoachwa kwa ajili ya huduma kama shule, hospitali na kadhalika. *(Makofi)*

Sasa tunachosema, tupange hii miji na tuwahi. Tatizo letu ni kwamba tunafumbia macho mambo yanayotokea katika miji yetu sasa. Wananchi wanajenga, tunamwona anajenga kwenye korongo, tunakaa kimya. Mvua zinaponyesha kukatokea mafuriko tunakimbia kwenda kumwangalia kama kanusurika ama hakunusurika. Sasa kwa nini hatukuwahi kumpatia eneo la kufaa kujenga? *(Makofi)*

Viwanja vikipimwa, tunapima viwanja vinne, vitano halafu vinapatikana kwa shida kweli kweli. Kwa hiyo, kukipata ni lazima uwe unafahamiana na wanaovigawa kwa maana ya kufahamiana. Ndiyo! *(Kicheko/Makofi)*

Mara ya kwanza tumepimiwa viwanja vingi, ni juzi vilipopimwa viwanja 20,000 na sina hakika kama zoezi lile la kuendelea kupima viwanja linaendelea. Sasa hii miji itakuwa ni mahali pa namna gani? Mahali ambapo kila mtu anaamua kufanya anavyotaka na mwisho itakuwa ni hatari kubwa sana. Sisi tunaopita kwenye Majimbo yetu unafuata barabara ukitegemea itakutoa upande wa pili, unakuta kuna mtu kajenga kaziba njia. Kwa hiyo, lazima urudi ukatafute njia ya kichochoro kingine cha kwenda huko unakotaka kwenda. Tunachosema ni kwamba, hii miji ipangwe.

Ninavyojua kwa Jiji la Dar es Salaam, *Master Plan* ya mwisho iliandaliwa mwaka 1970, miaka 37 iliyopita na ile *Master Plan* haikufuatwa, maeneo yaliyotengwa kwa shughuli mbalimbali yalitumika kinyume kabisa na ilivyokuwa imekusudiwa labda maeneo yaliyobaki kwa kiasi kikubwa ni maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Jeshi kwa sababu walihakikisha kwamba hayavamiwi. Lakini maeneo mengine yote yalivamiwa na kutumika kama watu walivyoamua kuyatumia.

Tunachosema ni kwamba, sasa hebu miswada hii itukumbushe tusimame kwanza tufanye tathmini ya hapa tulipo na tukubaliane tunakwendaje huko mbele. Mimi nikifikiria maeneo yangu ya Kimara, Mbezi Luis, Kibamba, Goba, sasa hivi wananchi wanajenga na kila mmoja anajenga anavyotaka. Kinachokosekana hapa siyo uwezo wa wananchi kujenga, ni wananchi kuwekewa utaratibu wa kujenga ambao utawawekea barabara za kufika kwao, utawaachia maeneo ya huduma na kadhalika na utazingatia hifadhi ya mazingira kama alivyozungumza Mheshimiwa Profesa Mwalyosi muda mfupi uliopita. Hilo ndilo tunaloomba lifanyike. Lakini tukiendelea kufumba macho na kuacha hali hii iendelee itakuwa hatari kweli kweli.

Ukienda Mji wa Tanga utakuta mitaa imepangwa, kwa hiyo kuna Mtaa wa kwanza, wa pili, wa tatu, wa nne, wa tano na kuendelea. Sasa ukienda kule Kimara huo mtaa utauona wapi? Barabara ya kwanza mpaka ya kumi na moja lakini ukienda katika maeneo tunayojenga sasa hivi hakuna barabara, kuna uchochoro ambao mtu anaweza kujenga tu akauziba, hakuna hata mamlaka inayomkumbusha kwamba hii ni barabara usijenge kwenye barabara hii. Hii ni kwa eneo la mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye maeneo ya Vijijini ni lazima nako tuwe na utaratibu wa matumizi ya ardhi. Sasa hivi katika Kijiji, watu wanajenga tu wanavyoona inawafaa. Lakini lazima tuhakikishe kwamba tunaacha maeneo kwa ajili ya kilimo na yasiondolewe katika kilimo bila kuwa na utaratibu mgumu kama huu wa kubadilisha matumizi ya ardhi Mjini kwa sababu kilimo ndicho kinachowapa wananchi uwezo wa kuishi katika Vijiji. Sasa kama ile ardhi ya kilimo inayofaa kwa kilimo, itatumiwa kwa mfano, kwa makazi au kwa shughuli zisizohusika ni kwamba patafika mahali hiyo ardhi ya kilimo haitakuwepo tena. Tulipata kuwa na mashamba makubwa yaliyokuwa ya Serikali au ya Mashirika ya Serikali, ilipofika mashamba yale hayatumiki tena, ombi la kwanza ni kwamba tupeni yale mashamba tugawane. Lakini mkigawana yale mashamba leo kila mmoja akapata heka moja na nusu kesho hamna mahali pa kulima, hata ile ajira ambayo ingepatikana kutokana na mashamba hayo haipo tena.

Kwa hiyo, tunapendekeza kwamba huu muswada uhakikishe kwamba maeneo yanayopangwa kwa ajili ya kilimo yanaendelea kutumika kwa kilimo na kama kuna haja ya kuyabadilisha kutoka kwenye kilimo kwenda kwenye matumizi mengine, basi utaratibu mgumu kama huu wa kubadilisha matumizi ya ardhi ufuatwe. Hivyo hivyo maeneo ya misitu ambayo yanaachwa na maeneo yanayotengwa kwa ajili ya mifugo na kadhalika, yabaki katika matumizi hayo na yabadilishwe tu pale ambapo utaratibu utakuwa umefuatwa. Kama tukifanya hivyo, huko mbele tunakokwenda naona kutakuwa ni kwa amani, kwa utulivu, kwa usalama na maendeleo yetu yatakuwa ya uhakika zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu Muswada ni mzuri na unazungumzia mambo mengi sana. Ni Muswada ambao unasisitiza sana utaratibu shirikishi, kupanga, nami nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hilo. Maana sasa hivi kuna tatizo, unaweza kuomba kiwanja ukapewa na Manispaa ya Kinondoni lakini ukaambiwa kilishagawiwa na Wizara. Kwa hiyo, sasa hawa wanatazama kwa macho kidogo ya husuda kwa sababu mmoja akigawa na mwingine akagawa unaishia na kitu wanachokiita *double allocation.* Nategemea kwa utaratibu huu unaopendekezwa katika sheria, mamlaka zinazohusika zitashirikishwa katika kugawa ardhi katika maeneo yao na kwa hiyo, migongano kama hii haitakuwepo tena, vinginevyo tutaendelea kuwa na matatizo kama yaliyopo hivi sasa.

Lakini napata tatizo; moja, tumeweka mamlaka hizi za kugawa ardhi, tumesema Kijijini mamlaka, Wilaya ni mamlaka, Mji, Manispaa, Jiji au Jiji Kuu ni mamlaka. Lakini sioni mahali ambapo tumezungumzia jinsi wanavyopata rasilimali za kutekeleza majukumu yao. Kijiji tukikipa mamlaka ya kugawa matumizi ya eneo lake: Je, utaalamu kinapata wapi wa kufanya kazi hiyo? Kama utalaamu hawana, hata wangekuwa na

*resources* za fedha, ni nani atakayewafanyia kazi hiyo? Tungeomba Waziri atufafanulie hili vizuri kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda katika ngazi za Wilaya na Sekretarieti za Mkoa tunakuta kuna watumishi, lakini mara nyingi sana tumekwama kwa sababu hakuna fedha za kufanya kazi hiyo, tumekuwa tukitaka kupima eneo la Goba, kwenda mpaka Madale, kwenda mpaka Mbezi Luisi ili eneo lile lipangwe vizuri wananchi waweze kukaa kama wanavyotakiwa kukaa. Tumekwama kwa sababu hatuna fedha za kupima japokuwa wapimaji tunao, kwa hiyo, tuna haja ya kuangalia hivi hizi *resources* zinapatikanaje?

Lakini ningeomba; moja, niungane na Mheshimiwa Dr. Mwakyembe, kwamba ni lazima upatikanaji wa ardhi uwe mwepesi kidogo. Sasa hivi tunapima hivi viwanja 20,000, lakini bei ya kiwanja haishikiki. Kile kiwanja ni kuanzia Sh. 400,000/=, Sh. 500,000/= mpaka milioni na zaidi. Sasa mtu mshahara wake ni Sh. 200,000/= kiwanja anunue Sh. 4,000,000/= na kujenga ajenge kwa Shilingi ngapi sijui! Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia nini tunachotaka kufanya hata kama itabidi Serikali itoe ruzuku bei za hivi viwanja ipungue ili wananchi waweze kujenga kwa utaratibu unaofaa. *(Makofi)*

Kutokujenga kwa utaratibu unaofaa kuna madhara makubwa sana kwa wananchi hao na kwa taifa kwa ujumla, na kwa hiyo kuna haja ya kuwasaidia wananchi ili waweze kujenga. Nilikwenda Botswana siku moja nikashangaa kidogo, maana mimi natoka Tanzania. Tumekuta eneo limepimwa, wameweka barabara za lami, wameweka nguzo, taa za umeme zinawaka na maji yapo. Nikauliza, hapa kuna nini? Mbona taa zinawaka porini? Nikaambiwa hapa pamepimwa, sasa pako tayari kugawia wananchi. Yaani mwananchi akienda pale anachotafuta ni pesa zake ajenge basi, huduma nyingine zote zimeshawekwa.

Sasa kwenye vile viwanja ishirini, ukitaka kwenda lazima upite kwenye viwanja vya watu wengine na wao wakijenga lazima uende ukapite kwenye makorongo pengine ukwame hata kwako hutafika. Sasa kuna haja ya kuangalia haya mambo mazuri yanayofanyika sehemu nyingine na sisi tuyachukue tuyafanye huku kwetu ili mambo haya yaweze kwenda sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tena kwamba hii miswada ni mizuri sana na inaweka utaratibu mzuri sana wa kufuata, tunaomba basi ufuatwe. Tunaomba kuanzia sasa tusimamie tuhakikishe kwamba kwanza tunasimamisha huu ujenzi holela unaoendelea ili tuweke utaratibu mzuri utakaofuatwa, kwa kufuata sheria hizi. Lakini kama tutaendelea kubaki namna hii, kama Mkoa wetu wa Dar es Salaam unavyojengwa sasa hivi, itakuwa ni hasara kubwa sana.

Mwisho, naomba tutambue kwamba Jiji la Dar es Salaam sio kisiwa, lina uhusiano wa karibu sana na Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Bagamayo na kadhalika. Kama unataka kupanga ukuaji wa Jiji la Dar es Salaam, lazima upange pia ukuaji wa miji hii mingine kwani inahusiana na Jiji la Dar es Salaam. Lakini sisi tunapanga, tumepata pesa kidogo za kupewa viwanja 10,000, tunakwenda tunapima pale Goba, lakini basi

tunamaliza. Lakini Goba panahusiana na maeneo mengine na baadaye patahusiana na miji ambayo inazunguka Dar es Salaam. Tukizingatia mambo haya yote na nini, nina hakika tutakuwa tena na miji ambayo imepangika. Mimi nina hofu kwamba tutakapokuwa na uwezo wa kupanga upya hii miji yetu, tutabomoa karibu theluthi mbili ya hii miji iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hii hoja, lakini nitamtafuta Waziri tuzungumze kwamba utekelezaji unaanza lini? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuzingatia kanuni, maana yeye amebana pale muda mrefu kwa sababu kulikuwa na msemaji.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami nichangie hoja hii muhimu ya Miswada mitatu iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, kwa kuwa ninazungumza kwa mara ya kwanza toka matukio ya misiba iliyolikumba Bunge letu ilipotokea, nadhani nitumie fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Tabora kuwapa rambirambi jamaa na ndugu wa Marehemu Akukweti. Pia napenda nimpongeze Mheshimiwa Batilda Buriani kwa kuchaguliwa kuwa Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Shughuli za Bunge. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Mtutura kwa kupata ushindi katika Jimbo la Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza katika wakati ambapo Waheshimiwa wengi wamekwishazungumza na hoja nyingi nilizotaka kuzizungumza zimekwishazungumzwa kwa namna moja au nyingine. Aliyezungumza hivi karibuni utafikiri alikuwa anaangalia *notes* zangu kwenye masuala kadhaa. Sasa nianze na hili la kupanga Miji. Ukiweka miundombinu yote kabla ya kuruhusu watu, huo ndiyo utaratibu ambao ninautarajia ufuatwe baada ya sheria hii kuwa imepita. Kwa sababu ni kweli tuko nyuma sana ndugu zangu katika maendeleo ya kisasa. Kaka yangu Mheshimiwa Keenja ametoa mfano wa Botswana, mimi niongezee hapo Pretoria na Johanesburg, ndivyo wanavyofanya wenzetu. Viwanja vinapimwa, vinawekewa huduma zote muhimu pamoja na laini za simu, wewe ukienda unavuta tu unapojenga, unavuta vyote, maji, simu, umeme unaunganisha maji machafu kwenye msingi mkubwa unaopita katika eneo ambalo unajenga.

Sasa *proper land use* kwa maana ya Muswada huu tunaoujadili sasa na hatimaye tutaupitisha, ningeutarajia basi tubadilike twende katika hatua hiyo. Sisi Watanzania huduma zinafuata watu baada ya kuwa wameshakuwa huko siku nyingi. Ushahidi tosha uko katika maeneo mengi, labda kwa kukumbushana tu, niwaondoe hapa sasa kifikra Waheshimiwa Wabunge niwapeleke Mbezi. Mkifika Mbezi kule Dar es Salaam kuna majumba mazuri sana, lakini hakuna mifereji ya maji machafu. Kila mmoja anavuta umeme wake, barabara ndiyo haisemeki. Lakini majumba mazuri, tena ya fahari. Sasa iko wapi *Land Use Planning* kwa maana ya makazi ya watu? Sasa hapo nilitaka nilisisitize ili Wizara inayohusika ilitilie maanani na kuangalia mkakati wa kuweza kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya upimaji hususan ya viwanja vya ujenzi iko nyuma sana na kasi ya ujenzi wenyewe ilimradi wananchi wanatangulia upimaji. Kule Tabora kuna maeneo yanajulikana kama Kariakoo, Kidatu, Tambuka Reli na sehemu nyingine. Maeneo haya wananchi wametangulia upimaji. Kwa hiyo, wanaishi huko, ndiyo lile alilolisema Mheshimiwa Kaka Keenja, anasema wale wapimaji wakienda kupima sasa itabidi Serikali iingie gharama kubwa zaidi kwa kuwalipa wale wananchi. Lakini wale wananchi bahati mbaya wataambiwa mlipojenga hapa, sisi hatukuwapa kibali, kwa hiyo hatuwalipi. Sasa katika hali hiyo tunawaweka wananchi wetu katika kitendawili.

Lakini nitumie fursa hii kumkumbusha Mheshimiwa Waziri Magufuli kinachoendelea kule Kibela Nairobi. Kibela *is the shut down* ya hali ya juu sana, hakuna barabara kama ambavyo wenzangu walioendelea kuzungumza walisema kule umeingia mradi wa *World Bank* chini ya ufadhili wa kitengo cha Mama mmoja anaitwa Prof. Tibaijuka, Mtanzania. Prof. Tibaijuka katika himaya yake ndiye anashughulika kupanga Kibela. Ni pesa nyingi sana zinahitajika. Kwa hiyo, ningeshauri vilevile Wizara yetu ya Ardhi ikaangalia namna gani tunaweza kuunganisha nguvu na mama Tibaijuka ili aje atusaidie na sisi hapa Tanzania hususan katika Miji mikubwa kama Dar es Salaam, kuyarekebisha maeneo aina ya Manzese, Buguruni, Tandika, kule Tabora, Kariakoo na Tambuka Reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachojitokeza hapa ni kwamba kasi ya upimaji inakuwa ndogo ukilinganisha na mahitaji ya viwanja. Labda ni kutokana na upungufu wa fedha. Nilikuwa napitia Muswada huu, naona kwamba utakuwa unatumia fedha za bajeti mwaka hadi mwaka; kwa utaratibu huo hatuwezi kuwa na matumizi tunayoyatarajia. Nashauri uundwe mfuko maalumu kwa ajili ya upimaji wa viwanja na mfuko huo utafutiwe vyanzo vya uhakika na sio bajeti ambayo ikishafika hapa tunasema tuna mafuriko, tuna njaa, hatuna umeme, kata hapa! Kata hapa! Unakata na kwenye viwanja, hatuwezi kwenda!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mengi yamekwishazungumzwa, labda sasa nihitimishe kwa kuongezea jambo ambalo limekuwa katikati ya taaluma yangu na ambalo limekuwa linanikera sana katika mipango ya maendeleo ya miji yetu, kwa maana ya ujenzi. Nchi yetu haina chombo kinachotoa mikopo ya kujenga nyumba na hauwezi ukajadili. Mimi nimeshangaa Muswada huu unazungumzia ardhi, unapita kimya kimya hakuna eneo moja linazungumzia *mortgage finance* na wakati tunataka kuboresha maisha ya Watanzania, nimeshangaa sana. *(Makofi)*

Sasa hoja yangu hapa ni kwamba, inawezekana *technically* ni kwamba katika hii miswada mitatu suala la *mortgage finance* haliingii, lakini tunazungumza mambo ya ardhi na makazi, kupima maeneo ya makazi. Sasa haya makazi yatajengwaje bila fedha? Ndiyo maana natumbukiza suala la *mortgage finance*. *Mortgage financing* Mheshimiwa Waziri anayehusika na eneo hili anafahamu. Ukweli ni kwamba, ni bidhaa kwa maana ya *product* ya mabenki, sio lazima uanzishe Benki mpya ili iweze kutoa *mortgage finance*, mabenki yaliyopo yanaweza kutoa *mortgage finance* ikiwa *environment* yetu itakuwa *conducive* kwa mabenki hayo kutoa *product* hii. *(Makofi)*

Kwa sasa *product* hii itolewe na mabenki yaliyopo nchini kwa sababu *the environment is just not conducive* na hasa kwenye suala zima la ku-*foreclose* kwa maana ya kushika dhamana ambayo yule aliyekopa aliwekeza Benki. Sheria yetu ya Ardhi, sikumbuki ni *Chapter* gani, lakini katika sheria nyingine ya Ardhi ambayo inazungumzia suala la *collateral* na *mortgage,* mabenki yanapata taabu sana kushika dhamana zilizowekwa kwa ajili ya ku-*finance* ujenzi wa nyumba. Sheria inataka kabla hujaishika nyumba hiyo iliyojengwa kwa mkopo wa Benki utoe *notice* isiyopungua miezi mitatu. Hapa kwa kuwa sijarudi kule kwenye sheria yenyewe nitoe tahadhari kwamba nisiseme miezi mitatu, niseme tu unatakiwa tu utoe *notice* ya muda mrefu kwa sababu baadaye inaweza kuonekana nimesema uongo.

Lakini sheria inataka Benki itoe *notice* ya muda ambao mimi nauita tena *notice,* sio moja, mbili, unatoa ya kwanza, unatoa ya pili, kama haijajibiwa ndiyo unashika ile nyumba ili uweze kuiuza. Mabenki yanasema ni nani uliyemkopesha ameshindwa kukulipa, unampa *notice* mbili na bado ile nyumba utaikuta katika hali ya kuweza kuiuza ukapata fedha nzuri, haiwezekani. Tukubali kwamba, kama tunataka *mortgage financing* tubadilishe sheria kwa sababu huyu mtu alikopa, akakubali kuweka dhamana ile nyumba, akishindwa kulipa iruhusiwe Benki iishike iiuze, biashara inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani nilisisitize hili ndani ya kuzungumzia Muswada unaohusiana na ardhi na makazi kwa sababu ni jambo nyeti, ni jambo muhimu na bila kufanya hivyo ni sisi Tanzania katika Afrika Mashariki tumebaki peke yetu na nadhani katika Afrika katika nchi chache zaidi na katika dunia ndiyo kabisa watu wanajenga nyumba kwa kutumia fedha zao, inakuwaje? Tutengeneze utaratibu wa kuwakopesha wananchi.

La mwisho, nasisitiza upatikanaji wa hati. Upatikanaji wa hati una matatizo makubwa, katika akaunti za mashirika mbalimbali na *Departments* za Serikali. Ukipitia utaoana kweli zina ma-*auditor* wanauliza *title* ya *asset* hii ipo wapi? Mashirika yana nyumba, Serikali ina nyumba hazina *title*. Sasa kama Serikali na Mashirika ya Serikali yanakosa *title*, mwananchi wa kawaida ataipataje? Hilo ni tatizo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Magufuli na dada yangu Mlaki, hili tatizo litengenezeeni utaratibu katika kanuni za utekelezaji wa sheria hii. Ijulikane kabisa ukishapata kiwanja hati inapatikana katika kipindi cha muda gani? Baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mada hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ila nadhani ulikuwa unasema Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Naibu wake sio dada yako na nani. *(Kicheko)*

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kushukuru sana kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja hii muhimu. Naomba na mimi nijiunge na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Mtutura kutoka kule Tunduru, lakini kwa sababu ni watani zangu, naruhusiwa kusahau anatoka wapi.

Vile vile nirudi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja na Naibu wake na watumishi walio chini yao. Huu Muswada kwa kweli umekuja kwa wakati muafaka, nausifu sana kwani umetoa madaraka hata kwetu sisi tunaokaa Vijijini.

Ningeomba sana nijielekeze kwa muda kuhusiana na upangaji wa matumizi ya ardhi ya Vijiji. Kule Rufiji kwa bahati nzuri tuna ardhi nzuri sana na misitu mikubwa sana. Tangu Wakoloni walivyoandika kwamba kule ni shamba la bibi, sasa hivi tunaita Hifadhi ya Taifa.

Hiyo Hifadhi ya Taifa tangu mimi ningali mdogo naambiwa usiingie huko, mwiko kuingia mpaka umri huu. Sasa watu wamezaliana, Wasukuma wameleta ng'ombe kule na ndugu zangu Wamang'ati siku hizi na sisi tunajifunza Kimang'ati. Ardhi hii iliyoambiwa shamba la bibi usiingie, bado inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaambiwa kuna mamlaka ya Halmashauri za Wilaya na Vijiji zinaweza kupanga upya. Kama jambo hili linawezekana kufanywa na mamlaka ya Wilaya tunashukuru. Kama haiwezekani, basi Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Taifa naiombea ichaguliwe haraka na wakae wakubali kwamba na sisi wa Rufiji sasa hivi tumekuwa wengi na ile mipaka mbele na sisi tupate ardhi kwa matumizi mazuri ya kujiendeleza katika kilimo. Kama nilivyosema, siku hizi watu wengi wakiwemo Wasukuma na Wamang'ati ili waendeleze ufugaji. Hii ni hoja muhimu, namwomba Mheshimiwa Waziri aichukue na aifanyie kazi.

Hii asilimia 60 nzima ya Rufiji ni hifadhi ya Selous. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri atuonee huruma. Tunataka ardhi ya kulima na kufanyia shughuli za ufugaji. Hoja ya pili inahusiana na Miji midogo. Miji midogo ya Wilaya imetangazwa muda mrefu.

Rufiji ina Mji wa Utete, Mji mdogo wa Ikwiriri na Mji mdogo wa Kibiti ambayo mpaka sasa hivi hakuna kinachoendelea. Mheshimiwa Waziri kitu gani kinachosimasisha utekelezaji wa hii miji midogo? Hiki ni kilio cha Watanzania wote.

Mji mdogo wa Utete ni mji wa zamani, wote mnafahamu kuwa vita ya Majimaji imepiganwa pale, ndiyo maana boma likajengwa. Sasa tunataka maendeleo pale. Wawekezaji wanakuja, wanataka kutengeneza pale kuwe na gati ya kufanya *boating* mpaka *delta* na mpaka Mloka. Wanataka kupanua kiwanja cha ndege, lakini ndugu wa Mipango Miji hawajatufanyia utaratibu mzuri, nusu tuko Kijiji, nusu Mji mdogo. Wengine wanataka kuwaingiza Wasomali kule. Tunasema hivi na sisi Utete tuendelee kidogo. Fanyeni haraka ili mtusaidie huyu Bwana anayetaka kuwekeza Utete aruhusiwe kuwekeza.

Hoja ya tatu ni utoaji wa ardhi kwa wananchi. Utakuta mamlaka inayotoa *offer* inaweza ikawa ya Halmashauri ya Wilaya, Manispaa kwa mfano Kinondoni hivi na wengine wanaweza kupata ardhi *offer* kutoka Wizarani. Matatizo ni makubwa, hawa watu wa Wilayani Kinondoni, kwa mfano wanafumbia macho ile iliyotolewa na Wizara. Hawatazamani, wanatoa viwanja upya. Basi anayepata taabu pale ni mwananchi.

Tunaloomba, kama ilivyokwishasemwa, kuwepo na ramani inayoonyesha kuwa Mtulia kapewa *area* hii. Sasa isionekane tena Afisa wa Manispaa ya Kinondoni au Temeke anatoa kiwanja kile kile tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana niupongeze Muswada huu hususan ukiangalia Ibara ya 42, isomeke pamoja na Sheria ya *Land Acquisition Act* na *Land Act* za 1969 na 1999. Hapa haki ya mmiliki imeelezwa vizuri na imerudiwa, kwamba kama ana *offer* ya ardhi na kama hajapata hati baada ya miaka mawili, hiyo *offer* inakuwa kamili.

Vilevile, kama ardhi hiyo inatakiwa kwa kubadilishwa kwa matumizi mengine, aandikiwe barua atie saini ya *dispatch book*, aitwe kwa majadiliano juu ya hiyo ardhi mnataka kufanyia nini? Kisha aridhie. Akisharidhia, kuna suala la gharama zilizolipwa kodi za kiwanja, halafu kuna suala la gharama kwa maana ya thamani ya kile kiwanja kwa bei ya soko. Hiyo ikiwa tayari, basi hakuna hoja.

Lakini mimi nina mifano mawili. Wa kwanza, mtu ninayemjua amepewa kiwanja mwaka huu wa nne au zaidi Manispaa ya Kinondoni katika Wilaya ya Kinondoni analipia mpaka leo, lakini hajapewa hati, badala yake, anasikia minung'uniko kuwa kiwanja hicho kitabadilishwa bwana, kitakuwa *play ground*, au itakuwa *garden*. Lakini sheria ipo, kwanini msimuite mmiliki na kumwambia maneno hayo, kwa kufuata sheria? Sasa hii inaleta hoja kubwa, kwamba tunalo tatizo la utekelezaji wa sheria zetu za ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri akubali kwamba lipo jinamizi linaloharibu mambo, linamziba Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu, huku chini watumishi wao wanajiendeshea mambo wanavyotaka. Mheshimiwa Waziri atuambie atatekeleza vipi Sheria hii, kwa sababu mpaka sasa maovu makubwa yaliyojitokeza ni mengi na hatuoni wahusika wanapewa adhabu, mathalan tuchukue mfano wa Madaktari. Daktari akikosea kweli kweli, hutangazwa, na cheti chake kinafutwa. Sijaona *Land Officer* yeyote aliyetangazwa kwa kazi ya *double allocation* au ya kuchukua mali ya watu bila taarifa zozote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge kama Sheria za kuwatangaza zipo Mheshimiwa Waziri azifufue na kama hazipo, basi aziandike katika *regulations* zake. Kuwepo na *seriousness* katika utendaji kazi. Wizara itapata heshima kama yupo mtekelezaji mzuri anayefanya kazi sawa sawa. Lakini jinamizi hili la ubinafsi linawakaba mno. Naomba Mheshimiwa Waziri aliondoe ili Wizara, sisi wananchi tupate haki zetu. *(Makofi)*

Kule Rufiji hali ni hiyo hiyo, nimeelezwa kwamba hao *Land Officers* wapo katika mamlaka ya Halmashauri, lakini mbona wanapata mishahara tunayoidhinisha hapa Bungeni? Kwa nini wasifuate Sheria za nchi katika kugawa ardhi na kuwapa wananchi haki zao?

Nataka kumaliza kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, kwanza ninakubali Miswada yote mitatu, ni mizuri, pili, ninakubali inatekelezeka mradi tu tuwe

na utaratibu wa kutekeleza, la sivyo, itakuwa tunachukua chupa mpya tunaweka mvinyo ule ule wa zamani, kutakuwa hakuna faida yoyote kwa wananchi.

Tatu na mwisho, ninaunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Juma Kilimbah na atafuatiwa na Mheshimiwa John M. Cheyo, sikuona orodha ya mwanamke yeyote.

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia niungane na wenzangu kama ulivyo utaratibu.

Kwanza nikushukuru wewe na pili niwashukuru Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Waziri John Magufuli na Naibu Waziri Mheshimiwa Rita Louise Mlaki pamoja na watendaji wao wote wa Wizara hasa kuleta Miswada hii mitatu muhimu mbele yetu na ili tuje tuipitishe kama Sheria.

Pia nimshukuru na kumpongeza jirani yangu Mheshimiwa Abdallah Mtutura kwa ushindi mzuri alioupata katika Jimbo la Tunduru na pia nikipongeze Chama Cha Mapinduzi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii tena niwapongeze wachangiaji wote waliochangia katika Muswada huu, kimsingi yote waliyoongea ni mambo nyeti na ninaamini kabisa kwamba ni mambo yanayowagusa wapiga kura wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia katika kuchangia zaidi ningependa nichukue fursa hii niombe ruhusa yako ninukuu maneno haya kupitia hiki kitabu cha Kiongozi cha Mwanakijiji, haya maneno yalitolewa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Aprili 25, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno haya ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu ni maneno mazito, naomba niyanukuu:

"Hatuwezi kushinda vita dhidi ya umaskini kwa silaha ambayo hatuna. Silaha ya uhakika aliyonayo kila Mtanzania ni ardhi. Kwa kutumia ardhi kama ardhi na ardhi kama mtaji, tunaweza kuushinda umaskini. Uwekezaji kwa sekta nyingine iwe madini, viwanda, utalii, biashara, miundombinu na kadhalika, unaweza kuwanyanyua wachache wakaondokana na umaskini. Lakini ardhi pekee ndiyo yenye uwezo wa kumnyanyua kila Mtanzania kwa pamoja aachane na umaskini." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu ni maneno mazito na hasa yanazungumzia hali ya Mtanzania jinsi alivyo maskini, kadhalika na michango yote ya Waheshimiwa Wabunge ukiangalia kwa undani hawapingani kabisa na Miswada hii na hasa huu Muswada wa matumizi ya ardhi. Lakini wasiwasi wao juu ya ardhi umekuwa ni juu ya namna ya wale wasimamizi wa Sheria yenyewe ambayo tunaweza tukaipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ili kweli tuweze kuondokana na umaskini na kweli Sheria hii ambayo leo hii naamini itapita ipo mbele yetu naamini itatekelezeka vizuri naamini kweli inahitaji usimamizi na isiwe ya ujanja ujanja ndani yake ambayo baadaye itaendeleza kuwafukarisha wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia kwa makini, nami nijikite kwenye Muswada wa Matumizi ya Ardhi na pamoja na kueleza kwamba Muswada unasema kwamba utakuwa ni *participatory*, lakini wakati nilipokuwa napitia baadhi ya maeneo na hasa nilipokwenda katika eneo la Muundo wa Utawala, nimejaribu kuyasoma yale maeneo kwa hatua moja hadi nyingine, lakini ukiangalia kwa undani unaweza ukakuta maeneo mengine yana mtego, ni kwamba hayashirikishi moja kwa moja jamii ya ngazi ya chini.

Mimi naishukuru Ibara ya 6 imempa mamlaka Rais kuunda hii Tume ya Taifa ambayo itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe watano, lakini sio zaidi ya kumi. Sasa ukiangalia majukumu yenyewe ya Tume yameelezwa katika Ibara ya 7, yamekuja (a) mpaka yanaishia (m), unaangalia haya majukumu yote yanaelekeza nguvu ya kiutendaji kwa Tume yenyewe, lakini sijaona eneo ambalo mtu wa chini anapewa nafasi ya kuweza kutoa maoni au mdau yeyote anayetumia ardhi kuweza kutoa maoni, kwa sasa hapa yote yanayoelezwa ni namna ya kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini moja ambalo nimeona pengine linaweza likatuletea mgogoro na hili katika kuchangia, Mheshimiwa Herbert James Mntangi amejaribu kuelezea na kuna kifungu hiki cha (k) kuhusu kuanzisha na kuendeleza mahusiano na nchi nyingine, mashirika ya kimataifa, masuala ya mipango na matumizi ya ardhi. Hii Tume ndiyo imepewa uwezo peke yake, inaweza ikashauriana na nchi nyingine.

Lakini Mheshimiwa Herbert James Mntangi alipokuwa anachangia alisema kwamba nchi yetu sasa hivi tupo katika *East African Community*, sasa tunakaa na tupo kwenye mchakato wa kuzungumzia shirikisho, leo mimi sikatai na hatukatai wawekezaji na tunakubali wawekezaji na kama tunavyosema, ili tuweze kujinyanyua kiuchumi tunakaribisha wawekezaji kama sera za nchi yetu zinavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo hili kama Tume peke yake inaweza ikatoa maoni au ikaamua juu ya matumizi ya ardhi, eneo lolote bila kushirikisha watu na hilo eneo likawa tayari limeshatolewa bado tunaweza tukawa tunakaribisha migogoro ambayo ipo mpaka sasa kama tunavyojionea katika baadhi ya sehemu migogoro ipo. Ukiangalia Tume ilipewa meno kwenye eneo hili lakini ukienda Ibara ya 8 ili kudhibitiwa mwananchi atakuwa hajashirikishwa. Kama itakuwa tayari mipango imepitishwa Ibara ya 8 inapendekeza kwamba Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iwe na Mamlaka ya kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na kushtaki Mahakamani ili kuhakikisha kuwa maagizo na maelekezo yake yanafuatwa kikamilifu.

Hapa amepewa mtu eneo na Tume, huku wananchi hatujawashirikisha kikamilifu. Sasa mwananchi akitaka kusema kwamba ni lazima hapa tuendelee kutumia hili eneo,

basi anaweza akashtakiwa na Tume. Hapa bado naona hii mitego mitego, nilikuwa napenda tu katika Muswada huu ili uweze kufanya kazi vizuri, ingeondolewa ili wananchi wetu basi waweze kufaidi rasilimali hii ya ardhi, waweze kufaidi kwa sababu hakuna mtaji wowote mwananchi maskini anaoweza kuwa nao isipokuwa ni hii ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba mambo mengi yamezungumzwa na wasemaji waliopita. Lakini niliwahi kusema katika kipindi cha Bunge lililopita la Bajeti namna ya ucheleweshwaji wa upimaji wa hii miji midogo hasa katika Jimbo langu la uchaguzi la Iramba Magharibi na nilitaja hii miji midogo Shelui, Misigiri, Kiomboi, Ndago na ukija katika Jimbo ninalopakana nalo la Iramba Mashariki katika eneo la Iguguno.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maeneo ambayo yamepanuka sana na sasa hivi upo mgogoro mkubwa sana wa matatizo ya mgogoro wa ardhi. Sasa Sheria itakapoanza kufanya kazi, namwomba Mheshimiwa Waziri tuhakikishe tunakwenda kupima maeneo hayo na kwa sababu wananchi wapo kila siku wanangoja kupata hizo hati na waweze kuhakikisha kwamba tayari wanaweza kwenda kuomba mikopo na waweze kujiendeleza katika kuondokana na hali ya umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa ni kwamba, yapo maeneo ambayo hayajapimwa, lakini maeneo haya katika Jimbo langu ni maeneo ambayo yana migogoro sana, ni maeneo ambayo yalikuwa ya asili.

Lakini Serikali kwa kupitia vyombo vyake, kuna eneo la Mikungu sehemu za Ndago. Hili eneo kumejengwa Magereza na limeanza kuwa na utata mkubwa kati ya wananchi kugombea ardhi na Jeshi la Magereza. Baadhi ya wananchi wanapigwa, wananyang'anywa mali na mifugo na Magereza. Kwa hiyo, nilikuwa naomba pia katika uainishaji na katika upimaji wa maeneo kama haya, migogoro hii midogo midogo tuhakikishe tunaitatua haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja hii asilimia mia moja hasa katika Miswada hii mitatu na naamini kwamba itafanya kazi na kuitakia mema nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa John Cheyo atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongela.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Miswada yote mitatu, lakini nitajikita zaidi katika Muswada wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utangulizi, nataka kusema kwamba ardhi tunayoizungumzia tayari ina watu, tayari tunailima, tunachunga na ndiyo Miji pale ilipo na juzi tumepitisha Sheria kwamba Ardhi ni mali, leo tunakuja na Sheria ambayo tunaipa mamlaka Tume, Kijiji, Wilaya na pia mtu mwingine yeyote atakayeamuliwa na Waziri kuweza kutawala ardhi au kutoa maamuzi juu ya matumizi ya ardhi.

Muswada huu ni mzito sana kwa wananchi. Ningependa kufahamu kama kweli Mheshimiwa Waziri amefanya kile ambacho Wazungu wanasema ni *impact assessment* ya Muswada huu. Muswada huu utageuza maisha ya watu wetu kwa kiasi cha namna gani? Katika nchi hii tumekuwa na maamuzi mengi sana juu ya watu na mara nyingine hayana matokeo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyokumbuka, mwaka 1964 tuliamua nchi hii tuwe na *block farms* kila mahali mashamba makubwa makubwa, tukahamisha watu, tukaondoa watu katika makazi yao, mwishoni hilo jambo halikufanikiwa na watu waliteseka sana. Mwaka 1974/1975 tumekuwa na mpango wa Vijiji, tukahamisha watu kwenye Vijiji, wengine tukachomea nyumba zao na wengine walikuwa wanawekwa tu hata kwenye mbuga huko, wengine wameliwa na simba kwa maamuzi ambayo yalifanyika na watu wengi walihangaika sana.

Ni miaka sasa karibu 32, leo tena tunakuja na Muswada wa matumizi ya ardhi na tunatoa mamlaka kwa Kijiji, *Village Council*, *District Council*, *National Commission* yaani Tume na mtu mwingine ambaye Waziri ataona kwamba atafaa. Hivi tumejiuliza kwamba kutatokea nini kwa watu ambao wamezoea kutumia ardhi kwa mambo mbalimbali?

Kwa mfano ukiangalia *Section 28* inatoa mamlaka kwa Tume kuamua matumizi ya ardhi, matumizi kwa ufugaji, kwa ajili ya vyanzo vya maji na kadhalika. Tume ikiamua kwamba ardhi yote ambayo Wamasai wanayo itakuwa ni ardhi ya wakulima, maana yake nini kwa Wamasai? Kwani *Maasai Land* ni mahali pa kuchunga na kwamba yeye tangu amezaliwa anajua kitu kimoja tu kwamba ni ng’ombe, maziwa na nyama na kuchunga kadhalika na Msukuma pia. Maana yake nini tunapotunga Sheria hii na tunaiwekea adhabu, tunasema kwamba kama usipofuata hii *Sheria Section 68* inatoa adhabu ya Shilingi milioni mbili, ndiyo maana yake. Ndiyo kusema kama wewe mchungaji Mmasai ukiingia katika sehemu ambayo haijatajwa ambayo ni ya kuchungia maana yake utapewa adhabu ya Shilingi milioni mbili, tumewatayarisha namna gani Wamasai kuweza kweli kujifunza kwamba sasa Tanzania imegeuka, ni Tanzania ambayo kama wewe umepangiwa ekari 20, basi unachungia kwenye ekari 20 tu?

Mimi napata wasiwasi, hatujafanya maandalizi ya kutosha na ndiyo kusema Sheria hii kama itaanza mara moja watu wengi watapata shida sana! Siyo kwamba hatuna historia ya watu kupata shida, kwani juzi tu hapa tumeamua kwamba, sehemu ya Mbarali kule ni chanzo cha maji, kwa hiyo, wafugaji wote ni lazima wahamishwe ili tupate maji Mtera. Lakini kwa bahati mbaya Mwenyezi Mungu ametuumbua, bado hatujahamisha mifugo yote Mbarali, bado hatujawatengenezea mahali pa kwenda pamoja na watu wengine kupigwa faini mpaka Shilingi milioni 60, sijui Sheria hiyo ipo wapi? Mungu katuonyesha kwamba tatizo letu la kujaza Mtera haikuwa ni ng’ombe kule Mbarali, lakini tatizo letu lilikuwa ni ukame. Hatujapata maji na mvua ya kutosha, sasa leo Mtera inatapika na ng’ombe bado wapo huko huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini watu wamepata shida, ng'ombe wanapelekwa Lindi ambako hakuna matayarisho, watu hawajajua kwamba baadhi ya majani hayaliwi na ng'ombe ambao wametoka *Sukuma Land*, hakuna Minada iliyoandaliwa, hakuna majosho yaliyoandaliwa ni shaghalabaghala, lakini uamuzi umefanywa. Sheria hii inaashiria kwamba tutaendelea huko huko.

Siyo hivyo tu, sasa hivi tumeingiliwa na homa ya mazingira. Mwenyezi Mungu ametupa ardhi, ametupa mazingira yetu tuyatawale na imo ndani ya Maandiko Matakatifu. *Management of the Environment* siyo tu kutunza, siyo tu *preservation*, nataka kutofautisha mambo mawili, yaani uhifadhi na *Management*, leo tunaanza kupata Sheria ya kila aina.

Juzi hapa nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa mmoja alikuwa anatoa amri kwa Waluguru kwamba, nataka Waluguru wote mteremke kutoka mlimani mje chini. Chini kwenyewe hakujaamuliwa ni chini gani na ni sehemu gani watakwenda Waluguru. Mluguru miaka yote, tangu mimi nazaliwa yupo kulekule mlimani, leo unasema teremka kwa amri sijui ya Waziri, *Village Council, District Council*, Tume na kadhalika. Hao ni Waluguru na wa Rungwe je? Kesho utawaambia wa Rungwe wote teremkeni chini! Wachaga je? Kesho utawaambia Wachaga wote teremkeni chini! Wasambaa nao je? Kesho utawaambia Wasambaa wote teremkeni chini! Ni kila siku utawaambia teremkeni chini? Ni amri za mara moja na zaidi kwa kasi mpya hii ni kesho, kesho kasi na nguvu, tutafika wapi? Muswada huu tutafika wapi? *(Makofi)*

Wito wangu ni kwamba huwezi ukakataa kupanga, lakini sijaona hapa nafasi ya mtu. Watu wanafikiria tu kwamba ardhi iko pale yaani ipo wazi tu, leo watu kila mmoja ana shamba lake, unapomwambia huyu mtu wa Kijiji kapange, akapange nini? Aniondoe kwenye shamba langu aweke nini? Tayari inaanza kutupa matatizo! Juzi hapa tumeanza kujenga Sekondari, kuna watu wengi sana Vijijini leo wananyang'anywa mashamba bila fidia na Shule yenyewe ni ya Kijiji, bila fidia anaambiwa tunaweka Sekondari hapa na wanalia tu wala hakuna utaratibu ambao kweli utamsaidia mkulima mnyonge mmoja mmoja aweze akafika mahali pa kupata haki. Hiyo ni Sekondari.

Leo hii unaweka mamlaka makubwa makubwa, sijaona katika Sheria hii ambapo mipango inayopangwa, kwanza, ni mipango ya miaka mingapi? Mbona hiyo mipango kama ni mikubwa hairudi Bungeni? Ningefurahi zaidi kuona hiyo *National Land Use Planning Commission* kama ingetengeneza mipango ikaileta Bungeni tukakaa na tukakubali kwamba tangu leo iliyokuwa inaitwa *Masai Land* sasa hivi ni *Ranch*. Sasa Mlima Kilimanjaro ambao Wachaga wanaishi sasa hivi ni Hifadhi ya Taifa na wote teremkeni; sasa hivi Waluguru wanaoishi katika Milima ya Uluguru sasa sisi tunakubali teremkeni wote! Mimi naona kuna haja katika Serikali kuamua kuwa na *coherence*, yaani uwiano wa maamuzi, naona kama kuna maamuzi hili linaamuliwa hivi na hili linaamuliwa vile, hakuna mtu anayeweka maamuzi haya pamoja na kusema kwamba maamuzi haya tukiamua hivi itatokea nini. Leo hii maamuzi ya kupenda misitu yanaleta hata hisia za kikabila, watu wanaanza kuishi pamoja, hata leo katika Bunge mtu anaweza kusema Wasukuma wamekuja Rufiji, leo hii kuna sehemu nyingine ambazo watu wameanza kugawanyika, mtu akionwa na ng'ombe, basi ataambiwa huyu ni Msukuma.

Leo hii kuna sehemu nyingine ambazo watu wameanza kugawanyika, mtu akionwa na ng'ombe, basi ataambiwa huyu ni Msukuma au Mmang'ati au Mmasai, tutaishi vipi?

Sasa hivi inaonekana kuna uhusiano ambao ni wa kuchukia ng'ombe na ndiyo maana Mwenyezi Mungu katuletea *Rift Valley* kutuonyesha kwamba mimi nakukabidhi mali halafu wewe unaichezea jinsi unavyotaka!

Kuna haja ya kuwa *serious* katika Serikali kwamba Sheria tunazozitengeneza na zaidi sheria ambazo zina-*affect* maisha ya watu, ambazo zinahusu maisha ya watu, zinazohusu mali za watu kweli zinaangaliwa kwa undani na kuona kweli kwamba hata adhabu tunazotoa ni adhabu ambayo atalipa nani? Unapoweka adhabu ya shilingi milioni mbili, ni nani atalipa hiyo shilingi milioni mbili? Au unataka kujaza tu Magereza kwa sababu labda naambiwa siku hizi ndani ya Magereza kuna *TV*, basi watu wote waende wakamwone Waziri Mkuu akihutubia, kwa hiyo, watu wote unawaweka ndani ya Gereza? Nani atalipa?

Kwa hiyo, vitu vyote hivi ni vya maana sana ila mimi nasititiza kwamba kabla hatujafika huko na vizuri ni kwamba Waziri amepewa nafasi ya kuweza kuuangalia huu Muswada. Kabla huu Muswada haujaanza kutekelezwa, ningependa kwanza elimu itolewe, hebu tuwaeleze wananchi kinagaubaga, maana ya Sheria hii katika maisha yao ni kitu gani na *Village Council* ili mtueleze mipaka yao ipo wapi? Humu imeandikwa kuamua tu na maamuzi yapo makubwa sana, hakuna mipaka na mkulima mmoja mmoja tunamlinda namna gani?

Sasa hivi wananchi wetu wa Tanzania ni *vulnerable,* mateso wanayopewa na *WEO* na *VEO* ambao hata zile shida hawazifahamu ni makubwa kweli kweli. Sasa leo mzigo kama huu tunauongeza na tunawapa watu nafasi ya kuweza kugandamiza watu wetu, mara nyingine tujiulize, hivi waliotuchagua ndiyo kweli watatuchagua tuje tutunge Sheria za kuwagandamiza zaidi au tutunge Sheria za kuweza kuwasadia? Haya ni lazima tujiulize. Sheria hii ni gandamizi, Sheria hii najua kupanga ni vizuri, lakini najua itapita kwa sababu Bunge lenyewe linajulikana lilivyo, lakini haitusaidii kutatua tatizo letu muhimu, yaani tatizo la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikubaliani na Muswada huu na ninataka iwe *recorded* hivyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Msemaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Mongella.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya mwisho usiku wa leo na mimi niweze kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda nikupe wewe salamu na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili kutoka kwa wananchi wa Wilaya ya Ukerewe ambao nilikuwa nao kwa kitambo katika kipindi kabla hatujaja Bungeni, wanasema

msiwe na wasiwasi wanaongeza juhudi za kuvua samaki ili msije mkaathirika na *Rift Valley Fever*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba nichangie Muswada huu. Kwanza, ardhi ni kitu katika historia ya wanadamu, imeleta furaha, imeleta maendeleo, lakini pia ni kitu ambacho kimeleta vita katika maeneo mengi.

Kwa hiyo, tunapozungumza ardhi tuliyopewa bure na Mwenyezi Mungu ni lazima tuzungumze kwa heshima kwa sababu au tunaweza kupata faida kubwa kutokana na kile tunachokifanya au kukipanga kama binadamu au tunaweza tukajiletea matatizo ya kudumu.

Kwa mfano, tunayo matatizo kama ya Zimbabwe, wenzetu matatizo makubwa ni ardhi na matumizi ya ardhi. Ipo mifano mingi tu *the Golan Heights* ni sehemu moja duniani inaleta matatizo katika matumizi yake na kila mtu anaigombania kwa sababu tu ni sehemu iliyo na maji ambayo ni rasilimali kubwa kwa maeneo hayo ya jangwa. Ipo mifano mingi tu hapa duniani ambapo watu wamekosa kuelewana kwa sababu ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaiunga mkono miswada hii huu kwa matumaini kwamba tunachokifanya leo itakuwa ni mwanzo wa kupanga vizuri matumizi ya ardhi ili tusije tukafika mahali tukapata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa niseme kitu kimoja. Kuna hatua moja sikuiona vizuri sana katika Muswada huu au kama ipo haikujieleza vizuri. Ukitaka kupanga ardhi na matumizi yake lazima kwanza uwe na picha za anga zinazokuonyesha milima ipo wapi, mito ipo wapi, mabonde yapo wapi na maziwa yapo wapi na kwa sasa hivi katika nchi yetu, hizo ramani zilikuwepo za mwanzo kabisa kabla hatujawa na watu wengi kama tulionao sasa. Lakini mpaka sasa hakujafanyika tena vipimo vya aina hiyo. Kwa hiyo, katika *Land Use Planning* kutakuwa na tatizo kubwa la kupanga tukiwa kwenye meza bila kujua kilichopo katika eneo ni kipi ama bila kujua uwiano wake na sehemu nyingine ni upi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano, ukichukua mbuga ya Serengeti, Mungu alivyoiumba alikuwa ameruhusu wanyama wale wazunguke na wana njia zao za kuhama ili kuweza kuendeleza uhai wao, walikuwa wakienda mpaka kufikia sehemu iliyopo katika Wilaya ya Bunda Pwani ya Ziwa Victoria. Kwa matumizi mabaya na kwa kutopanga sasa hivi maeneo hayo yamekuwa ni makazi ya watu bila mpango wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba, kwa sheria hii wale watakaohusika watayaangalia na maeneo hayo. Baada ya miaka michache ijayo kama *interference* ya *immigration* ya wanyama itaendelea kuwepo Serengeti labda itakuwa ni makazi ya watu badala ya kuwa ni *National Park*. Sasa nimetoa huo mfano kwamba ni vyema tukajua ramani ya nchi yetu, vilivyomo na mahusiano yake na sehemu nyingine. Ukiwa Ziwa Victoria, pale Pwani katika Wilaya ya Bunda huwezi kuona uhusiano wa eneo hilo na wanyama wa Serengeti na hivyo hivyo hata kwa binadamu. Nitawapa mfano, Wilaya ya Ukerewe nadhani ilikuwa ni *best land planners*. Tuna visiwa ambavyo

kulikuwa na maeneo maalumu ya kuchunga wanyama, kulikuwa na maeneo muhimu ya makazi ya watu na maeneo maalum yanayojulikana kwa kila mtu kwa ajili ya uvuvi. Lakini sasa hivi vurugu ni nyingi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, usiwe unakatisha kati ya Naibu Spika na msemaji.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Sasa ukiangalia visiwa wakati vinasimamiwa na wenyewe, mila na desturi zilikuwa zinatawala. Kwa hiyo, hakukuwa na uharibifu wa mazingira kwa sababu kila mtu alijua avue wapi na kila mtu alijua mifugo inakaa wapi. Kwa hiyo, kuna maeneo maalum ambayo lazima yaangaliwe, siyo kwa sababu tu ya sheria hizi tulizonazo, lakini pia ziangalie mila na desturi za watu wanaoishi katika maeneo hayo.

Nikichukua mfano wa Wamasai, tunawaona Wamasai wetu kwa mipaka tuliyowekewa. Eneo lote mpaka Umasaini Kenya ni eneo la kwao na matambiko yao yapo katika ukanda huu wote, wanafanya matambiko yao na hili tusilipuuze, wana mikutano yao ambayo inahitaji mahali maalum pa kuabudu na yapo maeneo mengi hata kwenye *National Park* ya Selous. Nadhani Wangoni na makabila ya Kusini wana matambiko yao na nilipokuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mzee Rashid Kawawa aliniomba rasmi kuruhusu zile njia wapite wakafanye matambiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nategemea kwamba watakaopewa jukumu hili hawatatufanyia mahesabu ya kusema mbili kujumlisha mbili ni nne; watakuwa ni watu wenye uelewa wa kila kuweza kujua mahusiano ya sehemu moja ya ardhi na sehemu nyingine ili wasikiuke taratibu za wanadamu wanaoishi katika maeneo hayo na wala wasifike mahali wakaharibu mazingira kwa sababu tu labda ya watu kuweka shinikizo la kutaka sehemu hiyo itumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni sehemu maalum kama za madini, tusipoziwekea alama mapema, mtu anaweza kutoa shinikizo la kutaka kuwekeza katika sehemu hiyo alime mihogo kumbe akijua chini kuna dhahabu. Kwa hiyo, kuna haja ya kuhakikisha kwamba tunajua vitu vyote hivi kwa kina kwa kutumia sheria hii na tunapofanya *Land Use Planning,* yule ambaye atasimamia shughuli hii ataisimamia kwa kuangalia haya yote ili baadaye tusije tukajuta kwa matumizi mabaya ya ardhi tukitumia sheria ambayo tumeitunga wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu sasa ambavyo ningependa niviongeze kwa kuboresha. Nakubaliana kabisa na mawazo ya wenzangu Waheshimiwa Wabunge ya kusema kwamba lazima nafasi ya Bunge iwepo katika kuangalia *Land Use Planning* isije ikawa ni suala tu la *commission* ambayo ikiangalia ikisharidhika, basi mambo yanaendelea na Bungeni tunabaki ni watu wa kulalamika na ku-*react* kwa sababu watu wa *Commission* hiyo hawakufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba pia niseme kwamba katika kutengeneza *Commission,* bado ninapata shida sana ya mawazo ya kale ambayo yanaonyeshwa katika

Muswada huu. Kwa sababu mawazo ya kale ni yale ya kuona kwamba wanawake ni nyongeza, inasema angalau wanawake watatu.

Sasa mimi nikisoma maeneo yaliyotajwa ambako hao Wajumbe wanapaswa kutoka, ni wapi ambako hutakuta mwanamke mpaka upate kigugumizi cha kusema iwe nusu kwa nusu? Ni wapi? Ni katika Wizara ya *Planning and Development* hakuna wanawake! Katika *Energy and Mining, Environmental, Finance, Health, Industry, Local Government, Natural Resources and Fisheries, Water Sources, Non Governmental Organization*! Kigugumizi hiki si mawazo ya kizamani hayo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unapaswa kusema iwe wanawake nusu kwa nusu kwa sababu katika Wizara zote na maeneo yaliyotajwa sasa hivi tuna wanawake ambao wana uwezo wa hali ya juu kuliko kuendelea kuweka ukiritimba wa *gender bias* ya kwamba *the male is powerful. I am sure with having demonstrated enough, the female is the best.* Kwa hiyo, iwekwe nusu kwa nusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono, lakini ile nusu kwa nusu iwekwe. Hakuna sababu ya ku-*demonstrate* mawazo ya kale katika sheria tutakayoitumia katika miaka inayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa niliseme ni kwamba, nilipokuwa nazungumza na wanavijiji na hili limesemwa na wengine, mawazo ya kusema ni vyema elimu ikatolewa, Mheshimiwa John Cheyo amelisema vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa nazungumza na wananchi Vijijini, Mabaraza ya Ardhi, wamenituma wapewe elimu, hawawezi kuendesha Mabaraza ya Ardhi bila kuwa na elimu ya kutosha ya kuhusu sheria zinazohusiana na ardhi.

Kwa hiyo, mimi nalifikisha hapa kwenu na kama hivyo ndivyo kwamba Mabaraza hayajapata elimu ya kutosha, basi *Land Use Planning* itabaki ni kugawa vipande vya ardhi kati ya watu na watu ama watumiaji au makundi ya watumiaji na haitakuwa *Land Use Planning*. Kwa sababu *Land Use Planning* ina *requirements* fulani za kusema hapa sasa tutatumia ardhi hii namna hii.

Sasa kama utaalam huo haupo kwa wanavijiji, zaidi sasa wanavijiji wataambiwa megeni hii ardhi, tunataka kuweka kiwanda. Kwa sababu wao hawatakuwa na upeo, watakubali kugawanya na katika kufanya hivyo, watapata matatizo ya kuvuruga ardhi badala ya kuitengeneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi suala ninalotaka kumalizia kubwa zaidi ni hili la kuheshimu wananchi wanaoishi katika maeneo hayo. Sisi tunaoishi Visiwani tunajua maana ya ardhi na ufinyu wa ardhi unaweza hata ukavuruga *Land Use Planning*. Kwa hiyo, kuwasikiliza wananchi katika hii *commission* ni suala la muhimu sana ili tuweze kusonga mbele na kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninaposema wananchi, ni wanawake na vijana, kwa sababu mara nyingi inapopangwa ardhi, vijana sijui watasimama wapi? Huwa hatuwazungumzii na hao ndiyo wanahitaji ardhi kuliko sisi wazee ambao tunamalizia muda. Kwa hiyo, *concept* ya vijana katika ardhi lazima iwepo.

Je, watoto hao wanaomaliza Darasa la Saba kila mwaka, tuna mpango gani katika *Land Use Planning* ya kuhakikisha kila mwaka na wenyewe wanajipatia ardhi kama ardhi ndiyo mtaji mkubwa? Akinamama katika *Land Use Planning* tutahakikisha namna gani shughuli za akinamama ambazo zinahitaji ardhi zinapewa ardhi na kwamba ni sehemu ya mkakati wa *Land Use Planning?*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Muswada huu wa *Land Use Planning* na niutakie mafanikio mema ukizingatia *is fifty, fifty* sio wanawake watatu kwa wanaume saba. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa michango yenu mliyotoa leo na huyu ndiye alikuwa msemaji wa mwisho kwa wale walioomba. Kwa sababu hiyo, tunapanga kwamba Waziri na Naibu Waziri wake wakajiandae vizuri kuweza kujibu hoja zilizosemwa na Waheshimiwa Wabunge kuanzia asubuhi. Kwa hiyo, kesho asubuhi, baada ya kipindi cha maswali, itafuata shughuli nyingine, lakini kwa Muswada huu tutamwita Naibu Waziri, halafu Mtoa Hoja, halafu tutaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima na kupitisha. Halafu tutakuwa na Miswada itakayoonekana katika *Order Paper* kesho. Kwa hiyo, naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi.

(*Saa 01.18 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 12 Aprili, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*